# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 16 Mei, 2025

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi za Wizara ya maliaislina Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 330

### Ujenzi wa Kituo cha Afya Namwanga – Masasi

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Namwanga baada ya Halmashauri ya Masasi kuanza ujenzi huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Namwanga kinajengwa kwa fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Masasi

ambapo kimeanza na ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD),* mpaka sasa Halmashauri ya Masasi imetoa shilingi milioni 100 na ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Masasi imetenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)* na Serikali Kuu itapeleka fedha za ujenzi wa majengo mengine katika Kituo cha Afya cha Namwanga, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali madogo mawili za nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kituo hicho kikikamilika kitawezesha kutoa huduma za afya katika kata nne ikiwemo Mpindimbi, Nanjota na Mijelejele; je, Serikali haioni haja ya kuharakisha mipango yake ili kuisadia halmashauri?

Swali la pili, Kijiji cha Chipingo kilichopo Kata ya Namwanga wananchi wake wanapata huduma mbali ambapo wanatembea zaidi za kilometa 60 na mwaka jana akina mama wawili walijifungulia darajani, je, Serikali imepanga kupeleka shilingi ngapi kusaidia juhudi za halmashauri katika ujenzi wa kituo hicho cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Namwanga ni kituo ambacho kitahudumia kata takribani nne zinazozunguka kituo hiki cha afya na ni kituo muhimu sana kwa wananchi wa Jimbo la Lulindi, Halmashauri ya Masasi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Hokororo kwamba baada ya halmashauri kutenga fedha na ujenzi kuendelea, tayari Ofisi za Rais, TAMISEMI tumekiweka kwenye mpango wa Mfuko wa Dunia kwa maana ya *World Bank* kwa ajili ya kupeleka fedha mapema iwezekenanvyo kujenga majengo mengine yanayobaki ili kiweze kutoa huduma zote za msingi za kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na zahanati hiyo, kwanza niwapongeze wananchi wa kijiji hicho kwa kuchangia nguvu zao kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya na niwahakikishie kwamba Serikali hii wa Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka minne imejenga na kukamilisha maboma ya zahanati zaidi ya 980 yakiwemo maboma katika Halmashauri ya Masasi.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie tu kwamba fedha zitapekewa kwa ajili ya kumalisha zahanati hiyo ili iweze kuanza kutoa huduma na kuondoa adha ya wananchi kusafiri umbali mrefu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa kukamilisha Vituo vya Afya Nangara na Singe? Singe ilikuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais, ni lini fedha hizi zitafika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Nangara tayari kimewekwa kwenye mpango wa Benki ya Dunia na Bahati njema Mheshimiwa Gekul tumewasiliana mara kadhaa, lakini pia tunafahamu Kituo cha Afya cha Singe ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na kama ilivyo utaratibu wa ahadi za viongozi wakuu, ahadi za Mheshimiwa Rais ni kipaumbele namba moja katika utengaji wa fedha kwa ajili ujenzi wa vituo hivyo.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Gekul kwamba vituo vyote hivyo vya afya tayari tumeviweka kwenye kipaumbele na mpango wake ni kupata fedha mapema iwezekanavyo kwa ajili ya kuvijenga ili vianze kutoa huduma hizo kwa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, lini Serikali itapeleka pesa katika Kata ya Ibumu iliopo katika Wilaya ya Kilolo kwa sababu wanatembea umbali mrefu sana kufuata matibabu zaidi ya kilometa 40 na hata Kata ya Mlafu jirani yao pia hawana kituo cha afya? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali iliweka utaratibu wa kujenga vituo vya afya katika kata za kimkakati ambazo zinakidhi idadi ya watu wasiopungua 10,000 lakini zenye umbali mkubwa wa kutoka kwenye kituo cha jirani zaidi cha huduma za afya. kwa hiyo, ikiwa kituo hicho cha kata hiyo inayotajwa na Mheshimiwa Mbunge inakidhi vigezo hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutafanya mawasiliano na halmashauri ili tuanze kutenga fedha kwa awamu kwa ajili za ujenzi wa kituo hicho cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka.

Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Oran Manase Njeza.

Na. 331

**Kupandisha Hadhi Barabara za Jimbo la Lupa**

**MHE. ORAN M. NJEZA K.n.y. MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itazipandisha hadhi Barabara ya Isenyela - Sangambi - Lupa - Lualaje na Chunya Godima - Sangambi kuwa chini ya *TANROADS?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, suala la kupandisha hadhi barabara ni la kisheria kwakuzingatia vigezo vilivyowekwa. Ikiwa kuna barabara ambayo inakidhi vigezo kutoka daraja la barabara ya wilaya kwenda daraja la barabara ya mkoa inatakiwa barabara hiyo ijadiliwe kwenye Kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa husika na ikionekana inakidhi vigezo ndipo bodi hiyo kupitia Mwenyekiti itamshauri Waziri mwenye dhamana na barabara kuwa barabara husika imekidhi vigezo vya kuwa na hadhi ya barabara ya mkoa na hivyo ipandishwe daraja na kuwa barabara ya mkoa chini ya *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, *TARURA* kwa kushirikiana na Bodi ya Barabara ya Mkoa itaanzisha mchakato wa kuzipandisha hadhi barabara hizo katika mwaka 2025/2026 ili ziweze kuwa chini ya *TANROADS*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, kwa kuwa barabara hizo zimeharibika sana na mvua zinazoendelea Wilaya ya Chunya, je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kurekebisha barabara hizo?

Swali la pili, je, ni lini Serikali itazipandisha Barabara za Ruanda, Sapanda mpaka Msituni ziliopo Wilaya ya Mbeya Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiwa inaendelea na taratibu ya kuzipandisha hadhi Barabara hizi za Isenyela - Sangambi - Lupa - Lualaje na Chunya Godima mpaka Sangambi, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuzikarabati barabara hizi. Kwa hiyo, katika mipango ya Serikali tayari kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili za kuendelea kuzihudumia barabara hizi na pindi zitakapopandishwa hadhi kwenda katika hadhi ya mkoa na kuanza kuhudumiwa na *TANROADS* basi angalau kwa kipindi hicho zinakuwa tayari zinaendelea kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili, kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu ya msingi kwamba mchakato wa kupandisha hadhi barabara kutoka barabara za wilaya zenye hadhi za wilaya ambazo zinahudumiwa na *TARURA* kuzipeleka kwenye hadhi ya mkoa na sasa zitahudumiwa na *TANROADS* kuna mchakato ambao unaanzia katika Bodi ya Barabara ya Mkoa.

Kwa hiyo, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Oran Njeza tutaanzisha mchakato huo katika ngazi ya kimkoa kwenye Bodi ya Barabara na kupeleka na kuwasilsiha mapendekezo kwenda kwa Waziri wa Ujenzi kwa ajili ya hatua ya kuweza kuzipandisha hadhi barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge sasa kuanza kuhudumiwa na *TANROADS* na kuwa na hadhi za kimkoa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Kikao cha Barabara cha Mkoa wa Kilimanjaro kilishapitia hatua zote na kupendekeza barabara ambazo zinatakiwa kupandishwa hadhi; je, ni lini sasa Serikali itamalizia mchakato huo wa

kupandisha barabara za Mkoa wa Kilimanjaro lakini zikiwemo za Wilaya ya Hai? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Bodi ya Barabara za Mkoa wa Kilimanjaro imefanya mchakato wa kuweza kubaini ni barabara zipi ambazo wanaona zinastahili sifa ya kuweza kupandishwa hadhi kutoka barabara za wilaya kuwa na hadhi ya barabara za mkoa na kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu ya msingi, kwamba baada ya Bodi ya Barabara kuwa imepitisha na imefanya mchanganuo na kuzibaini barabara hizi, basi mapendekezo yanawasilishwa Wizara ya Ujenzi na baada yah apo Wizara ya Ujenzi inaendelea na mchakato wa kuziidhinisha nakuzipandisha hadhi kuja sasa katika hadhi ya barabara za mkoa.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi tutaendelea kuwasiliana na wenzetu ili kuona wamefikia wapi katika hatua ya mwisho ambayo sasa ni ya kuidhinisha maombi ambayo yameletwa na Mkoa wa Kilimanjaro kwenye barabara hizi ambazo zitoke wilaya ziende katika ngazi ya mkoa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu sasa aulize swali lake.

Na. 332

**Kupandisha Walimu Madaraja kwa Msererko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapandisha madaraja kwa mserereko walimu wenye changamoto ya kupandishwa madaraja wakiwemo walimu wa Kakonko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Deus Sangu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 6(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura, 298 jukumu la kuwapandisha vyeo watumishi ni la mwajiri husika. Jukumu hili hutekekelezwa baada ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutoa mwongozo kuwataka waajiri kuandaa na kuwasilisha ikama na bajeti ya mwaka husika wa fedha na Ofisi kuridhia utekekelezaji wa bajeti hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/2025 Serikali imetoa mwongozo unaohusu upandishwaji vyeo na ubadilishaji kada ikiwemo na kwa watumishi waliocheleweshwa kupandishwa vyeo. Hivyo, nitoe wito kwa waajiri wote nchini kutekeleza kwa wakati mwongozo huo ili kuepusha malalamiko kwa watumishi wa umma wenye changamoto za kupandishwa vyeo wakiwemo watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza ninaishukuru sana Serikali kwa majibu, lakini nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya hasa ya kuangalia watumishi na kuwapandisha vyeo na kuwalipa stahiki zao. *(Makofi)*

Swali la kwanza, wapo walimu walioajiriwa mwaka 2013 katika Wilaya ya Kakonko lakini hawakupandishwa madaraja kama walivyostahili. Nini kauli ya Serikali kuhsuiana na walimu hao ambao hawakuweza kupata madaraja yao kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ninayo orodha ya watumishi wa Wilaya ya Kakonko ambao walishawasilisha majina na maombi kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri, lakini hawajaweza kushughulikiwa, je, yupo tayari nimkabidhi orodha hiyo ili imsaidie katika kuhakikisha kwamba watumishi hao wanapata stahili zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mwalimu Aloyce Kamamba kwa kufuatilia stahiki za walimu na masuala yote yanayohusu walimu nchini.

Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali yake mawili ya nyongeza kwamba kuna walimu mwaka 2013 walioajiriwa mwaka huo kwamba hawakupandishwa vyeo, ni kweli na siyo wote, mwaka 2013 kuna baadhi yao na katika zoezi hili tayari walimu wapatao 48,189 wameshapandishwa vyeo. Hata hivyo naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali tayari imeshatoa waraka kuwataka Wakurugenzi wote wa Halmashauri wahakikishe kuwa kabla ya mwisho wa mwezi huu walete majina ya watumishi walisahaulika, na siyo walimu tu ni watumishi wote wa umma wanatakiwa kutufikishia taarifa zao ili kabla ya mwaka wa fedha kuisha tuwe tayari tumewapandisha madaraja kulingana na walivyostahili kuwa, lakini orodha hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge unayo nakukaribisha, utaileta ili tuweze kuifanyiakazi kwa kuwa tayari utakuwa umeturahisihia kazi ya kuleta na pia katika Manispaa ya Kigoma Ujiji changamoto hii ni kubwa. Nitoe rai pia kwa Mkurugenzi ahakikishe orodha hiyo anaileta kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, katika mwongozo huo ambao mmeagiza wakurugenzi walete kwanza imechukua muda mrefu na walimu wengi pamoja na wafanyazi wengine waliojiendeleza wenyewe kielimu mmekataa kuwahamishia katika kile kipya walichokisomea ijapokuwa wamejilipia wenyewe.

Ni lini Serikali sasa mtaona umuhimu wa walimu waliojisomesha basi muwapandishe madaraja kwa kutumia kile walichokiongeza katika elimu yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna baadhi ya walimu waliojiendeleza na sio kwamba Serikali imekataa kuwafanyia *recategorization,* hapana, ni kwamba waajiri wao hawajaleta taarifa hizo ili tuweze kuzifanyia kazi, kwa hiyo naomba pia niendelee kutoa maelekezo au nitoe rai kwa Wakurugenzi wote kama kuna walimu au watumishi wa aina hiyo walete hizo taarifa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumi wa Umma na Utawala Bora nao wataingia kwenye orodha hii kabla ya mwaka huu wa fedha watafanyiwa *recategorization*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu wakati hilo linafanywa liangaliwe pande zote, maana ikitoe kila mtu alipo anaenda kusoma kitu kingine wakati aliajiriwa na kazi nyingine, sasa uko darasani atabaki nani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani muyaangalie kwa mapana yake maana vinginevyo kila mtu ataenda kwenye mrengo anaotaka halafu tutajikuta kuna kada tunakosa kabisa hao watu ambao watafanya hiyo kazi. Kwa sababu watu pia wajiendeleze katika maeneo yao ambayo Serikali wameajiriwa kwa ajili ya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 333

**Kuanza Kwa Mradi wa Maji wa Mto Rufiji**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Mto Rufiji utaanza baada ya upembuzi yakinifu kukamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa niaba ya Wizara ya Maji, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, Serikali inaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi mkubwa wa kutoa maji Mto Rufiji ambao utanufaisha wakazi wa Mikoa ya Lindi, Pwani na Dar es Salaam. Usanifu huo unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2024/2025 na Serikali itaanza kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jibu la Serikali limeonesha matumaini ya kukamilika upembuzi yakinifu wa mradi huu wa kuyatoa maji Mto Rufiji; na kwa kuwa ni maono ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan; na kwa kuwa Serikali hii imejaliwa ubunifu wa kutafuta vyanzo mbadala wa kutekeleza miradi.

Je, Serikali ipo tayari kuanza kutafuta chanzo mbadala kwa mfano ilivyoruhusu Mamlaka ya Maji Tanga kuwa na hati fungani ya kijani, lakini pia ilivyoruhusu Mfuko wa Barabara *(TARURA)* kuwa na *Samia Bond*; je, Serikali ipo tayari nayo kutekeleza mradi huu kwa kutumia hati fungani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali ilinunua magari ya kuchimba visima; na kwa Mkoa wa Pwani imefanyakazi nzuri kati ya visima 900 tumepata visima 35 na vimetoa maji vikiwepo visima 10 vya Wilaya ya Bagamoyo, lakini bado baadhi ya Kata zina changamoto kubwa ikiwemo Kata ya Makurunge; je, Serikali ipo tayari kuanza awamu ya pili ya visima vingine kugusa maeneo yenye changamoto ya maji ikiwemo Kata ya Makurunge, Bagamoyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nikupongeze sana Mheshimiwa Subira Mgalu kwa ufuatiliaji wa karibu sana masuala ya maji kumtua mama ndoo kichwani, lakini vilevile katika mradi huu kuona kwamba tunaweza tukatumia hati fungani ndiyo mpango wa Wizara kuhakikisha hati fungani itatumika pale inapowezakana.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na magari ya uchimbaji wa visima nipende tu kukupongeza pia kwa ufuatiliaji, haya magari yataendelea kuchimba visima nchi nzima na katika hili eneo la Makurunge na maeneo yote ambayo bado hayajapata visima naamini katika mwaka ujao wa fedha Mheshimiwa Mbunge maeneo hayo pia yatapatiwa visima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum nimeletewa hapa ujumbe na Wabunge wawili, lakini ujumbe uliotangulia ni wa Mheshimiwa Bilakwate, sasa mwenye majibu ni nani?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, mimi hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa wewe ndiyo una majibu? Haya. Mheshimiwa Bilakwate majibu yako huku naambiwa. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 334

**Mradi wa Maji Kyerwa**

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MHE ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, ni miradi gani ya maji inatekelezwa Kyerwa, mkandarasi ni nani, inagharimu kiasi gani na lini itakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imekamilisha utekelezaji wa miradi miwili ya Nyamiaga-Nyakatera na Mabira kwa gharama ya shilingi 2,159,974,805.35 iliyopo Wilayani Kyerwa, Mkoa wa Kagera. Miradi hiyo imetekelezwa na wakandarasi wa ndani wa Kampuni za *JAMTA Investment* na *AMRI AMIRI Co. Ltd.* ambapo kwa sasa inanufaisha zaidi ya wakazi 26,123 waishio katika vijiji saba vya Masheshe, Nyamiaga, Kagu, Nyakatera, Mabira, Nyakatete na Omkagando.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi minne ya Runyinya - Chanya, Kaisho - Isingiro, Kimuli – Rwanyango - Chakalisa na Kikukuru - Rubirizi kupitia wakandarasi wa Makampuni ya *JAMTA, SERENGETI* na *OTONDE* kwa jumla ya gharama ya shilingi zaidi ya bilioni 13. Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imekamilisha uchimbaji wa visima vitano vya Jimbo la Kyerwa katika Vijiji vya Nyakatuntu, Nyakakoni, Songambele, Kamuli na Nyaruzumbura kupitia

programu maalum ya uchimbaji wa visima 900. Kwa sasa kazi inayoendelea ni ufungaji wa pampu na ujenzi wa miundombinu rahisi ya kutolea huduma kwa wananchi inayotarajiwa kukamilika ndani ya mwezi Mei, 2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa miradi mingi ya maji kwenye Wilaya ya Kyerwa inachukua muda mrefu kukamilika kama ule Mradi wa Runyinya – Kimuli na wa vijiji 46; ni lini sasa Serikali itahakikisha kwamba inakamilisha miradi hii ili wananchi wa Kata ya Nyakantuntu na Kamuli waweze kunufaika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Halmashauri ya Mji wa Tarime tunapata Mradi kutoka Ziwa Victoria, lakini tuliahidiwa kwamba tungeweza kupelekewa visima ambavyo vingeweza kusaidia kwenye maeneo kama ya Shule ya Sekondari Nyandoto, Nyakisese na Mkongole vilevile Vituo vya Afya vya Kibumayi na Magena; ni lini sasa Serikali itapeleka uchimbaji wa visima hivi wakati tukisubiria mradi mkubwa wa Ziwa Victoria? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, lini tutakamilisha miradi hii ya vijiji 46 na huu mradi unaoenda kwenye hii Kata uliyoitaja Mheshimiwa Mbunge. Nikuhakikishie Serikali kadiri inapopata fedha tutahakikisha miradi hii inakamilika kwa sababu lengo la Serikali ni kuona wananchi wanapata maji safi na salama na kumpunguzia mwendo mwanamke ambaye anafuata maji umbali zaidi ya mita 400.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tarime hivi visima navyo vipo katika mpango, Mheshimiwa Waziri naye anaendelea kuona namna ya njema ya kuhakikisha visima hivi tunakuja kuvichimba mapema sana na dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mama ndoo kichwani inaweza kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Kata ya Kikukuru mkandarasi ameondoka *site* zaidi ya miezi miwili kwa sababu ya madai; ni lini atalipwa ili arudi *site* kukamilisha mradi huu ambao ni muhimu kwa wananchi wa Kikukuru? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza; lini mkandarasi atalipwa ili mradi ukamilike?

Mheshimiwa Spika, tayari Wizara imeanza malipo kwa wakandarasi wapo kwenye foleni wanapunguzwa taratibu na kadiri fedha inapopatikana tutahakikisha wakandarasi wote wanalipwa ili waweze kufanyakazi kadiri ya mikataba waliyosaini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona, mradi wa maji unaogusa Kata za Maji ya Chai – Kikatiti hadi Samaria Kata ya Maroroni inatekelezwa kwa kusuasua sana na katika ufuatiliaji wangu nimegundua kwamba mkandarasi pia mwenye matatizo kwa hiyo kuna haja ya kuchukua hatua stahiki mapema inavyowezekana.

Je, Waziri utakuwa tayari kuambatana na mimi twende jimboni tukafanye *site meeting* na *stakeholders* wote ikiwepo *DC,* Mkurugenzi na *RUWASA?* Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa swali gumu kidogo, sasa sijui ataambatana vipi na wewe? Nadhani sijui labda utamsemea Waziri sasa kwamba ataambatana na wewe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri karibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwanza mkandarasi yeyote ambaye hatekelezi majukumu yake anafahamu namna sheria ambavyo zinambana. Kwa hiyo, nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge naamini Wizara ya Maji wataenda kumshughulikia na kuona kwamba anafika *site* na kufanyakazi iliyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuambatana na yeye naomba nipokee na nitamfikishia Mheshimiwa Kundo naamini hatakuwa na kipingamizi katika hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 335

**Vita Dhidi ya Magonjwa Yasiyoambukiza**

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani kuhakikisha sekta zote zinashiriki vita dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza yanayosababisha vifo vingi nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Mpango Mkakati wa Tatu wa Kitaifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza, 2021 – 2026 ambapo unajumuisha sekta zote na umeainisha mikakati mahsusi ya udhibiti wa visababishi vya magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kuimarisha uratibu na ushirikishwaji wa sekta mtambuka, kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma, kuwajengea uwezo watumishi katika kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza, kuimarisha na kusimamia shughuli za utafiti pamoja na kuhamasisha wananchi kuhusu njia za kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza. Njia hizi ni kufanya mazoezi pamoja na kuzingatia kanuni bora za lishe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Benardeta Mushashu, swali la nyongeza.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya 33% ya vifo vinavyotokea hapa nchini vinasababishwa na magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari, *pressure,* magonjwa mbalimbali ya moyo na kadhalika. Je, nia afua gani hasa zinazotekelezwa ndani ya Tanzania ili wananchi wote wajue namna ya kujikinga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa matibabu ya magonjwa haya yanachukua muda mrefu kawaida ukiugua ni maisha yako yote na unakuwa unatumia dawa kwa hiyo nigare lakini kwa kuwa magonjwa haya yanaweza kuzuilika; je, kwa nini Serikali isiwekeze zaidi ikaweka mikakati mikubwa, bajeti kubwa katika kuzuia kuliko kungoja kuja kutibu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge na kwanza nimpongeze tu kama kiongozi katika Kamati inayosimamia afya kwa kweli

imekuwa ni eneo lake zuri sana ambalo amekuwa akilipigania wakati wowote na kulisemea.

Mheshimiwa Spika, niseme tu swali lake la kwanza ni afua zipi? Moja kwa kweli wewe mwenyewe umeona jinsi hata Bunge hili linavyosisitiza masuala ya kufanya mazoezi na kuishi maisha yenye afya na masuala ya lishe na wakati wote mmeona vyombo vya habari vikifanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini anajua tunasema hapa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amewekeza kwenye sekta ya afya zaidi ya shilingi trilioni 6.7 ambazo tu hazijaleta mapinduzi kwenye sekta ya afya ndani ya nchi lakini unaona sasa nchi zilizotuzunguka wanakuja kupata huduma ndani ya Tanzania. Ukiangalia vifaa vile ambavyo mimi na wewe tumekuwa tukitembea kwenye hospitali zetu za Mikoa, Taifa utaona asilimia kubwa ya hivyo vifaa vimekuja kutatua matatizo yanayotokana na tatizo ulilolizungumzia hapa. Kwa hiyo, moja; bajeti imetengwa vizuri lakini kwa kweli Serikali imezingatia kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, la pili kwa nini isiongezwe bajeti kwenye eneo hilo? Mheshimiwa Mbunge mimi nikuhakikishie inafanyika kikubwa sana kwenye eneo hilo ndiyo maana umeona miundombinu hata kwa mwaka 2022/2024 utaona jinsi ambavyo teknolojia imenunuliwa lakini umeona jinsi ambavyo miundombinu imejegwa kuanzia ngazi ya zahanati mpaka ngazi ya Taifa kuhakikisha tunawagundua watu kama hao mapema kabla ya magonjwa hayajafika mbali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na nianze kwa kuipongeza Serikali kwa jinsi inavyopambana na ugonjwa wa selimundu kwa sababu ugonjwa huu unaenea sana Ukanda wa Ziwa, Kati na maeneo mengine nchini. Sasa gharama za kutibu ugonjwa huu ni kubwa sana Serikali ina mpango gani kuhakikisha wananchi wanatibiwa bure kwa sababu gharama ni

kubwa na wananchi wengi hawawezi kumudu hizi gharama? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimjibu Mbunge bingwa wa Moshi Vijijini ambapo toka Moshi Vijijini ianzishwe haijapata mtetezi mzuri kama huyu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba selimundu kama ambavyo mnajua ni moja wapo wa uwekezaji ambao Rais wetu amewekeza kwenye nchi yetu kwa kiasi kikubwa na kama mnakumbuka miaka miwili iliyopita ukipata selimundu kinachokutokea ni kwamba tatizo linakusumbua na watu wengi hawafikishi miaka 45 anakuwa amekufa.

Mheshimiwa Spika, lakini Rais wetu ametuletea teknolojia na mnakumbuka tulivyokuja kwenye bajeti yetu ya mwaka jana uliona mtoto aliyeletwa hapa ambaye tayari ametibiwa ndani ya nchi hii na akapona selimundu na mpaka sasa watoto zaidi ya 30 wametibiwa na wote wametibiwa bure.

Waheshimiwa Wabunge, niwaombe tunapoelekea sasa kwenye Bima ya Afya kwa Wote nadhani ndiyo itakuwa suluhisho la kudumu kwa sababu sasa hivi hawa wanaotibiwa bure siyo kutoka kwenye bajeti ya Taifa ni juhudi za Rais binafsi kutafuta fedha kwa wadau na kusaidia hao maskini wasiyojiweza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa kifupi shukrani zenu nimeishapokea tayari, kwa hiyo moja kwa moja kwenye swali.

Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sababu moja wapo ya magonjwa yasiyoambukiza ni suala zima la mfumo wa chakula, namna ya ulaji wa chakula na kulikuwa na taasisi ambayo ilikuwa inashughulikia masuala ya chakula na lishe, ikarudishwa kwenye Wizara ya Afya; je, hamuoni

sasa kuna umuhimu wa Taasisi ya Chakula na Lishe kusimama yenyewe kama taasisi ili iweze kufanya utafiti? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Dkt. Mnzava kwamba masuala haya ukitaka kuyaondoa na kuyapunguza kabisa una-*deal* na eneo la lishe, lakini kuna mchakato maalumu uliofanywa na Serikali, ushauri na michakato mbalimbali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ndiyo maamuzi yaliyofanyika yakafanyika. Ninachotoka kumuhakikishia hii Taasisi ya Lishe inakuja ndani ya Wizara na kuwa kama Idara na Waziri wetu ataisimamia kwa karibu sana na kuhakikisha inaleta matokeo makubwa hata kuliko ilivyokuwa inajisimamia yenyewe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, kwa nini Wizara ya Afya isije na mpango mkakati kushirikiana na Wizara ya Michezo na Wizara ya Ujenzi kuhakikisha kwamba kunajengwa viwanja na ili wananchi waweze kuweza kukimbia, kutembea na kufanya mazoezi katika maeneo yetu ya halmashauri zetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimtoe tu wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, hicho kinafanyika na ndiyo maana unaona kuna ushirikiano mkubwa wa Wizara ya Afya na Bunge, lakini na Wizara ya Michezo. Hata ukapoona tunapongojea michezo ya *AFCON* na mambo mengine utaona ushirikiano wa karibu sana na Wizara ya Afya, lakini pamoja na Wizara ya Michezo katika kuhakikisha tunafanya hayo. Sasa kwa sababu ni masuala ya kibajeti kila wakati tunaenda kitaifa, lakini pole pole mpaka tutashuka kwenye ngazi ya wilaya, lakini mambo hayo yanakwenda na yanaenda pamoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, ni upi mpango wa Serikali wa kupunguza gharama za matibabu ya figo kwenye kusafisha pamoja na upandikizaji kwa sababu ugonjwa huu kwa sasa umekuwa ukiwaathiri sana Watanzania na hasa walioko vijijini kwa sababu hawana uwezo wa kukidhi gharama za upandikizaji, lakini pia za usafishaji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kumekuwepo na gharama kubwa za kusafisha figo na mambo mengine siyo tu figo, lakini hata tiba mbalimbali ambazo zinatokana na haya magonjwa ya kuambukiza, lakini kama anakumbuka Mheshimiwa Mbunge miaka mitatu iliyopita kusafisha figo ilikuwa ni shilingi 400,000 mpaka shilingi 600,000 lakini kwa sasa utakuta baadhi ya hospitali zetu zimeanza utakuta zingine shilingi 120,000 na zingine shilingi 200,000. Maana yake zinaanza kushuka, lakini mpango wa Serikali ni nini?

Mheshimiwa Spika, moja; ni kuhakikisha vifaa ambavyo vinatumika kwenye kufanya shughuli hiyo, vitendanishi na dawa tuna *access* moja kwa moja viwandani, lakini pia kuhakikisha katika watu wanaongiza nchini hivyo vitu tunaongeza wadau mbalimbali wanaoingiza ili kutengeneza *competition* ya wafanyabiashara ili pia kushusha bei wakati *MSD* nayo inatengeneza mkakati wa kwenda viwandani na kuhakikisha inachuka yenyewe na ku-*supply* kwenye hospitali zetu ili kushusha gharama.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi sasa aulize swali lake.

Na. 336

**Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza:-

Je, Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 2007 inayosema akina mama wajawazito watajifungua bure bila malipo bado ipo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 2007 ipo na inatumika kutoa miongozo katika uendeshaji wa utoaji wa huduma za afya nchini. Hata hivyo, Wizara ipo katika hatua za mwisho za mapitio ya Sera ya Afya ya mwaka 2007. Hata hivyo, kuanza kutumika kwa Bima ya Afya kwa Wote itakuwa suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza nishukuru kwamba Serikali imekiri kwamba hii sera ipo lakini kiuhalisia hakuna mama yeyote mjamzito hapa Tanzania anayejifungua bure.

Sasa nini kauli ya Serikali yakuzitaka hizi zahanati, vituo vya afya na hospitali ambazo zinatoza akina mama wajawazito kinyume na sera yetu ya mwaka 2007?

Swali la pili, sasa hivi mama akienda kujifungua anaambiwa lete nyuzi, lete dripu, lete *gloves* na hivyo vifaa sio vyote vinavyotumika na vikibaki vinabaki kule hospitali. Sasa nini kauli ya Serikali kuhakikisha hilo jambo haliendelei? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba hii sera hai-*apply*, ni kweli

ina-*apply* lakini kwa sababu ukiangalia na ukipiga hesabu ili uweze kuwahudumia wakina mama wote bure kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge, ametamani unahitaji shilingi bilioni 227. Ukweli hapa Bungeni ninyi mnajua wenyewe kwamba tumekuwa tukitenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya dawa tu, maana yake ni nini? Ni ukweli kwamba hutaweza kuwahudumia kina mama wote kwa bure kama ambavyo ametamani Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Mbunge, akumbuke tulikwenda ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na wewe jimboni kwako, unakumbuka mimi na wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu, alivyotuacha tulienda pamoja kwenye kituo cha afya kilicholalamikiwa, lakini hospitali ya wilaya, ulikuta kwamba walikosea kwenye kutengeneza maoteo. Maana yake tulikuta kwamba matumizi yao ya mwaka ni zaidi ya shilingi milioni 800 lakini wao wakaleta matumizi ya shilingi milioni 400 na wakati huo tayari wameshatumia shilingi milioni 507.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini? Kuna shida katika eneo la uongozi na kama unakumbuka tulienda kwa *DMO* tukakuta bado kuna zaidi ya shilingi milioni 400 kwenye akaunti hazitumiki, lakini hospitali haina dawa.

Kwa hiyo matatizo kama hayo ya uongozi yanaweza yakawa yanaleta shida, kwa hiyo, mimi nikuombe Mheshimiwa Mbunge, tuwasiliane ili tuweze kuliangalia kila jambo *specifically* ili tuli-*treat* kama linavyowezekana kwa sababu mengine yanawezekana yakawa ni ya kibajeti kweli kwamba wamemaliza hawana lakini mengine yanaweza yakatokana ni namna *leadership* wanavyofanya wenyewe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, vifaa vinavyobaki anavyokuwa ameleta mama kujifungua, ndio lilikuwa swali lake la pili. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, vifaa vinavyobaki ndio hayo hayo inarudi pale pale kwamba tunahitaji kujua *specifically* eneo husika, kwa sababu kama unamwambia mtu kuna vifaa vyake vinabaki, lakini mwisho wa siku zikibaki ni

zinakwenda wapi, ndio hayo bado tunasema kunawezekana kuna tatizo kwenye *leadership*, kwa sababu tulivyokwenda kwenye jimbo lake, tulikwenda tukakuta kwanza, tulikutana na nilisema lete hii inaitwa *slip* ya benki, lakini wakaleta *slip* ya benki moja ambayo mwisho wa siku tuliikuta imekuwa-*forged,* lakini mwisho wa siku tunakwenda tunakuta wana shilingi milioni zaidi ya 300, tukakutana na mambo mengi mabovu mabovu.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo wakati mwingine kuna mambo mengine yanatokea ni ya uongozi na mengine ni nje ya uwezo wa muhusika aliyopo pale. Kwa hiyo, kila jambo ninatamani tuli-*deal* kwa kuangalia tatizo limetokea wapi ili tuweze kuhukumu kwa haki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Pamoja na kuwa na sera nyingi, ipo pia sera ya watoto chini ya miaka mitano, kutibiwa bure na sera hii haijawahi kutekelezeka hata kidogo. Katika majibu ya msingi ya Naibu Waziri, yanasema ametoa takwimu ya wamama wajawazito, kwamba wakiwahudumia wote haitawezekana...

**SPIKA:** Mheshimiwa uliza swali.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, swali, sasa kama takwimu ya watu wanaopaswa kuhudumiwa ni wengi, watoto na akina mama wajawazito, kwa nini Serikali isitoke kuwaambia wananchi kwamba sera hizi hazipo ili waelewe kwamba hakuna bure kwa wajawazito wala hakuna bure kwa watoto chini ya miaka mitano? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, labda tu nimwambie Mbunge namuelewa sana, ila hata yeye kwenye mipango yake ambayo ameipanga, anaianza anapanga mpango mzima, lakini anautekeleza hatua kwa hatua na nimwambie tu kwa maana ya *exemption*, kwa maana watu

waliotibiwa na yeye mwenyewe anajua jinsi tumepambana na yeye kwenye hospitali yake ya rufaa kule Mbeya, kwa maana ya watu wa *exemption* kwa mwaka tu Serikali inatumia zaidi ya shilingi bilioni 667, lakini ukweli ukikuta waliohitaji *exemption* ni zaidi ya hao lakini pasingekuwepo na hiyo sheria pia hawa tuliyowasaidia shilingi bilioni 667 pasingekuwepo na namna ya kutekeleza.

Kwa hiyo, sheria ipo ila ni ukweli kwamba haijatekelezwa kwa 100% lakini siku zote unaweza ukapanga mipango, lakini bajeti ya kutekeleza kwa 100% inaweza isipatikane lakini ukitekeleza kwa 60% nayo ni utekelezaji, ni kujipanga kumalizia 40%. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, swali la nyongeza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha ya Serikali inatozwa kwa mujibu wa sera na kwa mujibu wa sheria; je, utolewaji wa huduma za afya zilipata wapi mamlaka ya kuwatoza hawa akina mama wajawazito pamoja na watoto wenye umri chini ya miaka mitano huku ikijua kabisa kwamba kasma ile haipo kwa mujibu wa sheria wala sera hairuhusu, waliruhusiwa na nani kufanya hayo? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nijaribu tu kumwambia Mpina, kuna sheria, kanuni lakini pia wakati...

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ni Mheshimiwa Mpina.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, *okay,* naomba nimjibu kaka yangu Mheshimiwa Mpina, kwa kumwambia wakati mwingine katika sheria, kuna wakati kuna sheria iliyopo, kuna kanuni zilizopo, lakini pia kuna kutumia busara. Maana yake sisi tuna bajeti ya shilingi bilioni 200 kwa ajili ya dawa na vitendanishi, lakini matumizi ni zaidi ya hiyo. Kwa hiyo, anapokuja mgonjwa

tunatumia hekima na busara yule anayeweza kulipa analipa, asiyeweza kulipa anahudumiwa na sheria iliyopo.

Kwa hiyo, kwa busara hiyo ndio maana yeye yupo salama, wananchi waliyopo kwenye jimbo lake wapo salama na leo Tanzania ina afya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru kunipa niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wakina Mama, kubeba *delivery kit* kuelekea katika hospitali wakati wa kujifungua hasa vijijini, wakienda wakakutana na changamoto ambayo wanatakiwa wafanyiwe *operation*, wanatakiwa walipe kwanza pesa ya *operation* ndio wafanyiwe *operation* na hii inapelekea akina mama wengi kufa wakati wa uzazi; nini kauli ya Serikali katika hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali kwenye eneo hilo ni msimamo wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipolihutubia Bunge hili kwa mara ya kwanza, alipofika eneo la huduma ya mama na mtoto alirudia mara mbili na akaongea kwa msisitizo mkubwa na ndio maana unaona baada ya yeye kutoka hapa Bungeni, alidumbukiza *resources* sekta ya afya na ndio maana leo tuna nishani kwenye eneo hilo la kina mama na watoto, ukilinganisha na duniani, tuna nishani ya kidunia ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kati ya Marais saba duniani waliyopata nishani yumo lakini kwa Afrika ni Rais pekee aliyepata.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kweli hayo yanayotokea, tamko la Serikali Mtanzania yeyote siyo tu mama mjamzito, akifika kwenye kituo cha afya ni lazima cha kwanza ni kuokoa maisha na kuhakikisha huyo mtu salama, ndio mambo mengine yafuate. Kwa hiyo, akipatikana mtu ambaye anasababisha kitokee kifo

kwa sababu alikuwa anasubiri fedha hata kwa maadili yetu unanyang'anywa cheti na hautaruhusiwa tena ku-*practise*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mbunge wa Shaurimoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 337

**Michango ya Bima ya Afya**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED** aliuliza: -

Je, kwa nini michango ya Bima ya Afya isiwe sawa na utaratibu wa michango ya pensheni kati ya mwajiri na mtumishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha Sheria ya Bima ya Afya, Sura 395, mwajiri huchangia asilimia tatu na mwajiriwa asilimia tatu ya kiwango cha mshahara ili kukidhi hitaji la mnufaika kupata huduma za afya katika vituo vilivyosajiliwa na mfuko. Michango ya Bima ya Afya inatofautishwa na michango ya pensheni kwa kuwa michango ya pensheni inahusisha malipo ya uzeeni na kiunua mgongo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa na swali moja la nyongeza.

Je, ni kwa kiasi gani *NHIF* huwa inachukua hatua kwa changamoto mbalimbali ambazo huwa zinajitokeza katika

hospitali mbalimbali hapa nchini juu ya wanachama wake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nijibu swali la kaka yangu analosema kwamba ni kwa kiwango gani ina *react* Bima ya Afya, inapotokea changamoto mbalimbali za Bima ya Afya kwa wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Bima ya Afya, imekuwa iki-*react* kulingana na matatizo yenyewe yanavyokuja na aina ya tatizo. Nikuhakikishie pia ni kweli kwamba hapa karibuni pamekuwa na malalamiko mengi sana kwa wateja, lakini pili, kwa kutoka maeneo mbalimbali kuhusiana na bima.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachotaka kumtoa Mheshimiwa Mbunge, wasiwasi kila wakati na wewe unajua sasa hivi tuna Mkurugenzi wa Bima ya Afya, dada yetu ambaye ana *experience* kubwa, *exposure* kubwa na ni mzuri sana kwenye kutatua matatizo. Nikuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kuwa matatizo ya nyuma uliyokuwa unayasikia kwa aina ya Mkurugenzi tuliyenaye sasa hivi nataka kukuhakikishia yanatatuliwa kwa wakati na yanasimamiwa kwa uadilifu mkubwa sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watumishi wa Serikali, wanapostaafu wanaendelea kupata huduma ya Bima ya Afya, je, upi utaratibu wa wazazi wa wale watumishi waliostaafu kuendelea kupata huduma ya Bima ya Afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwahudumia wazazi wa waliostaafu ambao mimi naamini watakuwa ni wachache sana, naomba tu niseme kwamba kwa sababu kama kumeibuka matatizo kama hayo kwa wakati huu,

nimuombe Mheshimiwa, kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati kwenye suala zima la Bima ya Afya kwa wote ambalo tunaelekea huko mbele, nafikiri ni moja wapo ya mchango mzuri ambao unaweza ukajadiliwa na kuona tunafanyaje kuhakikisha eneo hilo linaweza kuwa *covered* bila kuathiri mambo mengine ya kibajeti inapotokea masuala ya uendeshaji wa mfuko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq nilielewa vizuri swali lako? Kwamba mtumishi amestaafu, kwa maana ya kwamba kafika miaka 60 kulingana na yeye alipo ama 65, halafu yeye mzazi wake kuna mpango gani wa kuendelea kupewa bima na yeye, ndio nilielewa hivyo swali lako?

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Aaah.

Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani umesema umechukua hoja yake, mnaenda kuifanyia kazi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimechukua hoja yake, lakini ninamuomba tuendelee kujadiliana kwa pamoja.

**SPIKA:** Ahsante sana, haya ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 338

**Ujenzi wa Majosho Singida Mashariki**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga majosho ya kuogeshea mifugo kwenye vijiji vya Jimbo la Singida Mashariki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2022/2023 Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitumia kiasi cha shilingi milioni 92 kwa ajili ya kujenga majosho manne katika Halmashauri ya Ikungi linapopatikana Jimbo la Singida Mashariki ambapo kupitia fedha hizo Jimbo la Singida Mashariki lilifanikiwa kujengewa josho moja lililopo katika Kijiji cha Ntuntu lenye thamani ya shilingi milioni 23. Josho hilo limekamilika kwa 100% na linafanya kazi. Aidha, Wizara inaendelea kuratibu ujenzi wa majosho katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo vijiji vya Jimbo la Singida Mashariki kadiri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara inashauri Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi inayosimamia Jimbo la Singida Mashariki kutenga fedha kutoka katika mapato yao ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa majosho katika jimbo hilo kwa lengo la kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe, mbung’o na wadudu wengine, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, tunaishukuru Serikali kwa kutupatia fedha katika Kijiji cha Ntuntu tumeweza kujengewa josho na linafanya kazi tunashukuru sana, lakini katika Kijiji cha Siuyu tulikuwa na changamoto kubwa ya mgogoro, lile josho lilikuwa limejengwa kwenye maeneo ya Kanisa la *RC* pale Siuyu, tukawa tumeomba Serikali lihamishwe na eneo lipo tayari. Ni mwaka wa tatu sasa tumeahidiwa halijakamilika. Ni lini sasa Serikali itajenga josho katika Kijiji cha Siuyu ili kuondokana na changamoto ambayo ipo ikiwemo kuondoa mgogoro uliopo kati ya kanisa na wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kwamba katika Jimbo la Singida Mashariki ambalo sasa ni Ikungi Mashariki tuna mifugo mingi sana maeneo ya Isuna, Ng'ongosolo, Ulyampiti, Mang'onyi, Msule na Choda, ni lini sasa majosho yatajengwa kwa ajili ya afya ya mifugo ya wananchi ambayo ni uchumi mkubwa katika eneo hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nianze na hili la josho lililojengwa kwenye eneo la kanisa, tutatuma wataalamu kutoka Wizara ya Mifugo, kwenda kuangalia eneo hilo limekaaje na kisha tutachukua hatua ya kuhamisha josho hilo kupeleka kwenye maeneo ambayo wananchi watapendekeza, lakini hili la pili la wingi wa mifugo katika jimbo la Mheshimiwa Mtaturu, tutatuma wataalamu pia kwenda kuangalia idadi ya mifugo iliyopo hapo na uwezeshaji wa majosho yetu kama yanatosha kukidhi haja ya mifugo iliyopo hapo.

Kwa hiyo, tukishaona kuna umuhimu wa kujenga majosho mengine tupo tayari kupeleka majosho katika jimbo hilo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Sabu, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga majosho katika maeneo ya pembezoni mwa Mji wa Bariadi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, labda nimuombe Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili tutatuma wataalamu kwenda kuangalia umuhimu wa kujenga majosho katika maeneo hayo kulingana na wingi wa mifugo inayopatikana katika pembezoni mwa Mji wa Bariadi, lakini pia niiombe Halmashauri ya Mji wa Bariadi kuona umuhimu wa kuwajengea majosho wafugaji wetu katika maeneo haya yanayozunguka kwa sababu mifugo hawa wanaingiza kipato

ndani ya halmashauri, lakini pia Serikali Kuu. Kwa hiyo, tutatuma wataalamu kwenda kuangalia kama kuna umuhimu wa kuongeza majosho katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga majosho na malambo katika vijiji 90 vya Wilaya ya Kilwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Serikali inaendelea kujenga majosho, lakini pia na malambo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kulingana na umuhimu na mahitaji ya wafugaji wetu wanaopatikana katika maeneo hayo. Kwa hiyo, kama kuna mahitaji ya wafugaji wetu katika jimbo lake Mheshimiwa Mbunge, tupo tayari kujenga maeneo hayo kulingana na upatikanaji wa fedha kadiri ambavyo inawezekana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ufugaji ni mojawapo ya sekta muhimu sana za uchumi katika Jimbo la Mwibara, je, ni lini Serikali itajenga majosho katika Kata za Namhula, Igundu, Nansimo, Iramba na Kasuguti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, tutatuma wataalamu kwenye Jimbo la Mwibara kwenda kuangalia umuhimu wa kujenga majosho hayo, lakini pia kwa taarifa tulizonazo ni kwamba tayari kwenye jimbo la Mheshimiwa Mbunge tuna majosho zaidi ya matatu ambayo tumeyajenga kupitia bajeti iliyopita. Kwa hiyo, tutaendelea kuboresha, tutaendelea kuongeza majosho katika jimbo la Mheshimiwa na hakika mambo yatakwenda vizuri, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa nini Serikali hasa Wizara yako imezingatia zaidi ujenzi wa majosho na kutelekeza ujenzi wa mialo kama ilivyotelekeza katika Mwalo wa Ng'ombo kiasi cha mkandarasi kuondoka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Serikali imetelekeza huo mwalo, isipokuwa kilichotokea ni kwamba ni uhaba wa fedha, mara tu tutakapopata fedha tutamlipa mkandarasi huyo na atarudi *site* kwenda kukamilisha kazi ambayo amekwisha ianza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu, lakini pia majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa nilete tangazo la wageni waliopo hapa Bungeni asubuhi hii.

Wabunge mnaozungumza tafadhali mnyamaze nimesimama na kwa kuwa nilishasema mimi mwalimu sichoki kufundisha. Kwa hiyo, mtulie kidogo nimesimama.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wageni wa Mheshimiwa Jerry William Silaa ambaye ni Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na tutaanza na Ndugu Mohammed Khamis Abdulla ambaye ni Katibu Mkuu; Ndugu Nicholaus Mkapa ambaye ni

Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Juma Reli, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA);* Balozi Meja Jenerali Mstaafu Gaudence Milanzi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Shirika la Posta Tanzania; Balozi Meja Jenerali, samahani.

Yupo Mheshimiwa Balozi Valentino Mlowola, Mwenyekiti wa Bodi, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF);* na Balozi Adadi Rajabu, Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, ahsante sana na karibuni. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Hawa Ngh'umbi, Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano la Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; yupo Dkt. Jabiri Bakari, Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA);* Ndugu Macrice Mbodo, Posta Masta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania; Mhandisi Peter Mwasalyanda, Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wate; Dkt. Nkundwe Mwasaga, Mtendaji Mkuu, Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; Dkt. Emmanuel Mkilia, Mkurugenzi Mkuu Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi; Ndugu Benedict Ndomba, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Serikali Mtandao; Dkt. Goodwill Wanga Mtendaji Mkuu, Baraza la Taifa la Biashara; Ndugu Hillary Tesha, Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano la Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; na Mhandisi Cecil Francis, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika ya Mawasiliano Tanzania; karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Philip Besiimire, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mtandao wa Simu wa Vodacom, Ndugu Pierre Canton-Bacara, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Honora wanaoendesha Mtandao wa YAS; Ndugu Charles Kamoto, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mtandao wa Simu wa Airtel; Ndugu Tran Thi Thuy Dung, Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mtandao wa Simu wa Halotel; Ndugu David Mwankenja, Mkurugenzi wa Sera na Mipango; Ndugu Innocent Mushi, Mkurugenzi Mtendaji *Towerco of Africa;* Ndugu David Dzigda, Mkurugenzi Mtendaji Helos Tower; Ndugu Zhang Bihui, Mkurugenzi Mtendaji Huawei; na Ndugu Ramadhani Milanzi,

Mkurugenzi Mtendaji, *Raddy Fiber Tanzania,* karibuni sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Juma Simba, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa, Mkoa wa Dar es Salaam; Ndugu Ally Bananga, Katibu wa Mafunzo, Itikadi na Siasa wa Chama Cha Mapinduzi wa Mkoa wa Dar es Salaam. Haya ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Alhaji Saidi Side, Mwenyekiti wa CCM-Wilaya ya Ilala; Chifu Syvester Yerad, Katibu wa CCM, Wilaya ya Ilala. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ipo pia familia ya Mheshimiwa Jerry William Silaa, yupo Bi. Mariam Bakari Silaa ambaye ni mke wa Mheshimiwa Jerry. *(Makofi)*

Yupo pia Bi. Aisha Bakari ambaye ni shemeji yake Mheshimiwa Waziri; yupo pia *Comrade* Simba William Jerry Silaa ambaye ni mwanaye, ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wanne wa Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi ambaye ni Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na hii ni familia yake; yupo Ndugu Moureen Salla, huyu ni mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri; yupo Vaileth Kimwaga mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Sasa ili tusichanganye na hii ya Moureen Salla, mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri huyu Vaileth Kimwaga atakuwa ni mtoto wa kulea wa Mheshimiwa Naibu Waziri, maana sasa mambo yasiwe mengi. *(Makofi/Kicheko)*

Yupo Ndugu Doreen Bahati, dada wa Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana; yupo Ndugu Koletha Kipeta, dada wa Mheshimiwa Naibu Waziri, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengi Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni wengine sita wa Mheshimiwa Naibu Waziri ambao ni

ndugu zake kutoka Mkoa wa Dar es Salaam, sijui wamekaa upande gani, haya karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 19 wa Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli ambao ni Wenyeviti wa Kata wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Ilala, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi ambao ni rafiki zake kutoka Kata ya Mabogini, Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate ambaye ni rafiki yake kutoka Kyerwa, Mkoani Kagera, Ndugu Vumilia Leonard. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, ambaye ni Ndugu Eliud Kabelege, Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Amina Bakar Yussuf, ambao ni Ndugu zake kutoka Chang'ombe, Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria cha Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 22 wa Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, ambao ni watumishi wa Ofisi Kuu ya Dayosisi ya *Western Tanganyika* ya Kanisa la Angalikana Tanzania kutoka Kasulu, Mkoa wa Kigoma wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Dayosisi Mchungaji Joram Ntakije, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 54 na walimu saba wa darasa la nne, la tano, la sita na la saba kutoka Shule ya Msingi Enyorata iliyopo katika Kata ya Murieti, Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 64 na walimu nane wa Shule ya Awali na Msingi Bernhard Bendel kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanakwaya 39 wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri, Jimbo la Mbeya Mashariki, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 29 na walimu watatu kutoka Shule ya Awali Nuru iliyopo Kata ya Makulu, Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Haya tuwasubiri watoto wasimame ili wapate picha, waambieni tu taratibu tutawasubiri. Haya, waamsheni wote maana wengine wakikosa picha kumbukumbu zitakuwa ngumu kidogo. Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

Kuna huyo wa mbele bado amelala mwalimu, ili wapate picha vizuri. Haya ahsante sana. Haya, mpiga picha ninaamini umemaliza sasa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wafanyakazi wawili kutoka *University of Dar es Salaam Computing Center,* karibuni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo la wageni, sasa tunaendelea na ratiba yetu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninaomba Mwongozo wako kwa jambo lililotekea leo mapema nikirejea swali namba 336 ambalo lilijielekeza kuhusiana

na utekelezaji wa Sera ya Afya ya Taifa ya mwaka 2007 kwenye utoaji wa huduma bure kwa mama wajawazito.

**SPIKA**: Namba 336?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, limeulizwa na Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole.

**SPIKA:** Sasa ili twende vizuri ninaona na yeye ameomba Mwongozo, labda nimpe nafasi mwenye swali isije kuwa miongozo yenu inafanana. Ninampa nafasi mwenye swali kisha nitarejea kwako kwa sababu ni mwenye swali.

Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimesimama hapa kwa Kanuni ya 53 kuhusu swali kutokujibiwa kikamilifu nikiomba mwongozo wako kuhusu swali namba 336 ambalo limetokea leo mapema.

Mheshimiwa Spika, mapema leo niliuliza swali kuhusu Sera ya Afya ya mwaka 2007 kwa akina mama wajawazito kujifungua na nikataka nini kauli ya Serikali kwa hospitali za Serikali, zahanati na vituo vya afya ambazo zinatoza hela akina mama kwenda kujifungua kinyume na sera hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile nikauliza nini kauli ya Serikali kwa akina mama wajawazito wanapokwenda hospitali wanaambiwa walete nyuzi, leta dripu za maji, leta *gloves* na wakati mwingine hivyo vifaa havitumiki na hawarudishiwi, vinabaki hospitali jambo ambalo Serikali imeshindwa kutolea majibu hayo maswali. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, ni jambo linalolingana ama ni tofauti? Haya Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Mwongozo wangu kama nilivyoanza kusema awali wa swali namba 336 linalohusiana na Sera ya Afya ya Taifa ya mwaka 2007

iliyoelekeza utoaji wa huduma ya afya bure kwa mama wajawazito, lakini pia na watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Serikali wakati inajibu hapa swali hili imekiri dhahiri kwamba inatoza fedha kwenye huduma hii kwa baadhi na imeenda mbali zaidi ikasema wale wanapokuwa wanakuja na *kits* zile zinabaki, *that means* inatoza zaidi maana yake zikibaki haijaelekeza zinaenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kwamba sera ikishatungwa tunatunga sheria hapa, kanuni, miongozo kama vile Mheshimiwa Rais alikuja kuhutubia hapa Bunge akaelekeza dhahiri kwamba kuhakikisha wanapunguza vifo vya mama wajawazito nchini na kwa kweli amejitahidi katika hilo, lakini na taratibu mbalimbali kwenye utekelezaji, lakini zaidi huwa tukipitisha bajeti hapa kuna ruzuku inaenda kwa ajili ya huduma hii huko, ruzuku zinaenda kwa ajili ya huduma ya mama wajawazito na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nikasimama kutaka kujua kukuomba mwongozo wako kwa sababu hizi fedha kama ambavyo Serikali imekiri wanazitoza, hakuna kazima yoyote ambapo zinaelekezwa na Bunge lako Tukufu linaweza hata likashindwa kwenda kufuatilia mapato na matumizi ya Serikali hatuwezi ku-*account* katika hili.

Kwa hiyo, nikaomba Mwongozo wako haya maelezo ambayo Serikali imeeleza hapa utuelekeze zaidi maana yake sera ipo Serikali imekiri inatoza kinyume na sera, Mwongozo wako ni upi hizi fedha ambazo zinatozwa zinaelekezwa wapi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa George Mwenisongole, akitupeleka kwenye Kanuni ya 53 kuhusu swali kujibiwa kikamilifu na kwa maelezo yake anaona majibu ya maswali ya nyongeza yaliyoulizwa kwamba hayakujibiwa kikamilifu na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Sasa nimejaribu kufuatilia yale maneno aliyoyasema Mheshimiwa George na kwamba hajajibiwa, nikajaribu

kukumbuka na alichokisema Mheshimiwa Naibu Waziri, ili niweze kutenda haki kama limejibiwa kikamilifu au hapana nitaenda kufuatilia zile Taarifa Rasmi za Bunge kisha mwongozo utakuja kutolewa, kwa sababu pamoja na kwamba ametupeleka Kanuni ya 53 lakini hoja yake ni kwamba swali halijajibiwa kikamilifu.

Sasa ili niweze kuagiza kama swali lije lijibiwe upya au yale maswali ya nyongeza yaje yajibiwe upya lazima nipitie upya swali lililokuwa limeulizwa na majibu yaliyotolewa. Kwa hiyo, nitakuja kueleza baadaye baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Amesimama Mheshimiwa Esther Matiko kuhusu jambo linaloelekeana halifanani lakini linaelekeana na hili ambalo amelisema Mheshimiwa George Mwenisongole, lakini yeye ameenda moja kwa moja kwamba Sera inasema nini na kile kinachofanyika huko na ameongezea hapo sasa na mambo mengine kwamba hizo fedha zinapelekwa wapi, zikikusanywa.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza, mimi siyo mtu ambaye ninapaswa kuwa ninajibu maswali kujua kwamba pesa zikikusanywa sasa huwa zinapelekwa wapi, lakini nadhani swali hilo aliuliza Mheshimiwa Mpina, kama swali la nyongeza kwamba zile pesa zikikusanywa zinapelekwa wapi.

Sasa kwa utaratibu ule wa kawaida kabisa wa Serikali nadhani humu tukipitisha huwa tunapitisha kuna sehemu huwa panaandikwa maduhuli pale ambapo yanakusanywa na upande wa Serikali. Kwa hiyo, sisi huwa tunapitisha kama sehemu kwamba Serikali imesema itakusanya kwenye eneo hili kiasi hiki. Kwa hiyo, Serikali huwa inakusanya maduhuli. Sasa mkisema zinaelekea wapi sasa hilo ni swali lingine lije liulizwe kwa sura ambavyo Serikali itaweza kujibu swali hilo kikamilifu, lakini Serikali inaruhusiwa kukusanya fedha.

Sasa kuhusu sehemu ya kwanza ya kile ulichokiuliza kuhusu sera hii na kwamba sera inasema hivi, lakini uhalisia uliopo huko siyo wenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, iko tofauti ya kawaida kabisa ya maana ya sera na sheria, sheria lazima itekelezwe na sheria ndio maana inaitwa sheria ni msumeno, ikishatungwa lazima ifanye nini, itekelezwe, lakini sera ni makusudio ni jambo ambalo tunatamani, ni jambo ambalo kwanza siyo Bunge linalopitisha sera lazima tuwe tumeelewana hivyo. Sera ni Serikali inakuwa imejiwekea ni kama inaweka malengo inataka nini inakusudia kufanya nini. Sasa katika yale makusudio katika wingi wa yale majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri ni kwamba ni kweli Serikali imekusudia kufanya moja, mbili, tatu, lakini pale ambapo Serikali inakuwa haina uwezo wa kufanya hayo kwa kila mtu basi ndio huo utaratibu mwingine unawekwa.

Sasa pengine majibu sasa kama linatakiwa kujibiwa kikamilifu liulizwe kama swali upya ili watu waelewe ni yupi anayepewa yupi ambaye hapewi kwa sababu hata hao wengine tumeuliza hapa maswali mengi sana kuhusu figo na nini, wapo wanaotibiwa kwa msamaha, wapo ambao lazima walipe na hawa akina mama pia wapo wanaojifungua bila malipo na wapo ambao lazima walipe. Kwa hiyo, mazingira ni hayo, sasa upande wa Serikali ili iweze kujibu vizuri kwamba nani anayestahili kulipa nani ambaye halipi maana sisi tumeweka kama kundi moja kana kwamba hakuna wanaopata msamaha. Kwa hiyo, hapo sasa ni maana tu ya kawaida ya sera. Kwa hivyo, sera ikitekelezeka sawa, lakini sera inapaswa itungiwe sheria, kama sisi hatujatunga hapa sheria kwamba hicho ndicho kinachotakiwa kufanywa basi ni sera bado inabaki kama makusudio inabaki kama malengo, lakini kama tunataka itekelezwe vile ambavyo sera imesema basi lazima tutunge sheria hapa ndani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa majibu yale ambayo ninaweza kutoa kwa sababu umetumia hiyo Kanuni ya Mwongozo na mimi lazima nitoe Mwongozo, Mwongozo ni huo maana tu ya neno sera ni nini, hiyo inatupa picha Watanzania kwamba jambo gani ambalo Serikali limesema lazima ifanye na jambo gani ambalo inakusudia kufanya. Kwa hivyo, inaweza ikafanikiwa kufanya na inaweza isifanikiwe kufanya. Hizo ni maana za kawaida. *(Makofi)*

Sasa hilo jambo lingine ambalo linahusu sasa maswali mahususi ya Mheshimiwa George Mwanisongole, Waheshimiwa Wabunge tutarejea kwenu tutakapokuwa tumepitia Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo sasa tunarudi kwenye ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. AZIZA MAKWAI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Jerry William Silaa aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Mwenyekitii wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari - Fungu 68 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka 2024/2025 na lijadili na kuidhinisha mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge la 12 ambao ni mahsusi kwa ajili ya kujadili Bajeti ya Serikali.

Aidha, kwa heshima na taadhima ninaomba kutumia fursa hii kipekee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuanzisha Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tarehe 8 Disemba, 2024. *(Makofi)* Vilevile, ninapenda kumshukuru kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Ninamuahidi kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu aliyonikabidhi ya kusimamia sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari kwa juhudi, maarifa na uadilifu ili kuwezesha nchi kufikia adhma ya kuwa na uchumi wa kidijitali.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza miaka minne tangu aingie madarakani. Katika kipindi cha uongozi wake sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari imepata mafanikio makubwa ikiwemo; Kuanza ujenzi wa minara 758 katika kata 713 kupitia Mradi wa Tanzania Kidijitali; kuanza ujenzi wa minara 636 nchini kupitia Mradi wa Mawasiliano Vijijini; kufikisha huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye Wilaya 109 kutoka Wilaya 36 nchini; kufikisha Mkongo wa Taifa katika nchi ya Msumbiji na kuanza taratibu za ufikishwaji wa Mkongo katika nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo; kuongeza huduma ya mtandao wenye kasi kwenye maeneo ya watu *(population coverage)* kutoka 40% hadi 91%; kuimarisha upatikanaji wa intaneti nchini kwa kuongeza mkongo mmoja wa baharini wa 2Afrika; kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na mikongo ya baharini iliyopo Mombasa, Kenya kupitia mpaka wa Horohoro mkoani Tanga; kufanyika kwa Operesheni Anwani za Makazi mwaka 2022 na kuandaa mkakati wa miaka kumi (2024 – 2034) wa uchumi wa kidijitali. Wizara inatambua umuhimu na matarajio makubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais ya kufikisha huduma za Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa wananchi kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa

Rais. Aidha, niruhusu pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuongoza vyema, kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar pamoja na kuendelea kudumisha na kuuenzi Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawashukuru kwa maelekezo na ushauri wao wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Aidha, nimpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ya bajeti ambayo imetoa utekelezaji wa malengo ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 pamoja na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2025/2026. Napenda kuahidi kuwa Wizara itayafanyia kazi masuala yote yanayohusu sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari yaliyoainishwa katika hotuba hiyo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina maneno bora zaidi kuliko yale aliyotumia Mheshimiwa Aweso kukupongeza, ninaomba kuwaomba wananchi wa Mbeya Mjini wasifanye kosa, wakurejeshe kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuongoza Bunge letu na kazi kubwa unayoipa heshima nchi yetu kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muugano wa Tanzania kwa kuongoza na

kusimamia kwa umahiri shughuli za Bunge. Mheshimiwa Naibu Spika ni Mbunge mwenzangu kutoka Wilaya ya Ilala na ninaomba kuwaomba wananchi wa Ilala wa jimbo lake na wenyewe wamrudishe Bungeni kwa kazi kubwa aliyofanya ya kutuongezea shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kazi wanayoifanya ya kukusaidia kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa kusimamia shughuli za Bunge kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa dhati kumpongeza Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu; Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki na Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa ushirikiano wao kwangu na Wizara kwa ujumla katika kuhakikisha malengo ya sekta yanafikiwa. Aidha, ninaishukuru Kamati kwa kujadili na kupitisha kwa kauli moja Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 68 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati katika kuchambua, kushauri na kufuatilia majukumu yanayosimamiwa na Wizara. Maelekezo na ushauri wao kwa Wizara umezingatiwa, Wizara inaahidi kuendelea kuzingatia maelekezo ya Kamati katika mwaka 2025/2026 kwa maendeleo ya sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari, tunasema Kazi Iendelee. *(Makofi)*

Vilevile, napenda kuwashukuru Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu hususan wakati wa kuwasilisha taarifa mbalimbali zinazohusu Wizara. Wizara, itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya maendeleo ya wananchi kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine namshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kufanya uteuzi wa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi, Mbunge. Kwa niaba ya watumishi wote wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ninampongeza kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa katika nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwako wewe, Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, familia na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na Makamu wa kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Cleopa David Msuya, vilevile kwa kuondokewa na Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni kwa tiketi ya CCM na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani *(WHO)* Kanda ya Afrika. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina majukumu ya kuandaa, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sera zinazohusu mawasiliano, teknolojia ya habari (TEHAMA), posta na mawasiliano ya simu, kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa sera, mipango na miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali kwa wananchi, kufanya tafiti za maendeleo na ubunifu kwenye TEHAMA, kuendeleza wataalamu wa TEHAMA, kuanzisha na kusimamia *postcode*, kusimamia ujenzi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano, kusimamia ulinzi na usalama wa mtandao, kuboresha na kuendeleza utendaji wa rasilimali watu ndani ya Wizara na kusimamia taasisi, programu na miradi ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inasimamia taasisi saba ambazo ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA),* Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL),* Shirika la Posta Tanzania *(TPC),* Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF),* Tume ya TEHAMA *(ICTC),* Tume ya Ulinzi wa Taarifa

Binafsi *(PDPC)* na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano *(TCRA-CCC)*. 5

Mheshimiwa Spika, juu ya ukuaji na mchango wa sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari, kulingana na Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha mwaka 2023, sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari imekua kwa 7.6% mwaka 2023 ikilinganishwa na 7.4% mwaka 2022. Aidha, sekta hii imechangia 1.4% mwaka 2023 kwenye pato la Taifa ikilinganishwa na 1.5% mwaka 2022. Hata hivyo, takwimu hizi zinaonesha kuwa mchango wa sekta ni mdogo ikilinganishwa na uhalisia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari ni muhimili na kichocheo kikuu cha uchumi, katika mwaka 2025/2026 Wizara kwa kushirikiana na wadau wote muhimu wa Ukokotoaji wa Hesabu za Taifa *(System of National Accounts)* ikiwemo ofisi ya Taifa ya Takwimu *(NBS),* inatarajia kuanzisha Akaunti Maalum ya Uchumi wa Kidijitali *(Digital Economy Satellite Account – DESA)* ili kuongeza wigo wa upimaji wa mchango wa sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari kwa lengo la kutambua kwa usahihi mchango wa sekta hii kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa mawasiliano nchini; sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari imeendelea kukua, takwimu zinaonesha kuwa laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka milioni 73.5 Aprili, 2024 hadi laini milioni 90.4 Aprili, 2025 sawa na ongezeko la 22.9%. Watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka milioni 37.3 Aprili, 2024 hadi milioni 49.3 Aprili, 2025 sawa na ongezeko la 32.3%.

Mheshimiwa Spika, watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka milioni 53.7 Aprili, 2024 hadi milioni 66.5 Aprili, 2025 sawa na ongezeko la 23.9%. Aidha, idadi ya watoa huduma wa miundombinu ya mawasiliano imefikia 38 mwezi Aprili, 2025 ikilinganishwa na watoa huduma 27 mwezi Aprili, 2024 hii ni sawa na ongezeko la 40.7%. Watoa huduma za ziada *(Application Services and Value-Added Services)* wamefikia 136 ikilinganishwa

na watoa huduma 122 mwezi Aprili, 2024 sawa na ongezeko la 11.5%.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu unaashiria kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano na teknolojia ya habari katika maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma za mawasiliano. Hii imewezesha wananchi kufikiwa na huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi, kidijitali kama vile huduma za kifedha, afya kwa urahisi na kwa haraka. Vilevile ongezeko la huduma za mawasiliano limechochea ukuaji wa uchumi wa watu na Taifa kwa ujumla hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali imejikita katika kujenga uchumi wa kidijitali.

Mheshimiwa Spika, Wizara Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na wadau wengine imeanza utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa Miaka Kumi kuanzia mwaka 2024 – 2034 ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 29 Julai, 2024. Mkakati huu umeweka misingi ya kulipeleka Taifa kwenye uchumi wa kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA ambapo utekelezaji wa mkakati huu utawezesha kukuza matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma Serikalini. Ili kufanikisha utekelezaji wa Mkakati huu, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kutafsiri mkakati kwa lugha ya Kiswahili ili kuwezesha wananchi wote kushiriki katika utekelezaji wa mkakati pamoja na kutoa elimu kwenye taasisi za Serikali na binafsi kupitia mitandao ya kijamii, redio na televisheni.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa miundombinu ya mawasiliano nchini ni chachu ya kuwezesha Serikali kuwezesha Serikali kufikia uchumi wa kidijitali. Katika hili Serikali chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari ikiwemo kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo hadi sasa Wilaya 109 kati ya Wilaya 139 zimeunganishwa, ujenzi wa miundombinu ya mkongo wa baharini na nchi kavu inayounganisha Tanzania na Mataifa mengine duniani, ujenzi wa Minara 758 na kuanza ujenzi wa minara 636 kote nchini na

kuongezea uwezo minara 304 toka teknolojia ya *2G* kwenda *3G* na *4G* ili kuongeza matumizi ya intaneti.

Aidha, kufikia Aprili, 2025 miundombinu ya brodibendi inayotoa huduma za intaneti kiganjani kwenye maeneo ya watu imefikia 91% kutoka 80% mwezi April, 2024. Pia Serikali inaendelea na mradi wa kufunga mtandao wa intaneti katika maeneo ya wazi 50 yanayotumiwa na wananchi katika shughuli zao za kila siku ili kuongeza na kuhamasisha matumizi ya mtandao wa intaneti nchini. Maeneo hayo ni pamoja na masoko, stendi za mabasi makubwa na madogo na vituo vya mwendokasi.

Mheshimiwa Spika, katika kufikia azma ya  kuwa na uchumi wa kidijitali, Wizara yangu imeratibu ujenzi wa mifumo mitano ya kitaifa; mfumo wa ubadilishanaji taarifa *(Jamii X-change)* kwa upande wa Tanzania Bara na *Zan-Exchange* kwa upande wa Zanzibar ambayo inasimamiwa na Mamlaka za Utambulisho *(NIDA* na *ZCSRA);* mfumo wa utambuzi kidijitali (Jamii Namba); mfumo wa utambuzi wa wateja *(e-KYC);* mfumo wa malipo ya kidijitali *(Jamii Pay);* na mfumo wa usajili na uwezeshaji wa Wadau wa ikolojia ya ya tafiti na ubunifu za TEHAMA ikiwemo kampuni changa wa *Safari Hunt.* Aidha, kwa upande wa kisekta, Wizara imeratibu uboreshaji wa mifumo ya utambuzi na usajili kwenye taasisi za *RITA* na *NECTA*. Ujenzi wa mifumo hii inarahishisha utoaji wa huduma za Serikali na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kufikia lengo la Mheshimiwa Rais la nchi kuwa na *satelite* yake, Wizara imeanza taratibu za kuridhia mikataba miwili ya anga za juu ambayo ni mkataba wa kanuni zinazosimamia shughuli za mataifa katika utafiti, uchunguzi na matumizi ya anga za juu wa mwaka 1967 na mkataba wa usajili wa vifaa ama vyombo vilivyorushwa katika anga za juu wa mwaka 1975. Kukamilika kuridhiwa kwa mikataba tajwa kutatoa fursa kwa Wizara kuandaa Sera ya Anga za Juu na mkakati wake wa utekelezaji ambao utawezesha kuimarisha teknolojia ya anga za juu na *satelite*.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa wastani wa bei ya dakika ndani ya mtandao bila kifurushi (shilingi/dakika) bila

kifurushi zimeendelea kubakia wastani wa shilingi 26 kutoka mwezi Juni, 2024 hadi kufikia mwezi Aprili, 2025 wakati bei ya dakika nje ya mtandao bila kifurushi imeendelea kubakia wastani wa shilingi 28 kutoka mwezi Juni, 2024 hadi kufikia mwezi Aprili, 2025. Mwenendo wa gharama za rejareja za *data* bila kifurushi na kwenye kifurushi zimeendelea kupungua.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika robo ya mwaka inayoishia Machi, 2025 gharama za *data* ndani ya kifurushi zimeshuka kwa kiasi kidogo na kufikia shilingi 2.12 kwa *megabyte* kwa mwezi Aprili, 2025 ikilinganishwa na shilingi 2.16 kwa *megabyte* mwezi Juni, 2024. Usajili wa vikoa umeongezeka kufikia vikoa 33,494 mwezi Aprili, 2025 ukilinganisha na vikoa 30,090 vilivyosajiliwa kipindi kinachoishia Juni, 2024. Hili ni ongezeko la vikoa 3,404 sawa na 11.3%.

Mheshimiwa Spika, niruhusu sasa nifanye mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2024/2025; nikianza na ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 100.7 kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, habari na machapisho ya picha, mabango na majarida. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2025 Wizara imekusanya jumla ya shilingi bilioni 56.2 sawa na 55.8% ya lengo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 iliidhinishiwa kutumia cha shilingi bilioni 180.9. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 38.9 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 24.99 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 13.9 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 142 iliidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo shilingi bilioni 116.4 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 25.6 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 161.6 sawa na 89.3% ya shilingi bilioni 180.9 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge

katika mwaka wa fedha 2024/2025. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 13.4 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 11.1 ni matumizi mengineyo na shilingi bilioni 137.1 ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha shilingi bilioni 78.9 za ndani na shilingi bilioni 58.2 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024 katika kipindi cha Julai, 2024 mpaka mwezi Aprili, 2025, sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari tumefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo: -

(i) Kuandaa rasimu za mapendekezo ya kutunga Sera Mpya ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2025 na kuhuisha Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 na kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi ndani ya Serikali kwa ajili ya kuridhiwa;

(ii) Kufanya mapitio ya kanuni saba za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ambazo ni Kanuni za Maudhui Mtandaoni, Kanuni za Ubora wa Huduma za Mawasiliano, Kanuni za Leseni, Kanuni za Posta, Kanuni za Timu ya Uitikiaji wa Majanga ya Mtandao, Kanuni za Usajili wa Laini za Simu na Kanuni ya Viwango vya Ubora wa Vifaa vya Mawasiliano ya Kielektroniki na usimamizi wa taka zitokanazo na vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki;

(iii) Kuunganisha mifumo 898 ya kutolea huduma kati ya mifumo hiyo mifumo 514 ni ya Serikali na mifumo 384 ni ya sekta binafsi katika kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha mifumo inasomana;

(iv) Kusambaza na kusimika vifaa vya mkutano mtandao *(video conference)* kwenye halmashauri 100 nchini;

(v) Kukamilisha ujenzi minara 482 kati ya minara 758 iliyopangwa kujengwa katika kata 713 sawa na 63.6%

kupitia Mradi wa Tanzania Kidijitali. Aidha, minara 304 kati ya minara yote 304 iliyopangwa kuongezwa nguvu imetekelezwa kwa 100%;

(vi) Kuanza ujenzi wa minara ya simu na redio 636 ambapo hadi Aprili, 2025 minara ya simu 141 imekamilika na katika hiyo minara 68 inatoa huduma za mawasiliano;

(vii) Kukamilika kwa usimikaji wa vifaa *(active installations)* katika maeneo 25 kati ya maeneo 621. Aidha, usimikaji wa vifaa vya *Core Network* na *Datacentre* katika vituo vya *TTCL Dar es Salaam Telephone House* na *TTCL Dodoma Telephone House* umekamilika;

(viii) Kuhakiki anwani za makazi katika halmashauri 13 kati ya hizo halmashauri 11 Tanzania Bara na halmashauri mbili za Zanzibar. Hivyo, kufanya jumla ya halmashauri 41 nchini kufanyiwa uhakiki;

(ix) Kuunganisha mfumo wa *NaPA* na mifumo mingine 13 ya kutolea huduma. Aidha, mifumo mingine saba ipo katika hatua mbalimbali za uunganishwaji;

(x) Kuanza taratibu za ununuzi wa vishikwambi 3,482 kwa ajili ya kuwezesha ukusanyaji na uhakiki wa taarifa za anwani za makazi;

(xi) Kuunda moduli mbili za mfumo wa *NaPA* kwenye vivutio vya utalii na kutoa barua ya utambulisho kidijitali;

(xii) Kukusanya taarifa za anwani za makazi za huduma na vituo vya utalii katika hifadhi 24. Kati ya hizo hifadhi tatu ni za Ngorongoro na 21 ni za *TANAPA*;

(xiii) Kufanya maboresho ya mfumo wa *NaPA* ikiwemo kuwezesha upatikanaji wa huduma za anwani za makazi kupitia *USSD code*;

(xiv) Kujenga uwezo kwa wataalamu na Watendaji wa Serikali za Mitaa 8,010 kati ya wataalamu 31,465;

(xv) Kutoa ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 30 wa Serikali katika vyuo vikuu mbalimbali Uingereza, Ujerumani, Malaysia, Uturuki na Sweden. Aidha, watumishi 450 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika maeneo ya usalama mtandao, *software development, system administration, artificial intelligence* na *block chain* kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali;

(xvi) Kuratibu ujenzi wa mifumo mitano ya kitaifa, yaani Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa *(Jamii X-change* na *Zan-Xchange)* ambayo inasimamiwa na Mamlaka za Utambulisho wa *NIDA* na *ZCSRA*; Mfumo wa Utambuzi wa Kidijitali (Jamii Namba), Mfumo wa Utambuzi wa Wateja *(e-KYC),* Mfumo wa Malipo ya Kidijitali *(Jamii Pay*) na Mfumo wa Usajili na Uwezeshaji wa Wadau wa Ekolojia ya Utafiti na bunifu za TEHAMA zikiwemo kampuni changa *(Startups* wa *Safari Hunt)*. Aidha, kwa upande wa kisekta, Wizara imeratibu uboreshaji wa mifumo ya utambuzi na usajili kwenye taasisi za *RITA* na *NECTA*;

(xvii) Kuandaa miongozo mitano ya usimamizi wa TEHAMA ambayo ni Mwongozo Bora wa Matumizi ya TEHAMA, Mwongozo wa TEHAMA kwenye Makundi Anuai, *Enterprise Architecture Framework, Interoperability na Standardization Framework* na *Digital Public Infrastructure Tanzania technology Stack;*

(xviii) Kukamilisha ujenzi wa kilometa 3,621 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kati ya kilometa 4,442 sawa na 82%. Utekelezaji huu umewezesha kujengwa kwa jumla ya kilometa 13,820 kati ya kilometa 16,280 tangu mradi kuanza. Aidha, ujenzi wa vituo vyote 111 vya kutolea huduma za mkongo umekamilika kwa 100%;

(xix) Kukamilisha ufikishaji wa Mkongo wa Mawasiliano kwenye wilaya 10 za Bahi mkoani Dodoma, Kilindi mkoani Tanga, Chemba mkoani Dodoma, Kilosa mkoani Morogoro, Kwimba mkoani Mwanza, Siha mkoani Kilimanjaro, Mpwapwa mkoani Dodoma, Mlele mkoani Katavi, Malinyi mkoani Morogoro na Kalambo mkoani Rukwa. Hivyo, kufanya wilaya 109 kati ya wilaya 139 sawa na 78% kufikiwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

(xx) Kukamilisha ufikishaji wa Mkongo wa Taifa Mombasa, Kenya kupitia Kituo cha Horohoro - Tanga;

(xxi) Kukamilisha uunganishwaji wa vituo 59 vya *RUWASA* kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

(xxii) Kuunganisha maeneo manne ya huduma za *Wi-Fi* kwenye vituo vya treni ya mwendokasi ya *SGR* vya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma pamoja na Uwanja wa Taifa wa Benjamini Mkapa. Hivyo, kufanya maeneo yaliyounganishwa kufikia 10;

(xxiii) Kukamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Mahiri cha TEHAMA *(Digital Technology Institute)* kitakachojengwa Nala mkoani Dodoma;

(xxiv) Kuhuisha Mfumo wa Takwimu za Makosa ya Mtandao kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi pamoja na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

(xxv) Kuzindua Kampeni ya Usalama Mtandaoni "SITAPELIKI" ili kupunguza utapeli na ulaghai mtandaoni;

(xxvi) Kutoa leseni 2,886 za mawasiliano, kati ya hizo leseni 529 ni za rasilimali namba, leseni 1,850 ni leseni ndogo ndogo na leseni 487 ni leseni kubwa *(individual licences)*;

(xxvii) Kubaini na kuzifungia laini za simu 47,728 pamoja na nambari za Kitambulisho cha *NIDA* 39,028 ambazo zimehusika katika uhalifu;

(xxviii) Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa mkongo *(fibers)* na miundombinu ya watoa huduma za mawasiliano katika mikoa 30 ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani;

(xxix) Kufanya ukaguzi wa vifaa vya kielektroniki 678 kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi. Kati ya vifaa hivyo vifaa 278 vilikidhi vigezo na kuidhinishwa kwa matumizi. Aidha, uhakiki wa vifaa 400 unaendelea;

(xxx) Kuimarisha ushiriki wa Tanzania kikanda na kimataifa ambapo Wizara imeshiriki kwenye Baraza la Uongozi la *ITU*. Mkutano wa *ITU-T* wa *WTSA* mwaka 2024 nchini India; Kongamano la Kimataifa la Anga za Juu lililofanyika Milan, Italy; Mkutano wa Baraza la Uendeshaji wa Posta *(POC)* na Baraza la Utawala la *UPU*;

(xxxi) Kusainiwa kwa mkataba na kukabidhi miundombunu ya Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano kwa Serikali ambapo hadi sasa jumla ya kilometa 336 kati ya kilometa 2,020 zimekabidhiwa;

(xxxii) Kuanza ujenzi wa vituo nane vya kikanda vya ubunifu wa TEHAMA katika Mikoa ya Arusha, Mwanza, Tanga, Lindi, Dodoma, Mbeya na Zanzibar;

(xxxiii) Kusajili wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi 2,829; na

(xxxiv) Kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Wizara Mtumba, Jijini Dodoma ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 ujenzi umefikia 95%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa majukumu mwengine ya sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari

yameainishwa kwenye ukurasa wa 15 hadi 38 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba niwasilishe Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2025 /2026.

Mheshimiwa Spika, Wizara pamoja na taasisi zake zimeandaa mpango wake kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025; maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa wakati akihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; ahadi na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa kitaifa, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 mpaka 2025/2026); Dira ya Taifa ya Maendeleo na Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2021/2022 mpaka 2025/2026. Aidha, Wizara imezingatia Mwongozo wa Mpango wa Bajeti wa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vipaumbele vya bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2025/2026; Wizara imejikita katika utekelezaji wa vipaumbele vifuatavyo: -

(i) Kutunga, kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa miongozo inayosimamia sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari;

(ii) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na posta kote nchini katika kukamilisha ujenzi wa minara 758 na kuendeleza ujenzi wa minara 636 nchini;

(iii) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha biashara mtandao kwa kuhakiki taarifa za anuani za makazi katika halmashauri 28 na kusimamia uundaji wa mifumo ya kidijitali utakaowezesha biashara mtandao *(e-Commerce);*

(iv) Kuimarisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa uchumi wa kidijitali kwa kuunganisha wilaya 11 kwenye Mkongo wa Taifa;

(v) Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na nchi jirani ya Congo DRC kupitia Ziwa Tanganyika na kuunganisha wateja 90,000 kwa huduma ya *fiber* mlangoni kwako *(broadband)* kufikia Juni, 2026;

(vi) Kuimarisha ulinzi na usalama wa anga ya mtandao;

(vii) Kujenga uelewa wa wananchi juu ya ulinzi wa *data* na faragha zao na jinsi ya kukabiliana na matukio ya utapeli na wizi mtandaoni;

(viii) Kuwezesha upatikanaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Makosa ya Kimtandao nchini na kuongeza uwezo wa kitengo cha uchunguzi wa kidijiti kwa Jeshi la Polisi katika Ofisi ya Makao Makuu katika Kanda ya Mbeya na Mwanza;

(ix) Kutoa elimu juu ya miongozo na miundombinu muhimu ya TEHAMA na kuimarisha ulinzi wa miundombinu hiyo;

(x) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuchochea ubunifu na kuimarisha ustawi wa kampuni changa *(startups);*

(xi) Kusimamia uanzishwaji wa vituo viwili vya TEHAMA; cha Nala (Dodoma) na Buhigwe (Kigoma);

(xii) Kuwezesha uanzishwaji wa vituo vinne vya kukuza ubunifu wa TEHAMA katika ngazi ya wilaya; na

(xiii) Kuwezesha uanzishwaji wa vituo viwili vinavyotembea vya kupata taarifa za TEHAMA *(Mobile Access Centres)* na kusimamia utekelezaji wa vituo nane vya ubunifu wa kidijitali kama nilivyovitaja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, mipango mingine ya sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari inafafanuliwa kwa kina katika ukurasa wa 39 hadi ukurasa wa 54 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu yangu katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi, Mbunge na Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Naibu Waziri huyu amekuwa msaada mkubwa kwangu katika kufanya kazi za kila siku, amekuwa akijituma na amekuwa akishirikiana na Waheshimiwa Wabunge. Ninamuombea kila la heri, Mwenyezi Mungu amtangulie katika mtihani unaotukabili wote Novemba mwaka huu. Ninaamini atarudi ndani ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumshukuru Ndugu Mohammed Khamis Abdulla, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Ndugu Mohammed Khamis Abdulla kwenye Kamati ya Bunge wanamuita mtaalamu. Ni Katibu Mkuu mkimya, lakini amekuwa msaada mkubwa kwenye utendaji wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumshukuru Ndugu Nicholaus Merinyo Mkapa, Naibu Katibu Mkuu. Vilevile, ninaomba niwashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo katika Wizara; Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi za Taasisi zinazosimamiwa na Wizara; viongozi wa taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na taasisi kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Hakika mmekuwa msaada mkubwa, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara katika kutekeleza majukumu yake imeendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari. Kipekee napenda kushukuru mashirika yafuatayo; Shirika la Umoja wa Posta Afrika *(PAPU)*; Shirika la Umoja wa Posta Duniani *(UPU);* Shirika la Umoja wa

Mataifa la Mawasiliano *(ITU);* Benki ya Dunia kupitia dirisha la Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa *(IDA);* Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(AFD)* na Ubalozi wa Korea Kusini nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazishukuru pia Jumuiya za Kikanda na Kimataifa za Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya *(EU)* kwa ushirikiano wao katika masuala ya kikanda na kimataifa yanayohusu sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na washirika wa maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari inaendelea kuchangia katika kutimiza malengo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuwashukuru watoa huduma za mawasiliano kutoka katika makampuni ya simu ya Airtel, Vodacom, Viettel, Honora, *TISPA* na *TTCL* kwa utoaji na usambazaji wa huduma za mawasiliano nchini. Napenda pia kuzitambua taasisi za NMB, CRDB na *Tanzania Startup Association* kwa mchango wao wa kuendeleza na kukuza bunifu za TEHAMA nchini.

Kwa kumalizia natambua mchango wa wadau wote wa sekta ikiwemo Kampuni ya Minara Tanzania, *Herios Tower,* Huawei, *Softnet, Telecom Associate*, *TanzTech* pamoja na kampuni ya wazawa wa Kitanzania ya *Raddy Fibre,* kampuni ambayo iko Mkuranga, Tanzania inayotengeneza nyaya za *optic fiber* lakini hivi punde inaanza utengenezaji wa *laptop*, simu za kiganjani, simu janja na *tablets* na tutaitembelea hivi karibuni katika kuimarisha upatikanaji wa simu janja nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na washirika wa maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa shughuli za maendeleo zilizopangwa kutekelezwa zinatekelezwa na kuwezesha sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari kuchangia katika kutimiza Dira ya Taifa ya kufikia Uchumi wa Kati, wa Juu ifikapo mwaka 2026.

Mheshimiwa Spika, mwisho na kwa umuhimu wa kipekee naomba nitumie fursa hii kuwashukuru kidhati wananchi wangu wa Jimbo la Ukonga kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati katika kuliletea maendeleo kwenye jimbo letu. Kipekee ninaomba niwashukuru wananchi wa Kata zote 13; Kata ya Msongola, Kata ya Zingiziwa, Kata ya Chanika, Kata ya Buyuni, Kata ya Pugu, Kata ya *Pugu Station,* Kata ya Gongo la Mboto, Kata ya Ukonga, Kata ya Kipunguni, Kata ya Majohe, Kata ya Kivule, Kata ya Mzinga na Kata ya Kitunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa wamekuwa wakinivimilia katika utekelezaji wa majukumu yangu ya Kiserikali na mimi ninaomba kuwashukuru sana na ninaomba kuwaahidi nguvu bado ninayo na uwezo ninao, tarehe 28 Juni, saa 12.30 nitakuwa kwenye Ofisi ya Katibu wa Chama wa Wilaya kuchukua fomu ili kuendelea kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninaomba kumshukuru mke wangu Bi. Mariam Bakari Silaa. Binti huyu wa Kitanga amekuwa zaidi ya mke kwangu, amekuwa rafiki, amekuwa mfariji, amekuwa mlezi, ninamshukuru sana kwa kunivumilia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha niishukuru familia yangu ambayo leo imewakilishwa na mwanangu Simba William Silaa pamoja na ndugu zangu, jamaa na marafiki wote kwa ujumla kwa kunipa nguvu na moyo wa kutekeleza majukumu yangu katika Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba kwa muhtasari niwasilishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inakadiria kukusanya kiasi cha shilingi 100,369,242,000 ambazo zinatokana na mauzo ya huduma ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba

kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi 291,533,139,000 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu na vipaumbele vya Wizara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, shilingi 14,485,656,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo shilingi 6,958,609,000 ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi 7,527,047,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Shilingi 277,470,483,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na katika fedha hizo shilingi 98,480,905,000 ni fedha za ndani na shilingi 178,566,578,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na utaratibu wetu, sasa Mwenyekiti atakuja kunipokea.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma M. Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa ninamuita Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Mtaturu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba Taarifa yote ya Kamati, iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowekwa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza na utangulizi; ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne: -

(i) Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi, ambao unahusu msingi wa muundo wa taarifa;

(ii) Sehemu ya pili inahusu uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi wa mwaka wa fedha 2025/2026;

(iii) Sehemu ya tatu inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Serikali; na

(iv) Sehemu ya nne ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi, utekelezaji pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025; wakati Bunge lako lilipopitisha bajeti ya Fungu 68 kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imepitia taarifa ya utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati na kubaini kwamba kuna baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati ambayo utekelezaji wake ni endelevu na mengine hayajatekelezwa kikamilifu. Hivyo Kamati inasisitiza Serikali kufanyia kazi ushauri uliotolewa kama ifuatavyo: -

(a) Kamati iliishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa ujenzi wa vituo vya bunifu vya TEHAMA nchini. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeanza ujenzi wa vituo nane vya kukuza bunifu za TEHAMA kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya, Mjini Magharibi Zanzibar na kazi hiyo itakamilika mwezi Septemba, 2025.

(b) Kamati iliishauri Serikali kupitia upya mkataba wa ujenzi wa miundombinu ya njia ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaotekelezwa kati ya *TANESCO* na *TTCL*. Katika kutekeleza ushauri huu, Kamati imepokea taarifa kuwa *TTCL* na *TANESCO* wamehuisha na kupanua wigo wa ushirikiano kupitia mkataba maalumu wa kibiashara ambao unatoa fursa sawa ya matumizi ya pamoja kwa taasisi zote mbili nchini kote. Aidha, mkataba husika umewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya upekuzi.

(c) Kamati iliishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kupeleka Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye nchi jirani ikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kuongeza Pato la Taifa. Kamati imetaarifiwa kwamba mchakato wa suala hilo bado unaendelea. Kamati inaona kuwa kasi ya utekelezaji wa jambo hili ni ndogo hivyo msukumo unahitajika ili kukamilisha malengo ya mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kuhusu ukusanyaji wa maduhuli: -

(i) Kamati imebaini kwamba Wizara hii iliidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 100.7 kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, habari na machapisho ya picha, mabango, majarida, ambapo hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilikuwa

imekusanya shilingi bilioni 49.626 sawa na 49.3% ya lengo.

(ii) Upande wa taasisi zilizo chini ya Wizara zilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 691.067. Hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilikusanya shilingi bilioni 354.304 sawa na 51.3% ya lengo.

(iii) Imebainika kuwa baadhi ya taasisi zilikusanya maduhuli kwa kiwango cha kuridhisha kama vile *UCSAF* 92%, *TCRA* kwa 79% na *TCRA-CCC* 75%. Aidha, taasisi ambazo hazikuwa na makusanyo ya kuridhisha hadi kufikia Februari, 2025 ni *TTCL* kwa 35%, *ICTC* 39%, Shirika la Posta 44% na *PDPC* 10.8%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inazipongeza taasisi zilizofanya vizuri kwenye makusanyo na inaendelea kuishauri Serikali kuboresha mifumo ya makusanyo na ufuatiliaji ili kuongeza mapato ya Serikali, pia itathimini uwezo wa kila taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi mwezi Februari, 2025. katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 180.926. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 38.906 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 142.019 kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2025 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 118.515 sawa na 65.5% ya lengo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 22.663 ni fedha za matumizi ya kawaida sawa na 58.25% ya bajeti iliyoidhinishwa na shilingi bilioni 95.851 zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na 67.49% ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wastani hali ya upatikanaji wa fedha kwa Wizara unaridhisha kwani hadi kufikia mwezi Februari, 2025, fedha iliyopokelewa ilikuwa ni wastani wa juu ya 66.5%. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kwamba fedha

zote zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa kabla ya mwaka wa fedha 2024/2025 kuisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; Kamati imebaini kwamba baadhi ya miradi ya maendeleo ilipokea fedha kwa wakati na kuvuka matarajio wakati miradi mingine ilipokea fedha pungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba Mradi wa Mawasiliano Vijijini ulikuwa umepokea jumla ya 275.5% ya makadirio, na hivyo kuwezesha Serikali kusaini mkataba wa fedha mnamo tarehe 27 Septemba, 2024 baina ya Wizara ya Fedha na Benki ya Exim ya China kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine Kamati imebaini kwamba miradi mingine ilikuwa imepokea fedha pungufu ambapo, kwa wastani hadi kufikia mwezi Februari, 2025. miradi hiyo ni Anwani za Makazi na Postikodi ulipokea 10%; ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA *(ICT Park)* ulipokea 18.7%; Kuimarisha Uwezo wa Taasisi katika utekelezaji wa majukumu ulipokea kwa 33.6%; Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA ulipokea 47.3%; na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulipokea 50%. Kamati inaipongeza Serikali kwani wastani wa mapokezi ya fedha za miradi ya maendeleo ulikuwa ni wa kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025; Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi ili kujionea utekelezaji wa miradi iliyopo chini ya Wizara hii iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025 miradi iliyokaguliwa ni miradi ya Maabara ya Uidhinishaji wa Vifaa vya Kielektroniki *(TAL)*; Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo Vidogo vya kuendeleza ubunifu wa TEHAMA *(ICT- Park)*; na Kituo cha Taifa cha Kutunza *Data (NIDC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi iliyotembelewa na Kamati; mtiririko wa utoaji wa fedha kwenye baadhi ya miradi; Kamati imebaini kwamba kuna

changamoto ya utoaji wa fedha kwenye baadhi ya miradi kama vile mradi wa ujenzi wa jengo la Kituo Kikuu cha Ubunifu cha Umoja wa Kimataifa wa Mawasiliano fedha zimepokelewa kwa 18.7%, Anwani za Makazi na Postikodi imepokea 10%; Kuimarisha Uwezo wa Taasisi imepokea 33.6%; na Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA ni 47.3%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa minara ya mawasiliano; hadi kufikia Februari, 2025, *UCSAF* ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi bilioni 40.051 ambayo ni sawa na 92% ya lengo. Makusanyo hayo ni kutoka vyanzo vya mapato, ambavyo ni ruzuku toka Serikalini, tozo za huduma, ruzuku toka *TCRA* na wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba mfuko unaendelea na ujenzi wa minara 758 katika kata 713 nchini. Hadi mwezi Februari, 2025 minara 443 imejengwa sawa na 58.4%. Kati ya minara iliyojengwa minara 417 sawa na 55% inatoa huduma za mawasiliano. Aidha, minara iliyobaki ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya mradi huu na inaendelea kutoa ushauri kuwa fedha ziendelee kutolewa kwa wakati ili kukamilisha miradi iliyobakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC);* moja kati ya jambo ambalo Kamati ililifanyia tathmini ni ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka Tanzania hadi *DRC*. Kamati ilipokea taarifa kuwa shirika limekamilisha uchambuzi wa zabuni na majadiliano ya mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kuanzia Kigoma, Tanzania hadi Kalemie, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)*. Aidha, shirika linakabiliwa na changamoto ya uhaba na ubovu wa miundombinu ikiwemo barabara hususani maeneo ya vijijini. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ujenzi ili mkongo ujengwe kwa manufaa ya kukuza uchumi wa nchi na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio na makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake inakadiria kukusanya shilingi bilioni 885.762 kiwango hiki ni ongezeko la shilingi bilioni 93.995 sawa na 11.87% ukilinganisha na shilingi bilioni 791.767 iliyopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kipekee Kamati inazipongeza taasisi zilizopo chini ya Wizara, ambazo zimeongeza wigo wa makadirio ya makusanyo. Hatua hii itaongeza pato la Serikali na kuchochea uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya matumizi ya mwaka wa fedha 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 291.533 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 14.485 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 277.047 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara imeongezeka kwa shilingi bilioni 110.606 sawa na 161% kutoka shilingi bilioni 180.926 iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 hadi kufikia shilingi bilioni 291.533 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Fedha iliyotengwa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo imeongezeka kwa shilingi bilioni 135.027 sawa na 195%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za maendeleo na inatoa rai kwamba fedha zitolewe kwa wakati ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa vipaumbele vya Serikali kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2025/2026 bajeti imepungua kwa shilingi bilioni 24.421 sawa na 37% ukilinganisha na bajeti hiyo kwa

mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo ilikuwa ni shilingi bilioni 38.906 na sababu ya punguzo hilo ni kutokana na mabadiliko yaliyofanyika ya Idara ya Habari na Maelezo kuhamishiwa Wizara ya Elimu na Mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 277.047 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni nyongeza kwa 195% ukilinganisha na bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 98.480 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 178.566 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoni na ushauri; Kamati inaipongeza Serikali kwa ufanisi mkubwa, imeendelea kutoa fedha za kutekeleza majukumu mbalimbali ya Fungu 68 - Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari hususani katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali: -

(a) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika kuimarisha huduma za mawasiliano na kuhakikisha kuwa yanapatikana kwa urahisi kwa manufaa ya wananchi;

(b) Kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya utendaji kazi utakaochochea kuboresha huduma za Sekta ya Mawasiliano na matumizi ya TEHAMA nchini kwa kuwa sekta hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi;

(c) Kuunganisha taasisi za Serikali na miundombinu ya mtandao wa kasi; na

(d) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu na kuwepo kwa thamani ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza usimamizi madhubuti kwa taasisi ili ziweze kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na hatimaye kuboresha huduma za

Mawasiliano na TEHAMA katika kuongeza mapato ya Serikali. Maoni na ushauri mahususi.

(a) Ulaghai katika mitandao ya mawasiliano; katika Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 Serikali imeeleza nia ya kuimarisha mfumo wa TEHAMA wa udhibiti usalama na mapato katika Mawasiliano. Hata hivyo tatizo la uhalifu na utapeli kwenye mitandao ya mawasiliano bado linaendelea kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa pamoja na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na mamlaka husika, jitihada zaidi zinahitajika ili kutoa ufumbuzi wa kudumu sambamba na kuzuia jumbe fupi zinazotumwa bila idhini au matakwa ya mteja. Aidha, Wizara husika ishirikiane na makampuni ya mitandao ya simu pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ili kumaliza tatizo hilo.

(b) Fedha kutototolewa kwa wakati kwenye baadhi ya miradi iliyoko chini ya Wizara; pamoja na malengo mema ya kuanzishwa kwa mradi wa ujenzi wa vituo vya kuendeleza ubunifu na utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA, kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha kwenye miradi hii, hali hii inadhoofisha jitihada za kukuza uchumi na kutatua tatizo la ajira kwa vijana hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha za miradi hiyo zinatolewa kwa wakati ili kufikia malengo kwa wakati.

(c) Kutokuwepo kwa sera na sheria inayohusu bunifu za TEHAMA; moja ya changamoto inayoikabili vituo vya ubunifu za TEHAMA nchini ni kutokuwa na sera na sheria katika suala la uendeshaji na usimamizi wa vituo hivyo, jambo linalopunguza kasi ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuleta Bungeni muswada utakaowezesha utungwaji wa sheria husika ili kuweka mazingira wezeshi yenye kutoa ajira na kutambua bunifu za wananchi ipasavyo. Aidha, ujenzi wa vituo hivyo uende sambamba na kuongeza idadi ya wataalamu na wakufunzi wa kuendesha vituo hivyo ili iweze kuleta tija iliyokusudiwa.

(d) Gharama kubwa za uendeshaji wa kituo cha kutunza *data;* kumekuwa na changamoto katika uendeshaji wa mradi wa vituo vya kutunzia *data* nchini kunakosababishwa na matumizi makubwa ya umeme, ukomo wa matumizi wa baadhi ya vifaa vya miundombinu ya uendeshaji wa kituo cha kutunzia *data (life span)* na idadi ndogo ya vifaa vya kuhifadhia *data (racks)* ili kuendelea na utoaji wa huduma ya upangaji wa nafasi *(colocation)*. Hali hii inasababisha uwepo wa gharama kubwa katika uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti wa kutosha ili kubaini eneo lenye mazingira rafiki yenye hali ya baridi ili kujenga kituo kipya, hii itasaidia kupunguza gharama za umeme unaotumika kuendesha mitambo.

(e) Kutumia fursa ya kuwa na maabara ya vifaa vya mawasiliano ya kieletroniki; imebainika kuwa Tanzania ndiyo nchi pekee inayomiliki mtambo wa upimaji wa bidhaa za kielektroniki katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki, fursa hii ikitumiwa vizuri inaweza ikaingiza kiasi cha fedha kutoka kwa majirani zetu ambao hawana aina hii ya maabara, hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kutumia fursa hii ipasavyo ili kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iziunganishe mamlaka za udhibiti ubora wa bidhaa nchini kwa kutumia mfumo wa pamoja *(one single system)* ili kuleta udhibiti wa bidhaa za kielektoniki nchini, pia ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kwa watumiaji wa

vifaa hivyo na kubaini kama kuna ukiukwaji wowote ili kuondoa athari zinazoweza kutokea katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho na shukrani; nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa namna ya pekee naendelea kukushukuru na wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa na msaada mkubwa katika uendesahji bora wa shughuli za kila siku. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu aidha pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Spika, inamtakia kila la kheri Spika wetu katika uchaguzi unaokuja wa mwaka huu. Tunajua Jimbo la Mbeya limegawanya, tunajua kuna Uyole, lakini pamoja na ile Mbeya Mjini, lakini namjua Mheshimiwa Spika, wewe ni kama vile anavyocheza Ellie Mpanzu pamoja na Mohamed Hussein wanaweza kucheza namba yoyote, kwa hiyo, tunamtakia kila la kheri kwa jimbo lolote atakaloamua kugombea pale Mbeya tunaamini uwezo wake ni mkubwa na Wana-Mbeya wanampenda na hakuna matatizo yoyote, tunamtakia kheri arudi aje aendeshe Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, namna anavyosaidia kutekeleza majukumu yake, pamoja na Mheshimiwa Mwenyeviti na Waheshimiwa Wenyeviti wenzio wenzio ambao mmekuwa mkifanya kazi nzuri ya kuliongoza Bunge letu Tukufu.

Kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako Tukufu. Kipekee katika eneo hili tunampongeza sana Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Moshi Kakoso, amekuwa mlezi, amekuwa akitulea na akituelekeza mambo mbalimbali kwa uzoefu wake alionao na tunamuombea kila la kheri jimbo lake linaitwa Tanganyika sasa ili aende akafanye vizuri na arudi hapa kwenye Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwa hakika maoni na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika

kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe hao, lakini kutokana na muda sitasoma majina yao yote ila naomba yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* ili waweze kutambulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Jerry William Silaa ambaye alikuwa ni Mbunge wa Ukonga, lakini sasa limegawanya na jimbo lingine lile, ninamtakia kila la kheri kule atakapoamua kugombea na hapa ametaja kata zote bila hata kusoma, hii inaonesha kwamba ana uwezo mkubwa wa kuhudumia jimbo lile bila tatizo lolote. Kwa sababu tunakujua wewe una uwezo wa kucheza vizuri katikati kama mchezaji wa timu ile ingine inayosema hatutacheza, lakini naamini utafanya vizuri katika Bunge hili utarudi na kufanya kazi na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushirikiano ambao umeendelea kuipatia Kamati ukisaidiwa na dada yangu Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri, mkimya lakini mambo yake makubwa tunakutakia kila la kheri pale Mbeya. *(Makofi)*

Aidha, niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wakiondozwa na Ndugu Mohammed Abdullah ambaye tunamuita mtaalamu pamoja na Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Nicholaus Mkapa katika Kamati mlikuwa mna mchango mkubwa na watendaji wote ambao mpo hapa ambao mnasimamia Wizara hii, kwa hakika mmeifanya sekta ya mawasiliano na TEHAMA na inaendelea kuwa inaweka mchango mkubwa katika nchi yetu na inaendelea tunaendelea kuwatia moyo ili waweze kufanya kazi zaidi kwa bidii kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini sio kwa umuhimu, maana yake mwisho kabla ya mwisho siyo kwa umuhimu nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge - Ndugu Baraka Leonard kwa

kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho katika shukrani zangu nichukue nafasi hii kuwashukuru sana, sana watu muhimu wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki ambao sasa hivi tunaita Ikungi Mashariki kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa, tumefanya makubwa pamoja, maendeleo leo yanaonekana katika Jimbo la Singida Mashariki ambalo sasa linaitwa Ikungi Mashariki. Niwaombe tuendelee kuwa wamoja, tusiyumbishwe, tushikamane na wanasema katika mambo muhimu usiteme *Big G* kwa karanga za kuonjeshwa kwa sababu utakuja kupata matatizo makubwa twendeni pamoja tuendelee kuifanya kazi nzuri tuliyoianza tuimalize pamoja kwani bado nina nguvu tele na tarehe 28 Juni mapema ninakwenda kuchukua fomu kwa ajili ya kwenda kuomba ridhaa tena ya chama changu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Kamati kuhusu hoja; baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono 100%. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne (4): -

(i) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambayo inaeleza kuhusu Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

(ii) Sehemu ya pili ni kuhusu uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iii) Sehemu ya tatu ni maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Serikali; na

(iv) Sehemu ya nne ni hitimisho

**1.2 Namna Kamati Iliyotekeleza Majukumu Yake**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti mbalimbali yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya **Fungu 68 - Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilifanya yafuatayo: -

(a) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 (Kanuni ya 117 (1));

(b) Kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 (Kanuni ya 117 (2);

(c) Kupokea na kufanya uchambuzi wa Randama ya Wizara (Kanuni ya 115 (1)); na

(d) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SEHEMU YA PILI**

**2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**2.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** wakati Bunge lako lilipopitisha bajeti ya **Fungu 68** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imepitia taarifa ya utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati na kubaini kwamba, kuna baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati ambayo utekelezaji wake ni endelevu na mengine hayajatekelezwa kikamilifu. Hivyo Kamati inasisitiza Serikali kufanyia kazi ushauri uliotolewa kama ifuatavyo: -

(a) Kamati ilishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa ujenzi wa vituo vya bunifu vya TEHAMA nchini. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, Serikali imeanza ujenzi wa vituo nane (8) vya kukuza bunifu za TEHAMA

kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya, Mjini Magharibi Zanzibar na kazi hiyo itakamilika mwezi Septemba, 2025.

(b) Kamati iliishauri Serikali kupitia upya mkataba wa ujenzi wa miundombinu ya njia ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaotekelezwa kati ya *TANESCO* na *TTCL*. Katika kutekeleza ushauri huu, Kamati imepokea taarifa kuwa, Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)* na kampuni ya umeme ya *TANESCO* wamehuisha na kupanua wigo wa ushirikiano kupitia mkataba maalumu wa kibiashara ambao unatoa fursa sawa ya matumizi ya pamoja *(infrastructure sharing)* kwa taasisi zote mbili nchini kote. Aidha, mkataba husika umewasilishwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya upekuzi.

(c) Kamati iliishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kupeleka Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye nchi jirani ikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kuongeza pato la Taifa. Kamati imetaarifiwa kwamba, mchakato wa suala hilo bado unaendelea. Kamati inaona kuwa kasi ya utekelezaji wa jambo hili ni ndogo hivyo msukumo unahitajika ili kukamilisha malengo ya mradi.

## 2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025 kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, Wizara hii iliidhinishiwa kukusanya **Sh. Bilioni 100.7** kutokana na Mauzo ya Huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, na vyanzo vingine. Hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilikuwa imekusanya **Sh. Bilioni. 49.626** sawa na **asilimia 49.3** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa malengo ambayo Wizara ilijiwekea, ilitarajiwa kwamba, mauzo ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pekee yangeweza kuipatia Wizara mapato ya takribani **Sh. Bilioni 80.** Hata hivyo, kiasi cha fedha kilichokusanywa kufikia Februari, 2025 ni **Sh. Bilioni 40.1** sawa na **asilimia 50** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa Upande wa taasisi zilizo chini ya Wizara, zilikadiriwa kukusanya **Sh. Bilioni 691.067.** Hadi kufikia Februari, 2025, Wizara ilikusanya **Sh. Bilioni 354.304** sawa na **asilimia 51.3** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa wastani hali ya makusanyo ya Wizara na taasisi zilizo chini yake sio ya kuridhisha kwani yapo chini ya wastani ambapo ni robo ya tatu ya Mwaka wa bajeti ilitakiwa angalau yafike wastani wa **asilimia 66.6.** Hata hivyo, kuna baadhi ya taasisi zilikusanya maduhuli kwa kiwango cha kuridhisha kama vile UCSAF **asilimia 92,** TCRA kwa **asilimia 79** na TCRA-CCC **asilimia 75.** Aidha, taasisi ambazo hazikuwa na makusanyo ya kuridhisha hadi kufikia Februari, 2025 ni TTCL kwa **asilimia 35,** ICTC asilimia 39, Shirika la Posta **asilimia 44,** PDPC **asilimia 10.8.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inazipongeza taasisi zilizofanya vizuri kwenye makusanyo na inaendelea kuishauri Serikali kuboresha mifumo ya makusanyo na ufuatiliaji ili kuongeza mapato ya Serikali, pia itathimini uwezo wa kila taasisi.

### 2.3 Uchambuzi Kuhusu Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2025

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya **Sh. Bilioni 180.926.** Kati ya Fedha hizo, **Sh. Bilioni 38.906** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. Bilioni 142.019** kwa Miradi ya Maendeleo.

**KIELELEZO NA 1: MCHANGANUO WA HALI YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KUFIKIA FEBRUARI, 2025**

| BAJETI YA MAENDELEO | MAKADIRIO 2024/2025 | MAPOKEZI FEBRUARI, 2025 | % |
|---|---|---|---|
| FEDHA ZA NDANI | 116,469,894,000 | 64,013,787,953.93 | 54.96 |
| FEDHA ZA NJE | 25,550,000,000 | 31,837,415,900.00 | 124.60 |
| **JUMLA KUU** | **142,019,894,000** | **95,851,203,853.93** | **67.49** |

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2025 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Sh. Bilioni 118.515** sawa na **asilimia 65.5** ya lengo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, kati ya fedha zilizopokelewa, **Sh. Bilioni 22.663 ni** fedha za matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 58.25** ya bajeti iliyoidhinishwa na **Sh. Bilioni 95.851** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 67.49** ya bajeti iliyoidhinishwa **(Kama inavyoonyesha kwenye Kielelezo Na.1)**

**KIELELEZO NA 2:** Mchanganuo wa Hali ya Mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida kufikia Februari, 2025

| BAJETI | MAKADIRIO 2024/2025 | MAPOKEZI FEBRUARI, 2025 | % |
|---|---|---|---|
| **1. MATUMIZI YA KAWAIDA** | | | |
| MISHAHARA | 24,997,474,000 | 12,708,698,377.33 | 50.8% |
| MATUMIZI MENGINEYO | 13,909,189,000 | 9,955,164,825.73 | 71.6% |
| **JUMLA (O.C)** | **38,906,663,000** | **22,663,863,203.06** | **58.25%** |
| **2. BAJETI YA MAENDELEO** | | | |
| FEDHA ZA NDANI | 116,469,894,000 | 64,013,787,953.93 | 54.96% |
| FEDHA ZA NJE | 25,550,000,000 | 31,837,415,900.00 | 124.60% |
| **JUMLA (MAENDELEO)** | **142,019,894,000** | **95,851,203,853.90** | **67.49%** |

**Mheshimiwa Spika,** kwa wastani, hali ya upatikanaji wa fedha kwa Wizara unaridhisha kwani hadi kufikia Februari, 2025, fedha iliyopokelewa ilikuwa ni wastani wa juu ya **asilimia 66.5.** Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kwamba, fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa kabla ya Mwaka wa fedha 2024/2025 kuisha.

### 2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba baadhi ya miradi ya maendeleo, ilipokea fedha kwa wakati na kuvuka matarajio wakati miradi mingine ilipokea fedha pungufu.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Tanzania ya Kidigitali ulipokea **asilimia 128** ya lengo hadi kufikia Februari, 2025. Fedha hizi ni kutoka nje zimewezesha ujenzi unaoendelea mfano ujenzi wa Minara ya Mawasiliano na utekelezaji wa Anwani za Makazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba Mradi wa Mawasiliano Vijijini ulikuwa umepokea **asilimia 275.5** ya makadirio, na hivyo kuwezesha Serikali kusaini mkataba wa fedha mnamo tarehe 27 Septemba, 2024 baina ya Wizara ya Fedha na benki ya Exim ya China kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano nchini. Pia imewezesha ujenzi wa minara *(tower erection)* 108 kati ya 621 na minara 34 imeanza kutoa huduma.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Kamati imebaini kwamba, miradi mingine ilikuwa imepokea fedha pungufu ambapo, kwa wastani, hadi kufikia Februari, 2025. Miradi hiyo ni Anwani za Makazi na Postikodi ulipokea **asilimia 10,** ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA (ICT Park) ulipokea **asilimia 18.7,** Kuimarisha Uwezo wa Taasisi katika utekelezaji wa majukumu ulipokea kwa **asilimia 33.6,** Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA ulipokea **asilimia 47.3** na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulipokea **asilimia 50.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwani wastani wa mapokezi ya fedha za miradi ya maendeleo ulikuwa ni wakuridhisha.

### 2.5 Ukaguzi wa Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025

#### 2.5.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika,** katika kutathimini utekelezaji wa mpango wa maendeleo, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1), Kamati ilifanya

ziara ya ukaguzi ili kujionea utekelezaji wa miradi iliyopo chini ya Wizara hii iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ifuatavyo:-

**2.5.2 Miradi iliyokaguliwa**
**(a) Mradi wa maabara ya uidhinishaji wa vifaa vya Mawasiliano ya kielectroniki - TAL**

**Mheshimiwa Spika,** dhumuni la uanzishwaji wa maabara hii ni kuhakikisha kuwa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki vinatengenezwa au kuingizwa nchini vinakidhi viwango vya kitaifa, kikanda na kimataifa.
**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi huo na kuelezwa kuwa, Tanzania ni moja kati ya nchi 12 barani Afrika ambazo zina maabara ya uidhinishaji wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki, nchi hizo ni Tunisia, South Afrika, Ghana, Nigeria, Cameroon, Benin, Guinea, Togo, Senegal, Mali and Mauritania. Mradi huu ulianza kutekelezwa kuanzia mwezi Aprili, 2023 hadi tarehe 27 Machi, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** gharama za mradi huu ni **Sh. Bilioni 7.527** mpaka sasa, kati ya fedha hizo **Sh. Bilioni 1.496** ni kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa jengo la Maabara za Uidhinishaji wa Vifaa vya Mawasiliano, na **Sh. Bilioni 6.031** ni gharama ya ununuzi wa mitambo na usimikaji.

**Mheshimiwa Spika,** mpaka sasa mradi huu una maabara ya kupima mawimbi ya redio (radio frequency) na maabara ya kupima kiwango cha mionzi *(specific absorption rate)*.

**Mheshimiwa Spika,** tangu mwezi machi, 2024 tayari TCRA imefanikiwa kupima sampuli za vifaa 148 *(kwa modeli)* zikiwemo simu za mkononi na vishkwambi *(tablets)* na matokeo yalionyesha sampuli 6 hazikukidhi vigezo vya kutumika hapa nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa teknolojia inakua kwa kasi hivyo kupelekea mabadiliko ya mara kwa mara kwenye vifaa vya maabara ambavyo gharama yake ni kubwa.

**(b) Mradi Na. 4292 - Ujenzi wa kituo kikuu na vituo vidogo vya kuendeleza ubunifu katika TEHAMA (ICT Park)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeelezwa kuwa mradi huu ulitengewa kiasi cha **Sh. Bilioni 4,** hadi kufikia Februari 2025 fedha iliyopokelewa ni **Sh. Milioni 749.250** sawa na **asilimia 15.9** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** mradi umepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Kuandaa rasimu za miongozo mitano kwa ajili ya miundombinu muhimu ya TEHAMA, ambayo inajumuisha uendeshaji, usimamizi wa vihatarishi, ukaguzi, kukabiliana na majanga pamoja na mwongozo wa uhalisia na uadilifu wa data;

(ii) Kuandaa mkakakati wa taifa wa usalama mtandao ulioboreshwa; na

(iii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu ulinzi na usalama wa mtandao katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam, Mwanza, Tabora na Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** mradi una changamoto zifuatazo: -

(i) Kutokuwepo kwa sera na sheria inayohusu bunifu za TEHAMA; na

(ii) Fedha kuchelewa kutolewa kwa wakati hivyo, mkandarasi kutokamilisha ujenzi kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo malipo; na

**(c) Kituo Cha Taifa cha Kutunza Data - (NIDC)**

**Mheshimiwa Spika,** kituo hiki kinatoa huduma ya upangishaji wa nafasi *(Co-location/Virtual Server),* uhifadhi *(storage)* na uwekaji wa tovuti mtandaoni *(Web Hosting)*. Kituo kina mafanikio yafuatayo: -

(i) Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 kituo kimeunganisha jumla ya wateja 211 ambao wanatumia huduma mbalimbali. Kati ya hao, wateja wa taasisi za Serikali ni 123 na taasisi binafsi ni 88;

(ii) Jumla ya mapato kwa kipindi cha Julai 2023 - Juni ,2024 yalikuwa ni kiasi cha **Sh. Bilioni 5.045.** Vile vile katika Mwaka wa Fedha 2024 /2025 matarajio yalikuwa ni kukusanya kiasi cha **Sh. Bilioni 7.253.** lakini hadi Disemba, 2024 kiasi kilichokusanywa ni **Sh. 3.174.** sawa na **asilimia 43.7** ya lengo;

(iii) Kituo kinatarajia kuwa ifikapo tarehe 31 Juni, 2025 kitakuwa kimeunganisha wateja wapya 60 kati ya hao 30 watatoka taasisi na idara za Serikali na 30 kutoka kampuni binafsi;

(iv) Mkakati wa taifa wa uchumi wa kidigitali wa miaka (10) kuanzia 2024 - 2035 ulizinduliwa tarehe 29 Julai 2024 na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (Rais) wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** mradi unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Ukomo wa matumizi kwa baadhi ya vifaa vya miundombinu ya uendeshaji (life span);

(ii) Idadi ndogo ya vifaa vya kuhifadhia data (racks) ili kuendelea na utoaji wa huduma ya upangaji wa nafasi (colocation); na

(iii) Gharama kubwa za uendeshaji wa kituo cha kutunza data hasa matumizi makubwa ya umeme unaotumika kupooza vifaa na mitambo kutokana na jiografia yenye mazingira ya joto.

**2.6 Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi iliyotembelewa na Kamati**

**(a) Mtiririko wa Utoaji Fedha kwenye Baadhi ya Miradi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, kuna changamoto ya utoaji wa fedha kwenye baadhi ya miradi kama vile mradi wa ujenzi wa jengo la Kituo Kikuu cha Ubunifu cha umoja wa kimataifa wa mawasiliano fedha zimepokelewa kwa **asilimia 18.7,** Anwani za Makazi na Postikodi kwa **asilimia 10,** Kuimarisha Uwezo wa Taasisi kwa **asilimia 33.6,** na Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA kwa **asilimia 47.3.**

**(b) Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025, UCSAF ilikuwa imekusanya kiasi cha **Sh. Bilioni 40.051** ambayo ni sawa na **asilimia 92** ya lengo. Makusanyo hayo ni kutoka vyanzo vya mapato, ambavyo ni ruzuku toka Serikalini, tozo za huduma, ruzuku toka TCRA na wadau wa maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, mfuko unaendelea na ujenzi wa minara 758 katika Kata 713 nchini. Hadi Februari, 2025 minara 443 imejengwa sawa na **asilimia 58.4.** Kati ya minara iliyojengwa, 417 sawa na **asilimia 55** inatoa huduma za mawasiliano. Aidha, minara iliyobaki ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji.

**Mheshimiwa Spika,** wateja wa faiba (FTTH) 10,358 wameunganishwa sawa na **asilimia 8** ya lengo la nusu mwaka na **asilimia 4** ya lengo la mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya mradi huu na inaendelea kutoa ushauri kuwa fedha ziendelee kutolewa kwa wakati ili kukamilisha miradi.

**(c) Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC)**

**Mheshimiwa Spika,** moja kati ya jambo ambalo kamati ililifanyia tathimini ni ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka Tanzania hadi DRC. Kamati ilipokea taarifa kuwa, shirika limekamilisha uchambuzi wa zabuni na majadiliano ya mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kuanzia Kigoma Tanzania hadi Kalemie, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Mkataba wa mradi husika umepelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya upekuzi na unatarajiwa kusainiwa Machi, 2025. Vile vile imepokea taarifa kuwa, utelekezaji wa mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo Aprili, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyofikiwa shirika linakabiliwa na changamoto ya uhaba na ubovu wa miundombinu ikiwemo barabara hususani maeneo ya vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ujenzi ili Mkongo ujengwe kwa manufaa ya kukuza uchumi wa nchi na kuongeza pato la Taifa.

**2.7 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu 68) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2), Kamati ilifanya uchambuzi wake kwa kulinganisha makadirio ya matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwaka wa Fedha 2025/2026. Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(a) Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(b) Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(c) Makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**2.8 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeainisha vipaumbele mbalimbali kama ifuatavyo: -

(a) Kutunga, kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa miongozo inayosimamia Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;

(b) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na Posta kote nchini;

(c) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha biashara Mtandao nchini;

(d) Kuimarisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa Uchumi wa kidigitali;

(e) Kuimarisha ulinzi na usalama wa anga ya mtandao; na

(f) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuchochea ubunifu na kuimarisha ustawi wa kampuni changa *(startups)*.

## 2.9 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake inakadiria kukusanya **Sh. Bilioni 885.762** kiwango hiki ni ongezeko la **Sh. Bilioni 93.995** sawa na **asilimia 11.87** ukilinganisha na **Sh. Bilioni 791.767** iliyopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. **Kielelezo Na. 3** kinaonyesha mchanganuo wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli hayo.

**KIELELEZO NA 3: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| NA | TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2024/2025 (TZS) | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2025/2026 (TZS) | MAKUSANYO KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA MAKUSANYO | OFAUTI YA ASILIMIA (+/-) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | WIZARA | 100,700,000,000.00 | 100,369,242,950.00 | 49,626,389,613.00 | 49.3% | -0.33% |
| 2 | TCRA | 201,736,566,472.99 | 245,989,519,796.00 | 158,433,060,089.39 | 79% | +22% |
| 3 | TCRA – | 710,000,000.00 | 710,000,000.00 | 532,500,000.00 | 75% | 0% |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | CCC | | | | | |
| 4 | TTCL | 377,912,000,000.00 | 408,736,163,000.00 | 133,469,800,664.00 | 35% | +8% |
| 5 | TPC | 38,865,885,000.00 | 37,997,501,000 | 16,976,906,830.00 | 44% | -12% |
| 6 | UCSAF | 43,614,542,504.00 | 64,196,337,542.00 | 40,051,875,143.59 | 92% | +47% |
| 7 | ICTC | 6,428,707,300.00 | 6,718,050,253.92 | 2,486,439,962.00 | 39% | +4.5% |
| 8 | PDPC | 21,800,000,000.00 | 21,046,025,040.00 | 2,353,559,226.17 | 10.8% | -3.46% |
| | **JUMLA** | **791,767,701,276.99** | **885,762,839,581,92** | **403,930,531,528.15** | **51%** | **11.87%** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kipekee, Kamati inazipongeza taasisi zilizopo chini ya Wizara, ambazo zimeongeza wigo wa makadirio ya makusanyo. Hatua hii itaongeza pato la Serikali na kuchochea uchumi.

**2.10 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, **Fungu 68** – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. Bilioni 291.533** ambapo kati ya fedha hizo, **Sh. Bilioni 14.485** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. Bilioni 277. 047** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**KIELELEZO NA 4: Ulinganisho wa Bajeti ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025- 2025/2026**

| MAELEZO | BAJETI YA MWAKA 2024/2025 | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 38,906,663,000 | 14,485,656,000 | -24,421,007,000 | -37% |
| MIRADI YA MAENDELEO | 142,019,894,000 | 277,047,483,000 | 135,027,589,000 | +195% |
| **JUMLA KUU** | **180,926,557,000** | **291,533,139,000** | **110,606,582,000** | **161.6%** |

**Mheshimiwa Spika,** bajeti ya Wizara imeongezeka kwa **Sh. Bilioni 110.606** sawa na **asilimia 161** kutoka **Sh. Bilioni 180.926** iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 hadi kufikia **Sh. Bilioni 291.533** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Fedha iliyotengwa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo imeongezeka kwa **Sh. Bilioni 135.027** sawa na **asilimia** 195 (kama ambavyo imeainishwa katika **Kielelezo Na. 4).**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za maendeleo na inatoa rai kwamba fedha zitolewe kwa wakati ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa vipaumbele vya Serikali kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 bajeti imepungua kwa **Sh. Bilioni 24.421** sawa na **asilimia - 37.** ukilinganisha na bajeti hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ambapo ilikuwa ni **Sh. Bilioni 38.906** ya sababu za punguzo hilo ni kutokana na mabadiliko yaliyofanyika ya Idara ya Habari na Maelezo kuhamishiwa Wizara ya Elimu na Mafunzo.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. Bilioni 277.047** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni nyongeza kwa **asilimia 195.** ukilinganisha na bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kati ya fedha hizo, **Sh. Bilioni 98.480** ni fedha za ndani, na **Sh. Bilioni 178.566** ni fedha za nje

**SEHEMU YA TATU**

**3.0 MAONI NA USHAURI**

**3.1 Maoni na Ushauri wa Jumla**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa ufanisi mkubwa imeendelea kutoa Fedha za kutekeleza majukumu mbalimbali ya **Fungu 68 -** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inaishauri Serikali: -

(a) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika kuimarisha huduma za mawasiliano na kuhakikisha kuwa yanapatikana kwa urahisi kwa manufaa ya wananchi;

(b) Kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya utendaji kazi utakaochochea kuboresha huduma za Sekta ya Mawasiliano na matumizi ya TEHAMA nchini, kwa

kuwa sekta hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi;

(c) Kuunganisha taasisi za Serikali na miundombinu ya mtandao wa kasi *(broadband infrastructure)*

(d) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu *(sustainability)* na kuwepo kwa thamani ya Fedha *(value for money);* na

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza usimamizi madhubuti kwa taasisi ili ziweze kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na hatimaye kuboresha huduma za Mawasiliano na TEHAMA katika kuongeza mapato ya Serikali.

**3.2 Maoni na Ushauri Mahususi**

**(a) Ulaghai katika Mitandao ya Mawasiliano**

**Mheshimiwa Spika, Katika** "Ilani ya uchaguzi mkuu wa Mwaka 2020" Serikali, imeeleza nia ya kuimarisha mfumo wa TEHAMA wa udhibiti usalama na mapato katika Mawasiliano. Hata hivyo tatizo la uhalifu na utapeli kwenye mitandao ya mawasiliano bado linaendelea kwa kasi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa, pamoja na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na mamlaka husika, jitihada zaidi zinahitajika ili kutoa ufumbuzi wa kudumu sambamba na kuzuia jumbe fupi zinazotumwa bila idhini au matakwa ya mteja. Aidha, Wizara husika ishirikiane na makampuni ya mitandao ya simu pamoja na Wizara ya mambo ya ndani ili kumaliza tatizo hilo.

**(b) Fedha kutotolewa kwa wakati kwenye baadhi ya miradi iliyoko chini ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na malengo mema ya kuanzishwa kwa mradi wa ujenzi wa vituo vya kuendeleza ubunifu na utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA. Kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa Fedha kwenye miradi hii, hali hii inazoofisha jitihada za kukuza uchumi na kutatua tatizo la ajira kwa vijana nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha za miradi hiyo zinatolewa kwa wakati ili kufikia malengo kwa wakati.

**(d) Kutokuwepo kwa Sera na Sheria inayohusu bunifu za TEHAMA**

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto inayoikabili vituo vya bunifu za TEHAMA nchini ni kutokuwa na sera na Sheria katika suala la uendeshaji na usimamizi wa vituo hivyo, jambo linalopunguza kasi ya utekelezaji wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuleta bungeni Mswada utakaowezesha utungwaji wa Sheria husika ili kuweka mazingira wezeshi yenye kutoa ajira na kutambua bunifu za wananchi ipasavyo. Aidha, ujenzi wa vituo hivyo uende sambamba na kuongeza idadi ya Wataalam na Wakufunzi wa kuendesha vituo hivyo ili iweze kuleta tija iliyokusudiwa.

**(e) Gharama Kubwa za Uendeshaji wa Kituo cha Kutunza Data.**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na changamoto katika uendeshaji wa mradi wa vituo vya kutunzia data nchini, kunakosababishwa na matumizi makubwa ya umeme, ukomo wa matumizi wa baadhi ya vifaa vya miundombinu ya uendeshaji wa kituo cha kutunzia data *(life span)* na idadi ndogo ya vifaa vya kuhifadhia data *(racks)* ili kuendelea na utoaji wa huduma ya upangaji wa nafasi *(colocation)*. Hali hii inasababisha uwepo wa gharama kubwa katika uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti wa kutosha ili kubaini eneo lenye mazingira rafiki yenye hali ya baridi ili kujenga kituo kipya, hii itasaidia kupunguza gharama za umeme unaotumika kuendesha mitambo.

**(f) Kutumia Fursa ya kuwa na maabara ya vifaa vya mawasiliano ya kieletroniki**

**Mheshimiwa Spika,** imebainika kuwa, Tanzania ndiyo nchi pekee inayomiliki mtambo wa upimaji wa bidhaa za kielektroniki katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki, fursa hii ikitumiwa vizuri inaweza ikaingiza kiasi cha fedha kutoka kwa majirani zetu ambao hawana aina hii ya maabara, hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kutumia fursa hii ipasavyo ili kuongeza pato la nchi,

**Mheshimiwa Spika,** Serikali iziunganishe mamlaka za udhibiti ubora wa bidhaa nchini kwa kutumia mfumo wa pamoja (one single system) ili kuleta uthibiti wa bidhaa za kielektoniki nchini, pia ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kwa watumiaji wa vifaa hivyo na kubaini kama kuna ukiukwaji wowote ili kuondoa athari zinazoweza kutokea katika jamii.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, namshukuru Naibu Spika, kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha kwa ufanisi vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea

kuisimamia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako tukufu. Kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue wajumbe hao ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ifuatavyo:

1. Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. - Mwenyekiti
2. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. - Makamu
3. Mhe. Kapt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb. - Mjumbe
4. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. - Mjumbe
5. Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. - Mjumbe
6. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. - Mjumbe
7. Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb. - Mjumbe
8. Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. - Mjumbe
9. Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb. - Mjumbe
10. Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. - Mjumbe
11. Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb. - Mjumbe
12. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. - Mjumbe
13. Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. - Mjumbe
14. Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako Mb. - Mjumbe
15. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb. - Mjumbe
16. Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. - Mjumbe
17. Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. - Mjumbe
18. Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. - Mjumbe
19. Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Mwatumu Dau Haji, Mb. - Mjumbe
21. Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb. - Mjumbe
22. Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry W. Silaa, (Mb) kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wake, Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb).

Aidha, niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bw. Mohammed Khamis Abdullah, Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano na TEHAMA na inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidii.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bw. Baraka I. Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi **ya Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI**
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu
16 Mei, 2025

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, ahsante sana kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa taarifa hiyo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka 2025/2026.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na shughuli yetu, tuna wageni wengine naomba niwatangaze kama walivyo.

Wageni wa Mheshimiwa Spika, wageni 57 wa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kutoka *Bilal Muslim Mission* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Spika kutoka *Bilal Muslim Mission* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Jerry William Silaa ambaye ni Waziri wetu wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, hao ni Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi na Maafisa kutoka Wizara na taasisi zake. Naona hawajaingia bado, lakini pia tuna mgeni mwingine wa Mheshimiwa Jerry silaa ambaye ni Mr. Victor Zakayo kutoka Kampuni ya Minara, karibu sana. *(Makofi)*

Tumeambiwa pia tuna wadau kutoka taasisi ya fedha *NMB, CRDB na NBC* kama wameingia wapo wameshaingia karibuni sana wadau hawa wetu wa Benki za *NMB, CRDB* na *NBC*. *(Makofi)*

Wapo kuna viongozi na wataalamu kutoka sekta binafsi, karibuni sana viongozi na wadau kutoka sekta binafsi. *(Makofi)*

Pia kuna viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Ilala, karibuni sana viongozi wetu wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 41 wa Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest ambao ni wanfunzi 31 na walimu 10 wa Shule ya Awali Msingi Firdaus kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Shule ya Firdaus. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan Ndugu Said Ally Said baba yake mdogo kutoka Zanzibar, karibu sana baba yetu kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava Ndugu Elizabeth Riziki mwanzilishi wa Taasisi ya *Africa Tintanks* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana taasisi yetu ya *TinTanks* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya rafiki zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, wanafunzi wa Shahada ya Udaktari kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Matibabu ya Kikristo, Kilimanjaro *(KCMC),* karibuni sana wageni wetu wote ambao mpo muda huu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza sasa na uchangiaji wa Wizara hii. Tunaanza na Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu ajiandae.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kabisa kwa dhati ya moyo wangu kwa kunifanya kuwa mchangiaji wa kwanza katika hotuba ya Wizara hii muhimu kwa nchi yetu, lakini nikushukuru wewe na Kiti chako kwa niaba ya Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti kwa namna ambavyo mmetupa fursa Waheshimiwa Wabunge kutoa mivhango kwa maslahi ya nchi yetu tunapoenda kumaliza bajeti ambayo itatufanya Wabunge twende kwenye *election* na turudi tukiwa na nguvu tele ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mimi nitajikita kwenye mambo makubwa mawili na kwa kweli mchango wangu utakuwa katika mambo ya kitaifa, nina imani mambo ya jimboni, mambo ya minara na sisi pia tunahitaji *fiber* nina imani kabisa Waziri na timu yake wamejipanga watayafikisha, lakini leo mchango wangu utakuwa kutoa ushauri katika masuala mazima ya kitaifa kwa lengo la kuisaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi yatakayoleta tija katika kuleta *investment* katika Taifa letu katika masuala mazima ya sekta ambayo Mheshimiwa Jerry anaiongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu lilitunga Sera ya Mawasiliano mwaka 1997 na Sera ya Mawasiliano ya mwaka 1997 ilijikita katika kuhakikisha Taifa letu linavutia uwekezaji mkubwa katika sekta ya *telecommunication* na mambo yanayohusiana na mawasiliano katika Taifa letu. Naomba nilipe Bunge lako Tukufu

taarifa kuwa mwaka 2010 Serikali yetu walileta Bungeni *Electronic and Postal Communications Act,* ikatungwa ambayo iliweka vipengele ambavyo hivyo vitakuwa mwongozo wa hoja ninayotaka kuijenga siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ambayo sasa inaongozwa na Mheshimiwa Rais mwanamama shupavu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan inapaswa kupongezwa kwa kiwango kikubwa Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takribani katika kipindi cha miongo 20, tumeona leo tumepewa *statistics* Taifa letu limeweza kuwa na *line* zilizosajiliwa zinazowafanya watu waweze kuwasiliana kwa kufika line milioni 97, hongera Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, hongera Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *Electronic and Postal Communications Act* iliyotungwa mwaka 2010 na kuja kusisitizwa kwa *Finance Act* ya mwaka 2016 na kufanyiwa marekebisho *revision* ya Sheria ya *Electronic and Postal Communications Act* ya mwaka 2022 *section* 26(1) na (4) ninaomba Mheshimiwa Waziri ukae kwa kutulia na Mheshimiwa Naibu wako mnisikilize ushauri ninaokwenda kuwapa kwa maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii tulipoitunga mwaka 2010 na tukafanya mabadiliko yake mwaka 2022 katika masuala ya kampuni za mawasiliano, tulitunga *article* ambayo iliyalazimisha makampuni yote ya simu Tanzania kuji-*list* katika *stock of exchange* kwa kuyataka kuachilia 25% ya *stake* zinunuliwe na Watanzania na lengo la sheria lilikuwa jema kabisa kuwafanya Watanzania waweze kumiliki uchumi wa Taifa lao ili tunaposema tunakuza uchumi raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wawe sehemu ya kumiliki uchumi wa Taifa letu kwa lengo ya kuwafanya sehemu ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa bahati mbaya sana niseme initial wakati sheria hii inatungwa tulipokuja kuifanyia

*revision* mwaka 2022 tukatoa kipindi cha miezi sita kuhakikisha makampuni yote ya *telecommunication, M&O* zote za nchi yetu zinakwenda kuji-*list* ndani ya miezi sita katika *DSE* ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo hisa ambazo zilifanyiwa *evaluation* na *owner* wa kampuni, kampuni ya kwanza ilikuwa ni *Vodacom Tanzania*. Walipokwenda kuji-*list* kwenye *stock of exchange* hisa ziliuzwa kwa shilingi 850 kwa hisa moja, Watanzania wanaofanya biashara, viongozi wa Serikali, sisi Wabunge na wananchi wa kawaida wakavutiwa kwenda kununua hisa, wakawekeza katika *stock* ya 25% na kwa bahati mbaya sana sheria ile ilitaka 25% ya watakaonunua hisa wawe Watanzania tukawa tumewa-*exclude foreign investors* katika kununua zile hisa 25%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jerry, kaka yangu, naomba unisikilize sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyozungumza hapa, baada ya Watanzania kutoa mitaji yao wakanunua hisa kwenye kampuni ambayo ilikuwa ya kwanza ku-*list* kwenye *stock of exchange,* kwa bahati mbaya sana nataka nikwambie *as today* tunavyozungumza kwa kipindi cha miaka nane watu wamechukua fedha zao na mitaji wamewekeza kwenye *Vodacom,* kwa miaka nane leo tunazungumza, ukiangalia *dividend* ya fedha za Watanzania walizowekeza kwenye sekta hii ya mawasiliano katika kununua hisa kwenyeKampuni ya *Vodacom*, nataka nikuambie, leo tunavyozungumza kwa miaka nane mtu mmoja kwa hisa moja amelipwa shilingi 245, amelipwa shilingi 245 sawa na wastani wa shilingi 35 kwa mwaka kwa hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kujenga hoja, kama mtu huyo amenunua hisa za shilingi milioni 100 angechukua fedha hizi akaamua kuziweka hata katika *treasury bond* au kwenye *fixed bond* bei…

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi? Mheshimiwa Kanyasu.

**TAARIFA**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa mchangiaji, anachangia jambo muhimu sana. Mimi ni sehemu ya watu walionunua hisa lakini hatujawahi kuona hilo gawio, lakini hata ukitaka kuziuza hakuna mtu wa kumuuzia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Elibariki Kingu, unaipokea hiyo Taarifa ya Mheshimiwa Kanyasu?

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa hii ya *DC* mstaafu mwenzangu na Naibu Waziri mstaafu. Lengo langu ninakwenda kujenga hoja na hayo nitafika huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuambie katika kipindi cha miaka nane Watanzania kwa kuwekeza pesa katika *DSE* kwa kununua hisa za *Vodacom,* wastani wa shilingi 35 kwa mwaka fedha ambazo hata mtu angezichukua akaamua kumkopesha Mzee Lukuvi bado angeweza kulipwa fedha ambazo zingeweza kuwasaidia Watanzania maskini hawa waliowekeza katika mtaji huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni nini? Kama Taifa, Mheshimiwa Waziri ninakusihi, mnapopewa nafasi na madaraka kuwashauri wakubwa na Serikali, washaurini viongozi wetu kwa maslahi ya Taifa ambayo yataweza kuvutia *investment*, siyo ku-*deter investment* katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninapozungumza hisa hizi ambazo wananchi *initially* walizinunua katika *DSE* kwa shilingi 850 leo nakwambia hisa hizi zime-*drop* kutoka shilingi 850 mpaka shilingi 720 na hata ukizitangaza hakuna mtu wa kuzinunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja hii, je, ni mitaji ya watanzania wanyonge wangapi waliyochanga fedha zao wakazipeleka *DSE* kununua hisa za *Vodacom*...

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wake umemalizika anamalizia sentensi ya mwisho.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wake umemalizika malizia sentensi ya mwisho Mheshimiwa Elibariki.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hoja hiyo, ninakuomba Waziri utakapokuja kuhitimisha utusaidie kutupa majibu, nini msimamo wa Serikali, kama hamtakuja na majibu ya kutosha tutakwenda kushika shilingi. Utuambie mnakwenda kufanya nini ku-*revise* hii sheria, muache soko liamue watu kwenda kuji-*list* kwenye *DSE* na watu wakifanya hivyo tutakuwa tumeokoa mitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nakuomba radhi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri, ninyi nataka niwashauri. Mwaka jana mwezi wa nane Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwenu muweze kuhakikisha kwamba *TTCL* inajiendesha kibiashara. Nakuomba dakika moja tu.

Mheshimiwa Waziri nataka niwasaidie, tumemuona Kadogosa ana *SGR,* Serikali kupitia kodi za Watanzania tumejenga *SGR* ya *telecommunication* ambapo *fiber* tumeizungusha nchi nzima. Mheshimiwa Jerry, kwa nini *fiber* hii hamuitumii kibiashara, kwa nini tuendelee kutoa fedha za Watanzania kuipa *TTCL* wakati kodi za Watanzania zimetumika kujenga *fiber?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupa *analysis* ndogo ya Uganda pekee yake ningekuwa nina muda ningekupa *analysis* ya Mataifa 12, kwa upande wa Uganda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Elibariki Kingu umeeleweka vizuri sana. Umeeleweka vizuri sana, nakushukuru. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na niipongeze Serikali kwa jinsi ambavyo inaendelea kuimarisha mawasiliano hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita kwenye mambo machache ambapo ni mambo kama mawili au matatu. Jambo la kwanza; kwanza tuwapongeze kwa ujenzi wa minara kwenye maeneo mbalimbali nchini kuhakikisha kwamba Serikali na nchi yetu ina kuwa na mawasiliano vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuomba kwamba kuna maeneo ambayo bado yana mikwamo ya minara hususan Makete kuna minara ambayo haijajengwa mpaka sasa hivi Kijiji cha Usalimwani, kumekuwa na changamoto kati ya watu wa *UCSAF* pamoja na watu wa hifadhi ambapo mnara unatakiwa ujengwe. Tunaomba watu wa Wizara hii muingilie kati ili muweze kusaidia ujenzi wa mnara ule ili wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia aliyozungumza Mheshimiwa Kingu kwamba *fiber* ipo na tunatamani itumike kibiashara kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma hii, lakini pesa inazokusanya kwenye shirika hili hatuwezi kukubaliana na kile ambacho Mheshimiwa Rais kila mwaka akisimama wakati wa kugawa magawio anakuwa anaizungumzia *TTCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati Mheshimiwa Nape ni Waziri, Rais alisema kwamba kwa nini mnahangaika na mambo ya *line* za simu wakati mna *fiber* ambayo pekee inaweza ikaendesha shirika la *TTCL. Fiber* peke yake tu inatosha kuwapa ninyi utajiri na kuhakikisha kwamba Shirika linasimama na kuwa imara. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwamba ukaliangalia Shirika la *TTCL* kwa jicho la karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye suala la *cashless economy*. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Gavana wa *BOT,* lakini na watu wa *BOT* kwa sababu wao wameshaanza kuonesha mwenendo kwamba kuna umuhimu kwenye Taifa letu kutoka kwenye mifumo ya *cash* kwenda kwenye *cashless economy* na tayari *BOT* imeshatoa tangazo lao wakiziomba benki, lakini pia wakitoa maelekezo kwamba kutakuwepo na kupungua kwa kodi au kuweka *incentives* kuhakikisha kwamba watu wengi wanahamia kwenye matumizi ya *cashless economy,* na nitumie nafasi hii ninyi kama Wizara ya Mawasiliano mna ufunguo mkubwa kuhakikisha Taifa linahama kutoka kwenye matumizi ya *cash* na kwenda kwenye *cashless economy.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ndiye utakayeweza kumsaidia Waziri wa Fedha ili kuongoza *tax base,* wewe ndiye utakayemsaidia Waziri wa Fedha kuhakikisha kwamba walipa kodi wanakuwa wawazi na wanakuwa wengi kwa kuhakikisha kwamba Watanzania wengi wanahamia kwenye *cashless economy*. Wanahamiaje? Kwa kuongea na mitandao ya simu, kuwasiliana na Wizara ya Fedha na *TRA* kuhakikisha kwamba kama kuna makato na nini ziweze kupunguzwa kama ni *incentives* kuhakikisha kwamba Watanzania wengi wanahamia kwenye sekta ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Taifa la Rwanda, wenzetu kutoa pesa mfukoni na kulipa ni kitu ambacho hakiwezekani, kila kitu ni kwenye simu, hii inasaidia kupunguza mambo ya rushwa, lakini pia inapunguza mambo ya *money laundering*, ni vitu ambavyo vinakwepeka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninatamani uwe *champion* kwenye nchi hii kuhakikisha Taifa linahamia kwenye *cashless economy*. Watu waone kutumia pesa kwenye mfumo ni rahisi zaidi kuliko kutembea na maburungutu ya fedha mfukoni kwa sababu ni hatari kwa usalama wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la usalama wa mawasiliano; bado kumekuwa na kesi nyingi za watu kutapeliwa, bado kumekuwa na kesi nyingi za mambo ya *AI* kwa maana ya *artificial itelligence*. Wewe ndiye unayesimamia eneo hili, tunatamani, tunaelekea kwenye uchaguzi uhamasishe matumizi sahihi ya teknolojia kwa maana ya akili mnemba ili Watanzania wengi wawe na *awareness,* wekeni elimu kwenye vipindi vya *television* na redio ili kuhakikisha watu wengi wanakuwa na elimu kuhusu athari na madhara ya matumizi ya akili mnemba kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtu akiamua kwamba aweke sura ya Mheshimiwa Jerry Silaa sehemu ambayo Mheshimiwa Bashungwa yupo anafanya hivyo na anatokea. Kitu ambacho siyo sahihi kwenye Taifa letu na kinaweza kutuletea madhara makubwa kwa sababu watu wamekuwa wepesi kuamini vitu ambavyo muda mwingine havipo, lakini wanaamini kwa sababu hawana elimu kwamba *artificial intelligence* inaweza ikamfanya nini mtu katika mazingira gani na ikaonekana mtu amefanya hilo tendo kumbe siyo yeye na hususan kipindi hiki cha uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni hili ambalo Mheshimiwa Kingu amezungumza. Mheshimiwa Waziri kwa kweli ni lazima utoe tamko leo kwa sababu hata mimi nina wahanga, Wana-Makete ambao walinunua hisa *Vodacom* baada ya Serikali kutangaza kwamba *Vodacom* iwe *listed* kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange* wakajiingiza huko, walivyoingiza hiza zao hadi leo mitaji hiyo imelala, yaani mtu ameenda kununua hisa za shilingi milioni 200, shilingi milioni 100, milioni 300 badala ya mtaji kukua, mtaji sasa umekufa na bahati mbaya hata hizo hisa alizonazo hazihusiki popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wewe ndiye una dhamana ya kutuambia leo kwamba hao Watanzania hatima yao ni nini, kama tunaenda ku-*review* sheria, tu-*review* sheria ili tuweze kunusuru, lakini leo wewe mwenyewe kama Waziri ukitaka kujiuliza, je, yale mashirika yote ya mawasiliano ambayo mlikuwa mmeomba yawe *listed* kwenye *stock exchange,* yote yaliji-*list,* kama mmoja ameji-*list* na ameingia mhanga na hisa hazikui maana yake ni kwamba kuna changamoto kwa Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ilikuwa njema kwamba Watanzania wengi waweze ku-*own* uchumi, waweze ku-*own* kuingia kwenye mifumo hii ya mawasiliano kwa sababu biashara ya hisa ni biashara kubwa duniani lakini hiki kilichoweza kutokea kwa watu ambao walinunua hisa za *Vodacom* imekuwa msiba badala ya kuwa mtaji. Kwa hiyo, muda mwingi sisi Wabunge tunapigiwa simu kwamba bwana tusaidie tufanye hiki, leo tunatamani kwamba Serikali itoe kauli, mitaji iliyolala, mitaji iliyo-*freeze,* mitaji ambayo imegota kwenye *Vodacom* kwenye soko la hisa mnaenda kufanya nini ili kunusuru Watanzania hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mfahamu kwamba hii ni sekta binafsi, sekta binafsi ni lazima ilelewe na kama hatuwezi kulea sekta binafsi Watanzania watakuwa waoga kwenda kwenye hilo eneo kuwekeza kwa sababu hao wengine wameshapata maumivu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, na Jerry Silaa ni kijana *smart,* tunaamini kabisa kwamba huwezi kuruhusu fedha hizi za Watanzania ambazo kwa takribani miaka saba, miaka nane zimelala hazikui ziko pale, zitaenda kunusuriwa kwenye maisha ya watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wengi wamepata shida kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nikuombe suala la hisa za Watanzania ambazo ziko kwenye shirika la *Vodacom,* leo Serikali itoe kauli na msipotoa kauli kwa kweli tutakuwa tayari kushika shilingi kuhakikisha kwamba tunanusuru. Nia ilikuwa njema, lakini wema wa nia hii umeenda kuleta

matatizo kwa hiyo ni lazima tutokea katika huo mtego ambao kwa kweli umeshikilia fedha nyingi za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niendelee kumtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri anavyoendelea kuandaa majibu kuhakikisha kwamba anatupa majibu kwenye huu uwekezaji kwenye Shirika la *Vodacom,* nini kitaenda kutokea leo kwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Richard Sanga, nilimtaja Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambayo kimsingi ni Wizara muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani na pongezi nyingi tumezitoa, lakini tuna mpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo alikuwa na maono makubwa katika Wizara hii na ndiyo maana aliipunguzia mzigo akaitoa Wizara ya Habari akaiweka sehemu nyingine akaiacha Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa sababu ni kitu ambacho Waziri ata-*focus* kuhakikisha kwamba anaisaidia nchi katika sekta hii muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii inachochoea shughuli zingine za uchumi katika nchi yetu. Kwa mfano watu wa fedha kwenye mambo ya *transaction* wanategemea sana Wizara hii, kama nilivyosema mawasiliano ya simu yanategemea sana Wizara hii, lakini kama haitoshi tumeona hata ajira nyingi zikisimamiwa vizuri zitatokana na Wizara hii ambayo inawagusa zaidi vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia maeneo machache sana, kwanza nitachangia Mradi wa Tanzania Kidigitali. Mradi huu tulivyojulishwa kwenye Kamati pamoja na taarifa iliyosomwa hapa ni kwamba tuliambiwa umefikia 78% kwa maana ya utekelezaji wake na fedha zimetoka hazina matatizo yoyote, mradi unakwenda vizuri na tunaendelea kusema tu kwamba mradi huu uendelee kusimamiwa na Wizara na tuendelee kuhakikisha kwamba lengo la kuunganisha taasisi zote zisomane ndiyo lilikuwa lengo la Mheshimiwa Rais kwamba kupitia mfumo huu au mradi huu itasaidia taasisi zetu kusomana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia zaidi ya taasisi 100 kwa maana ya Bara pamoja na Visiwani, wote kwa maana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tayari taasisi 100 zimeshafikiwa na mradi huu na zimeanza kusomana. Hii ni kazi kubwa sana, nikupongeze Waziri, Mheshimiwa Jerry Silaa kwa kusimamia kazi hii nzuri ambayo inaenda kutupa heshima kama nchi na haya yalikuwa maagizo ya Mheshimiwa Rais mwenyewe kuhakikisha kwamba mifumo inasomana na huu ndiyo mwelekeo wa kwenda kwenye *e-card* kwamba sasa tuachane na mtu kuwa na kadi nyingi mpaka zinavimbisha suruali kumbe ni kadi huna fedha, una kadi nyingi mara *NHIF*, sijui una leseni, mara sijui una kitambulisho cha mpiga kura, mara wale wapenzi wa mpira una kadi ya kwenda kuchanja kwenye mpira, yaani unakuwa na lidude kubwa kumbe hata fedha hamna, umejaza kadi nyingi ambazo kimsingi ikipatikana *e-card* itasaidia sana kuondokana na changamoto ambayo tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nikuombe sana, endelea na kazi hii kuhakikisha kwamba mradi huu mkubwa wa Serikali wa Tanzania Kidigitali unaenda kukamilika na kuhakikisha kwamba Tanzania inaendelea kuwa mfano wa nchi zingine katika Afrika pamoja na dunia, lakini itasaidia sana kupunguza watu kulipa kwa *cash,* itakuwa *cashless,* sasa watu watakuwa hawatumii fedha *cash* katika kununua maeneo mbalimbali, lakini zaidi ya hapo itasaidia ukusanyaji wa kodi, kwa sababu kila *transaction* itapita kwenye mfumo wa ki-*electronic* itasaidia kujua nani amepata mapato gani na mwisho wa siku ni rahisi hata *TRA*

na watu wanaohusika na kodi kuweza kukusanya kirahisi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sekta hii au Wizara hii ni muhimu sana. Mheshimiwa Waziri, nikuombe nenda ukasimamie na tuhakikishe kwamba tunafikia malengo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni eneo hili la vituo vya umahiri vya kuwajengea vijana wetu uwezo ambavyo tumesikia hapa kwamba vijana wetu kwa maana ya hizi kampuni ndogo ndogo za *startups* ambazo tunaamini zikijengewa uwezo zitawafanya vijana wengi waingie kwenye ajira na nikupongeze sana mwaka huu tulipokuwa pale Arusha mliweza kutoa hata tuzo kwa vijana wabunifu wa Tanzania ambao kwa kweli wengine walikuwa hawaamini mpaka walilia wakati wanapewa na kutambuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lile endelea nalo kwenye mikoa yote, isiwe eneo moja Dar es Salaam na Arusha, nenda mikoa yote Tanzania, vijana wabunifu wapo, tuwajengee uwezo na tuweze kuwatia moyo na nimefurahi sana kuna baadhi ya maeneo mliwapa hadi mtaji, yaani kwamba kijana ameanzisha bunifu yake, hana uwezo wa fedha mnampa fedha ili aweze kukuza bunifu yake na mwisho wa siku anaenda kuajiri vijana wengine. Pia hii itapunguza vijana kubaki kwenye mambo ya *betting* na mambo kama hayo kwa sababu watakuwa na kazi kamili ya kufanya na vijana wetu wengi wana uwezo mkubwa kwenye sekta hii ya *ICT. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana uendelee kuwalea kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata fursa hii ambayo kimsingi Rais amesema Wizara yako ikisimamiwa vizuri itasaidia sana kuleta ajira nyingi kama ambavyo tumesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema vile vituo viongezewe kasi viweze kukamilika ili vijana wetu waweze kupelekwa kule kwa ajili ya *training,* lakini siyo vijana tu hata watu wazima ambao wana shughuli zao zingine wanaweza kwenda kujifunza pale na kuweza kupata uwezo mzuri zaidi wa kutumia *ICT. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni suala la kupongeza, minara 758 kazi inaenda vizuri, tumepata taarifa kwenye Kamati na mimi binafsi katika Jimbo la Singida Mashariki nimepata minara miwili imeshakamilika kule Misughaa pamoja na pale Lighwa, wananchi sasa hivi wana-*beep* hata wakiwa chumbani ndani, wanaweza kuwasiliana kokote walipo, zamani ilikuwa mpaka mtu aende juu ya mti, anaenda anatafuta mawasiliano, hii ilikuwa ni hatari sana wengine wanagonjwa na nyoka katika maeneo yale, lakini leo wanapata mawasiliano ya moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupongeze sana, nani kushukuru kwa kumleta Mheshimiwa Naibu Waziri pale kwenye jimbo langu, pale Matare ule mnara umefikia karibu 80% unaenda kukamilika, watu wangu wa Jimbo la Singida Mashariki ambayo ni Ikungi Mashariki wanaenda kupata mawasiliano yale ambayo yalikuwa hayapatikani kwa sababu hata kuna vijana walikuwa wanachelewa kuoa kwa sababu hawawezi hata kuwapigia simu wapenzi wao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaamini kupitia hili litasaidia sana na Mheshimiwa Naibu Waziri rudi mlete Waziri muje mzindue ile minara kuonesha kwamba kazi kubwa ya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanyika vizuri katika Jimbo la Ikungi Mashariki katika sekta ya mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kule Mang’onyi ule mnara ambao ulikuwa unaendelea msukumeni mkandarsi aweze kumaliza na kule Mang’onyi kuna mambo ya uchumi mkubwa wa madini, niombe sana mkaboreshe mawasiliano ili kuondokana na tatizo la kiusalama katika eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye eneo hili la hii sheria ambayo tulikuwa tunaambiwa hapa, ni Sheria ya *Electronic and Postal Communication Act* ya mwaka 2010. Sheria hii ni vizuri mkaingalia, imefanyiwa marekebisho mwaka 2010 lakini baadaye ilifanyiwa marekebisho mengine mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachojiuliza ni kwamba kama tulikubaliana mashirika au watoa huduma wote waingie kwenye soko la hisa, kwa nini awe ni mtuy mmoja *Vodacom* aliingia na yeye akatii maagizo ya sheria hii? Wengine bado wanatoa sababu ndogo ndogo ambazo zingine hazina mashiko, lakini kama ninavyosema tunaangalia hawa wahanga waliopata shida na Mheshimiwa Kanyasu ameeleza yeye ni mmojawapo wa wahanga ameweza kupeleka pale hisa zake na bado akitaka kuomba hizo kwa maana aende akauze, anasema haziuziki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu hatuwezi kuuita kama ni utapeli, hatuwezi kuita ni jambo gani, lakini ni jambo lina ukakasi. Mimi niombe sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais ana nia njema na nchi hii Watanzania wake hawa wamewekeza mle hamna sababu tuwaangalia kwa jicho la huruma. Mheshimiwa Sanga nilikaa kule kwa akina Mapembelo ni watu wazuri wa uwekezaji kama wanalia namna ile nani atawekeza kwenye nchi yetu?

Kwa hiyo niombe sana mliangalie siyo vibaya sheria ikitoka ikawa haitekelezeki basi turudi tena tuiangalie, si udhaifu ni kuendelea kujiimarisha na kuifanya Tanzania iwe salama kwa ajili ya wananchi kuishi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema nimalizie kidogo kwamba Mheshimiwa Kanyasu ananiambia kwamba hata wale watoa huduma kwa maana ya wakala wanaeza kuwa barabarani tu wanapata zaidi ya faida milioni tano mpaka kumi kwa mwaka, lakini kama huyu ambaye ametoa hela nyingi kwenye soko la hisa ambayo linauzwa kila siku mpaka huko duniani leo hii anashindwa kupanda anapata shilingi 200 kweli kwa mwaka kwa miaka nane? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sasa kama wanasema wenyewe wataalamu wa biashara wanasema inakuwa ni biashara hasara wakina Meku wanasema hivyo. Hatuna sababu ya kuendelea na biashara hasara, tuwasaidie Watanzania hawa wenye nia njema ya kusaidiana kukuza Uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya naunga mkono hoja ndugu yangu Mbunge wa Ukonga ambaye sasa ndiyo kuna kingine pale sijajua, nikutakie kila lakheri kwenye bajeti hii ukatekeleze vizuri pamoja na watendaji wote wa Wizara, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Miraji Mtaturu. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mheshimiwa Stanislaus Shing'oma Mabula, ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa kwa nafasi ya kuchangia. Niendelee kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuendelea kutoa mchango katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niendelee kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono makubwa aliyokuwa nayo ya kusongesha maendeleo ya Taifa letu. Hakika kupitia sekta hii ya mawasiliano na teknolojia ya habari, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha *vision* kubwa, maono makubwa ya namna ambavyo anatamani kuibadilisha Tanzania na kuweza kunufaika ipasavyo na sekta hii ya mawasiliano na teknolojia ya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika natoa pongezi nyingi sana kwake na kwa nini ninazungumza hivi kwamba ana maono makubwa Dkt. Samia Suluhu Hassan?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia namna ambavyo anasisitiza kuhusu uchumi wa kidigitali na taarifa ambazo Afrika inakwenda kunufaika na uchumi wa kidigitali, utamwangalia Dkt. Samia Suluhu Hassan kumuona ni Rais wa aina gani. *Africa Digital Economy* inatarajiwa mwaka 2025 kufikia thamani ya bilioni 180

na inatarajiwa itakapofikia 2050 uchumi wa kidigitali wa Afrika utafikia bilioni 712. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia kwa uelewa wangu mdogo Wizara hii ni Wizara wezeshi. Ni Wizara wezeshi ambayo inawezesha kurahisisha shughuli na utendaji wa Serikali, lakini kuwezesha kuwa kama kichocheo cha kuchochea uchumi kupitia sekta mbalimbali za kiserikali na sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Wizara hii inayoongozwa na mtu bingwa kabisa shemeji yangu mwenyewe Jerry Silaa. Hakika kwa programu au kwa Mradi wa *Digital Economy,* Tanzania na uchumi wa kidigiti mradi huu ambao ni wa milioni 150 hakika ni mradi ambao unakwenda kufanya mapinduzi makubwa katika Taifa letu. Niwapongeze sana sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wako *Engineer* Maryprisca pamoja na watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kuhakikisha mradi huu wa Tanzania ya Kidigiti unakwenda kusimama sawasawa na umeweka msingi mzuri wa kurahisisha shughuli za Serikali pamoja na kukuza biashara ya uchumi wa kidigitali nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa uchumi wa kidigiti pamoja na uwepo wa Tume ya TEHAMA umeweka msingi mzuri wa kutumia kundi kubwa la vijana ambalo ndiyo *population* kubwa nchini kuhakikisha inakwenda kuzalisha ajira mbalimbali kwa vijana wa Kitanzania. Ukiliangalia soko la *Africa e-Commerce* pamoja na uchumi wa kidigitali unatarajiwa kuzalisha fursa za ajira milioni 200. Kwa hiyo, kuna wimbi kubwa la fursa katika sekta hii ya habari na teknolojia. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika mradi wa uchumi wa kidigiti umefanya mambo makubwa katika Tanzania yetu na umeweka msingi mzuri ambao matarajio yangu kwa sababu mradi huu unakwenda kukamilika, ninaomba sana kuhakikisha uendelevu wa mradi huu. Mradi huu ambao umekwenda kuweka *base* nzuri ya kuhakikisha tunakwenda kukuza muunganiko wa kimtandao *(internet connectivity)* nchini ambalo ni jambo la muhimu katika

kurahisisha *e-Commerce* nchini Tanzania, hakika tunahitaji mwendelezo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeona mradi wa Tanzania ya kidigiti ambao umeweza kutengeneza ile sehemu maalumu ya *data center* ya kuhifadhi *data* zetu katika sehemu moja ambayo ni salama na kuweza kulinda *data* zetu zisiweze kuhamishwa kirahisi kwenda mataifa mengine. Hii nayo ni biashara ndani yetu, *data* zetu zimekuwa zikichukuliwa kirahisi mtu yoyote kutoka mataifa mengine amekuwa akiingia na kuchukua data kirahisi. Maana yake Tanzania tulikuwa tuko uchi, yoyote anaweza kutafuta chochote Tanzania na akaweza kupata lakini kwa miundombinu ambayo imewekwa katika *data center,* ambayo imegharimu bilioni 60 hakika ni mapinduzi makubwa ya Tanzania na Uchumi wa kidigitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, niombe sana, sekta hii ya kuhifadhi *data* zetu na zisiibiwe ni sekta muhimu kwa ulinzi wa Taifa letu. Naomba sana muendelee kuwekeza nguvu katika jambo hili la uhifadhi wa *data* zetu na vilevile kuongeza nguvu katika sekta hii ya kuhakikisha inaunganika kama mlivyopanua wigo wa kuanzisha dirisha la shughuli za kiserikali kwa kupitia mradi huu wa Tanzania ya Kidigiti, mpanue wigo kama ambavyo mmefanya na *NECTA* tayari, kama ambavyo mmefanya na sekta ya madini tayari, kama ambavyo mmeunganika na *NIDA* kwa maana ya kwenda kuanzisha zile Jamii Namba, Jamii *Exchange, N-card* na *soft card* tunatamani muendelee kuingia kwenye sekta ya ulinzi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuona pale Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani Bwana Bashungwa anaona. Mkaunganike tuone namna ambavyo tunapokuwa tunamiliki silaha mfumo unakwenda kutambua wananchi wote wanaomiliki silaha, wananchi wote ambao wanafariki silaha zile zinahamishika vipi? Silaha zile zinarithishwa vipi. Ni kwa kupitia mfumo huu wa kidigitali tunaweza kuendeleza ku-*enhance security* ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie suala zima la hisa ambazo zimewekwa na wananchi wa Tanzania kwa kupitia

Kampuni ya *Vodacom*. Nimependa maono ya wenzangu ambao wametangulia kuyatoa na ninaomba nisisitize kwamba dhamira na lengo la Mtanzania mmoja kuweka fedha zake pale ni kupata faida. Sasa wakati yote yanakwenda kufanyika mimi binafsi sitaelewa zaidi ya kuona ni namna gani ninapata fedha zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo ninaomba Waziri atakapokuja ku-*wind up* aje na kusema ni namna gani Watanzania watapata fedha zao mengine yote ni longolongo. Tunaona ni namna gani watu wame-*invest, end of the day* miaka 10-15 nataka kupata riba yangu ambayo kama ninavyapata *UTT*, ambayo kama ninapata kwenye *treasury bond* na huku nione *the return of the investment* ambayo mimi nimeiwekeza ndania ya miaka 10 niione kiganjani kwangu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, yote yafanyike lakini *at the end of the day* tuone wananchi wamepata fedha zao mikononi na hiyo ndiyo itakuwa *solution, whether* itaendelea ama sheria itabadilishwa *end the day we need money* kwenye mikono yetu na Watanzania tuliwekeza kwa namna njema ya kuweza kurudisha fedha hizo kwenye mikono yetu. Mheshimiwa Waziri hili ninaamini unaliweza, uwezo wako hauna mashaka, tunakutegemea na tunakutarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa 100% ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge. Nilimtaja Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mheshimiwa Banaya Liuka Kapinga na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, wajiandae

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa muda mchache huu kuchangia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri kwa namna ambavyo kwa muda mfupi toka amekwenda kwenye Wizara hii lakini tumeona namna ambavyo amekuwa na juhudi za

juu kabisa kuhakikisha kwamba yeye na wasaidizi wake Wizara inazidi kuwa imara kwa sababu kwa wakati tulionao ni wakati wa kiteknolojia, ni wakati wa kidigitali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaamini kwamba Wizara yako ikifanya vizuri sana ndivyo Taifa letu litakavyoendelea kuboreka zaidi na kama unavyofahamu hata kukusanya mapato hivi sasa nchi nzima kwa kweli kuna wakati tunakoelekea matumizi hata ya fedha za mfukoni yanaendelea kupungua sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nikupongeze sana Mheshimiwa Jerry na kabla sijaendelea nikutakie kila la kheri, sijui ni Ukonga sijui ni Kivule, lakini tunaaamini wewe ni mtu muhimu sana na bado tunakuhitaji kwenye jengo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze pia Naibu Waziri Maryprisca kwa kuendelea kukusaidia, Katibu Mkuu na menejimenti nzima ya Wizara yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba nianzie pale ambapo ameishia Mheshimiwa Ulenge na sisi tunatoka kwenye mikoa na majimbo ya wafanyabishara wengi tumepata changamoto sana kwenye hili jambo ambalo limezungumzwa na karibia kila mmoja hapa juu ya makampuni ya simu kuji-*register* kwenye Soko la Hisa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niongee kienyeji kabisa kama vile ambavyo wapiga kura wetu wanatupigia simu na kuongea kienyeji kabisa. Ukiruhusu kwenye jumba hili kila Mbunge aseme wako Wabunge wa kutosha sana humu ambao wananung'unika kama mmojawapo Mheshimiwa Kanyasu na hawawezi kusema kwa wingi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ilifanya kwa nia njema sana mwaka 2017 kuhakikisha kwamba tunaangalia namna bora ya kuendelea kuboresha maisha ya Watanzania wenzetu kwa kutunga sheria ambayo ilielekeza na ikatoa mwanya kwa makampuni kuji-*register* kwenye soko la hisa na wenzetu wa kampuni mojawapo ya simu ya *Vodacom* wao wakawa *sharp* zaidi na huu u-*sharp* walioutumia haukuwa ni mbaya ulikuwa ni u-

*sharp* wa kibiashara kutokana na sheria tuliyopitisha ingewezekana ikawapa ahueni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu walifuatwa mpaka kwenye makazi yao, walifuatwa mpaka kwenye maofisi kule nje, wakashawishika kwamba inawezekana ukinunua hisa leo za shilingi kadhaa kwa kipande cha shilingi 850 inawezekana baada ya miezi sita ukauza hisa hizo kwa shilingi 4,000 na kadhalika na watu wakaenda mpaka mabenki wakakopa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninao ushahidi wa wananchi kutoka Ukerewe, kutoka Ilemela, kutoka Nyamagana, mmoja tu alikuwa ananiambia kila siku ananipigia simu na Mheshimiwa Waziri nilituma hizi *message* kwako mara kadhaa kwamba mimi nimeenda kukopa benki shilingi milioni 60 mwaka 2017, fedha hii nikaenda kuwekeza, nikanunua vipande vyangu 70,600. Nikawekeza nikitegemea kila baada ya mwaka au kila baada ya miezi kadhaa nitapata gawio langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha sana na ndiyo maana nimesema niongee kienyeji kabisa, toka amewekeza ile fedha shilingi milioni 60 gawio lake la kwanza amelipata mwaka 2024 kwa shilingi 11 kwa *share* kiasi cha shilingi 700,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtu kama huyu ameuziwa nyumba leo anaishi kwenye nyumba ya kupanga. Nataka tulichukue hili kama sisi tuone Mheshimiwa Waziri likuingie ili uone namna ambavyo tunaweza tukafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wengi wa namna hii, sasa tuamue jambo moja, sisi ndiyo tunatunga sheria Mheshimiwa Waziri turudi humu ndani tutakaporudi, sheria hii tuiangalie na tuifanyie marekebisho na tutakapoifanyia marekebisho tuamue mambo yafuatayo; aidha, tuamue kurejesha fedha za watu na faida au tuamue vinginevyo iliwatu wetu hawa wanaoteseka na nia yao njema ya kuwekeza waweze kupata unafuu wa maisha. Leo ukimuuliza Mheshimiwa Kanyasu hapa… *(Makofi)*

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa ya Mheshimiwa Kiswaga.

**TAARIFA**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana mchangiaji anachangia vizuri, lakini hapa tusimwingize matatizoni Waziri; moja, kwamba unajua hisa huwa inapanda na kushuka, inawezekana umeweka hapa laki mbili baada ya miaka miwili hela yako ikawa 40,000 inategemeana na hisa inavyopanda. Sasa unapomwambia Waziri aende akaiambie *Vodacom* au kampuni fulani siyo kwamba naitetea *Vodacom* lakini naelezea biashara ya hisa ilivyo.

Kwa hiyo, tusimwingize Waziri matatizoni hapa, kama ni suala la kubadilisha sheria tutabadilisha, lakini siyo suala la kusema alipwe na faida, atalipwa na faida kutoka wapi? Kwa sababu hisa kama imeshuka utalipwaje na faida, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana Mheshimiwa Kiswaga, mimi ninafahamu huyu amekuwa... *any way* nisiende huko hoja yake siipokei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachojaribu kusema Mheshimiwa Kingu alieleza vizuri sana kwa *details* kwa nini tulifikia hapa na mimi nimetaka kusema niongee kienyeji sana ili nieleweka na walionituma. Ningeweza kwenda kwa utaratibu mwingine kabisa, lakini ninachotaka kusema Mheshimiwa Waziri ndiyo amebeba Wizara hii. Wizara ya Mawasiliano ndiyo mama mlezi wa makampuni yote ya simu Tanzania, sasa anataka mimi niondoke hapa nikalalamikie kampuni la simu nyumbani kwake, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaeleza changamoto wanazozipata wananchi na sisi Wabunge miongoni mwetu tumeingia kwenye hili jambo, tumenunua hisa mwaka 2017 leo miaka minane, utaratibu gani unafanyika. Ninachotaka Serikali

iingilie kati kujaribu kusaidia wananchi, *it's over,* nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili Mheshimiwa Waziri tunao mradi wa Mkongo wa Taifa; Mkongo wa Taifa wengi tunapenda kuuita ni *SGR* nyingine na Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana umeeleza vizuri kwenye mafanikio tuliyonayo. Sasa hivi tuko takribani wilaya 109 ambazo zimeshafikiwa na Mkongo wa Taifa, lakini malengo yetu ni kufikia wilaya zote nchini. Sasa Mheshimiwa Waziri tunazifikia wilaya kwa kiwango gani? Je, tunafika tu makao makuu ya wilaya tunaacha tunaondoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitamani Mheshimiwa Waziri kuna maeneo bado hatujafanya vizuri sana kwenye matumizi mazima ya usambazaji wa Mkongo wa Taifa na Mheshimiwa Waziri hapa tu kwa kuokoa muda labda tufahamu kwanza uwezo wetu tulionao wa ndani na tunasambaza mkongo huu tumeshauzambaza asilimia ulizozitaja Mheshimiwa Waziri karibia 40% nadhani bado ni kidogo sana kulinganisha na uhitaji tulionao. Kwa mafano umesema maeneo ya wazi 50 peke yake. Je, ni kweli ukiona maeneo ya Waziri nchi hii kwenye miji mikubwa tu ukichukua Dar es Salaam peke yake unaweza kumaliza hayo maeneo 50, hujaja Mwanza, hujaenda Tanga, hujaenda Mbeya, hujaja Dodoma na sehemu zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninachotaka kusema nikuombe Mheshimiwa Waziri kupitia wewe mwenyewe na timu yako nzima unao wataalamu wa kutosha, hebu tujikite kwa nguvu zote tulizonazo hii biashara wamesema hapa wenzangu. Kwa nini tunakwama? Kwa nini mpaka leo usafiri na *SGR* kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma hapa kuna maeneo katikati unapoteza kabisa mawasiliano, lakini unaenda kwenye kituo cha stesheni kimoja nimekaa juzi nisikitaje jina nimekaa karibia masaa mawili nasubiri treni hata pale penyewe tumeshindwa kufunga mkongo wa mawasiliano ili angalau tunapata *internet* muda wote. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu suala la kibiashara hebu tulitazame kiukweli kabisa tuone hapa

nchini kwetu uwezo wetu wa usambazaji na uzalishaji wetu unafanana na huko tunakopeleka nje? Huko tunakowapelekea nje wako tayari au hawako tayari na kama hawapo tayari sisi tumechukua *initiatives* gani au ndiyo *easy* tu leo tunataka tukifika pale *border* tumemaliza, lakini ukienda Congo wanatuhitaji sana, ukienda Rwanda wanatuhitaji sana, ukienda Burundi wanatuhitaji sana, Kenya wenyewe wanatuhitaji sana kuliko chochote kile kupitia mkongo huu. Kwa hiyo, ninakuomba leo tulitamani sana, hata Dar es Salaam yenyewe tunayoizungumza ingekua imejaa Mkongo wa Taifa kila sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo viko vikampuni vya simu vimekuja vinaanza kuteka baadhi ya maeneo. Mheshimiwa Waziri utajikuta wewe kwa sababu hii ni biashara tena unaanza kutoa bure na hii sio biashara ya bure tulitegemea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** ... kila sehemu mimi nikisimama hata pale *Nyerere Square* ninaweza kukaa nikaangalia kwenye *internet* nikakutana na *internet* ya Mkongo wa Taifa nikajaza pale nikachati kwa muda mrefu na gharama nafuu kabisa ambayo nitakayoifanya.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri na nikutakie kila la heri na ninaamini kwamba utakapokuja ku-*wind up* utatupa majibu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninakutakia kila la heri Mheshimiwa Waziri Mwenyezi Mungu akutangulie. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stansalaus Mabula, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Benaya Kapinga na Mheshimiwa Salome Makamba, ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, sauti yangi sio nzuri lakini mtanivumilia na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaunga mkono hoja, lakini naomba nitumie jukwaa hili kuwapa pole wananchi wa Kata ya Lukalasi katika Kijiji kile cha Maliba wananchi watatu waliingia kwenye mgodi bahati mbaya wakabomokewa na gema, kwa hiyo, wamekaa ndani siku tisa na wawili wamepatikana usiku wa kuamkia leo wakiwa tayari wamefariki, bado wanamtafuta mmoja.

Kwa hiyo, ninawapa pole sana wananchi wa Kata ya Lukalasi. Tunajua wananchi hawa walikuwa wanaenda kujitafutia kipato, lakini limewakuta hilo janga. Mwenyezi Mungu azipokee roho za marehemu mahala pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niishukuru sana Wziara hii, Nimshukuru Mheshimiwa Jerry Silaa lakini nimshukuru Naibu Waziri na wataalamu wote katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mimi ninaingia jimboni kwangu tulikuwa na shida sana ya mawasiliano, kata 16 zote zilikuwa hatupati mawasiliano. Ukipata mawasiliano basi ni yale ya kubahatisha bahatisha ama ukae kwenye mti au ujiegemeze sehemu fulani, lakini nikushukuru sana Mheshimiwa Jerry umefika hapa kupitia ile miradi ya ujenzi wa minara, leo hii kata zote tunapata mawasiliano vizuri, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pale Sala ujenzi wa mnara umekamilika, pale Kihangimauka ni kilometa 15 tu ulikuwa unatoka Mbinga Mjini tulikuwa hatupati mawasiliano; kilometa 15 tu. Leo hii tayari mnara umekamilika wananchi wanapiga simu wanafurahia mawasiliano, lakini ukienda katani kwangu mwenyewe nilikuwa ninapata shida leo hii Tigo, Vodacom, Airtel,

na Halotel wapo, mitandao minne, kwa kweli tunakushukuru sana. Ukienda Kata ya Kitura ni hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua jimbo lile lina milima, kwa hiyo, ilikuwa shida sana kufanya *connection,* lakini kazi kubwa imefanyika. Nikupongeze sana wewe na nimpongeze Naibu Waziri, lakini pia niwapongeze wataalamu wako, wataalamu wale wa kanda ni wasikivu sana, ukiwaambia wanakwenda mara moja wanachukua hatua. Sasa hivi tulikuwa na shida ya *internet* wameenda wameongeza uwezo wa *internet* baadhi ya maeneo tunapata ile *4G* na bado *2* na *E,* lakini ninajua mko mbioni kuongeza kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili linalosemwa hapa la mkongo ninajua umefika Mbinga, sasa haujasambaa. Ninaomba sana sasa uende kwa kasi. Sisi Wana-Mbinga tunapenda ku-*google*. Tunapenda kutafuta bei ya mazao na unajua sisi ni wakulima sana. Kwa hiyo, ninaomba sana kupitia hiyo endeleeni kupeleka huko, lakini kiujumla ninashukuru sana. Sasa hivi zile kata ambazo zilikuwa na shida kama utakosa mtandao fulani basi wa pili lazima uupate, sasa hivi hatuna shida kiasi kile. Kwa hiyo, ni kazi kubwa na nzuri imefanyika. Hongera sana Waziri na timu yako kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine na mimi nimepatwa na butwaa hapa kidogo kwenye hili jambo ambalo linasemwa la suala la uwekezaji wa Vodacom. Ni kweli na Mheshimiwa Kiswaga ametoa taarifa hapa kwa Mheshimiwa Mabula, biashara ya hisa ina kupanda na kushuka. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Mabula alisema mimi ninaongea kienyeji na ni kweli kabisa, Watanzania wengi hawako kwenye hizi biashara, ni mambo ambayo watu wanajifunza baada ya kusikia huko duniani watu wamefanya biashara ya hisa wakatajirika na Watanzania sasa wanataka kujiingiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachosema hapa ni kuona hasara waliyopata Watanzania hawa tuwasaidie. Ni ukweli kabisa kwamba ukiwekeza kwenye hisa kuna kupata faida na kuna kuporomoka. Kwa hiyo, Wtanzania hawa hata tulipoanzisha

mfumo huu wa kununua vipande vya Umoja, kuna Watanzania walienda wakakopa kwenye benki. Bahati nzuri Serikali ilifanya jambo moja zuri sana, vipande hivi vya Umoja vilikuwa vinauzwa kwa shilingi 70 na Serikali ilikuwa ina-*top up* shilingi 30 kujaribu kuwahamasisha Watanzania hawa waweze kuingia kwenye hii biashara. Unaona kitu kama hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo inafanya vizuri, hii biashara ni nzuri sana na pale ambapo inafanya vibaya ndio yanatokea mambo kama haya.

Kwa hiyo, ombi langu mimi hapa na ombi la hawa Watazania walioingia kwenye hii biashara kuomba huruma ya Serikali. Nini kifanyike ili hii hela iliyowekezwa pale ikalala iweze kuwakomboa. Kama mfano alioutoa Mheshimiwa Mabula pale, mtu kaenda kukopa shilingi milioni 60, akaenda kuwekeza kwa nia kwamba angepata faida. Bahati mbaya ile hela iko kule imezama na ikizama haimsaidii yule Vodacom na haimsaidii huyu aliyewekeza. Sasa ina maana gani? Hela imekaa tu pale imelala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni bora Mheshimiwa Waziri haya mambo yanawezekana. Kama kuna *loophole* ya kukaa chini na *initial owners* mkafanya *resolution* ya aina yoyote ile ili kuwasaidia hawa watu lingekuwa jambo bora sana kwa nchi yetu. Mimi ninajua nia njema ya Serikali ni kutaka kuwafanya Watanzanua waone huu uchumi na ni kitu kizuri sana, lakini sasa tumefika sehemu tumekwama. Tuendelee kukaa tu hivi hivi tukwame? Hapana, ni lazima tuwasaidie Watanzania hawa mwisho wa siku nchi iende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kile hii Vodacom ilikuwa iko juu sana, yaani siyo uongo ilikuwa inafanya vizuri sana na ndiyo maana unaona hisa moja iliuzwa shilingi 850. Katika bei hizi za hisa ukiona kampuni inauza hisa kwa shilingi 800 naa ujue iko kwenye nanihii kubwa sana. Kwa hiyo, kwa kadiri inavyokwenda tulitarajia baada ya mwaka au baada ya nini, hisa ipande ifike hata shilingi 1,000 au 2,000 lakini sasa imeenda inashuka, maana yake ni kitu ambacho siyo cha kawaida. Kwa nini? Kwa sababu kampuni

haijafanya vizuri. Sasa kama haijafanya vizuri kuna namna ya kuifanya kampuni iweze kuongeza, halafu ifanye vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, njia moja ya kufanya ni kufanya *resolution,* wafanye *resolution* na Waziri yuko kwenye nafasi ya kuwasaidia hawa waliokuja wakanunua na wale *initial owners* ili kufanya hiyo *resolution* na mwisho wa siku Vodacom iweze kusimama kama kampuni nyingine. Mbona Tigo hawajaingia na mbona wale wengine hawajaingia? Ili sasa wote wawe kwenye nanihii moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nzuri ni lazima i-*practise* kwa wote, sheria inayo-*practise* upande mmoja haifai, yaani kwa nini muibane Vodacom tu, kwa nini isiwabane na wale wengine kule? Sheria ili iwe nzuri, wote wawe sawa kwa sababu wote hawa ni *competitors,* Wote wawe kwenye *level* moja.

Mimi ombo langu, wewe Mheshimiwa Waziri ni wakili msomi, unayajua haya mambo, ni kweli kabisa his ani biashara ipo lakini inawezekana ikauzwa na inawezekana tukafanya *resolution* mkakubaliana nini kifanyike kati ya wawekezaji hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niombe sana, tafuta huo mwanya muweze kuwasaidia Watanzania hawa. Watanzania hawa ni maskini mno, wameambiwa tu ukiwekeza unapata faida. Sasa bahati mbaya wamewekeza wamepata hasara. Tuwasaidie waokoe hata kidogo kilichobaki huko wafanye mambo mengine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha?

**MWENYEKITI:** Kengele imelia.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya Kapinga ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba na Mheshimiwa Frorent Laurent Kyombo ajiandae.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Wizara hii muhimu sana ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kujaribu kumshauri Mheshimiwa Waziri, nianze na hili suala la hisa na Sheria ya Kielektroniki na Mawasiliano ya Posta *(The Electronic and Postal Communications)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchokisema Wabunge wenzangu, sisi hatuombi hisani ya Serikali, wananchi warudishiwe pesa zao. Tunaitaka Serikali iingilie kati changamoto ambayo wao wenyewe kama Serikali wameisababisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu moja; sheria hii imefanyiwa marekebisho kuanzia 2010, 2017 na 2022. Ukisoma kifungu cha 26 cha sheria kinasema watoa huduma wote wa mawasiliano ni lazima wahakikishe wanauza 25% ya *share* zao kwa umma na ikaenda mbele zaidi ikatoa mpaka *deadline,* ikasema ndani ya miaka miwili baada ya sheria hii kusainiwa ni lazima wawe wameuza *share* zao kwa umma. Wakatoka hapo wakatoa mpaka na adhabu kwa wale ambao hawatafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mashirika yanaweza yakashindana na Serikali? Walifuata kile ambacho Serikali ilitaka. Vodacom akaenda kuuza *share* kwa umma na wananchi kwa sababu hawakulindwa na hawakupewa elimu, walienda kununua zile *share* na wamenunua *share* wamepata hasara. Tatizo hili kalisababisha nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi wa Shinyanga hajui hata ofisi za Vodacom zinazouza hisa ziko wapi, mwananchi wa Katavi hajui ofisi za *share* za Vodacom zinakouzwa. Yeye alienda

benki, akakopa hela akanunua kwa sababu alijua Serikali ipo inamlinda na itamsimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea *billions of moneys.* Tunawaongelea Watanzania maskini ambao wameathiriwa na sheria hii. Kukiri kosa siyo udhaifu. Tulitunga sheria ambayo leo imesababisha hasara kubwa na hata Serikali yenyewe inakiri. Walisema kampuni zote za mawasiliano, watoa huduma siyo Vodacom na Tigo peke yake. Wale wanaouza *fiber,* sijui *data* na nini, wote wanatakiwa wahakikishe wanauza *shares* zao 25% kwa umma. Wamefanya Vodacom peke yao. Serikali imefanya nini kwenye hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sheria haitekelezeki, kurudi nyuma siyo kukiri udhaifu. Tunataka Serikali iingilie kati na leo hii mimi ninawajua wengi na wengine ni Wabunge wako humu ndani wamenunua hisa za shilingi milioni 20, lakini leo wakienda kule hisa haziuziki wanalipwa shilingi milioni nane; shilingi milioni 12 ni hasara. Hilo ndilo lilikuwa lengo la Serikali kufilisi watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni lazima iingilie kati kama mtu wa katikati kati ya mwananchi na hii kampuni ya Vodacom ambayo imeuza *shares* zake ambazo leo zimedorora na wananchi wamepata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema kwamba suala hili tuwaachie Vodacom na wananchi ndiyo hivyo hisa za shilingi milioni 20 mtu analipwa shilingi milioni nane. Amewekeza kwa miaka, ana madeni, ana riba na ana marejesho. Hela hizo za kuongezea atazitoa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaishauri Serikali na siyo kwa mara ya kwanza, tukubaliane tu, makosa yalifanyika. Siku zote kwenye maeneo ya biashara *market force* ndiyo inaamua mtu akauze *shares.* Mimi nimefungua kampuni yangu ya *private,* ninafanya biashara, ninataka niongeze mtaji, zipo njia nyingi. Ninaweza nikaenda kuchukua mkopo lakini pia ninaweza nikaigeuza kampuni yangu kutokana na sheria za kampuni ikawa kampuni ya umma nikauza *shares* kwa watu na nikapata mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kampuni zilishinikizwa na Serikali ikwenda kuuza *share* kwa *public* kwa sheria ya mwaka 2022. Ni lazima Serikali i-*take responsibility* kwa kuingilia kati hizi *billions of moneys* za Watanzania. Walipwe na tena walipwe siyo tu, wanasema ni lazima wafanyiwe *indemnification.* Walipwe na walipwe na pale ambapo wamepoteza ili kusudi *next time* kosa kama hili lisijirudie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulifafanua vizuri suala hilo ningeomba niongelee suala la wizi wa mitandaoni na huduma za hzi kampuni za simu. Hata wewe mwenyewe na Mheshimiwa Spika ni mashahidi. Sisi ambao tuko kwenye mitandao tunaona kila siku namna ambavyo majina yetu yanatumika vibaya. Watu wanatapeliwa tuna kwenye namba hii na watu wanatapeliwa fanya hiki. Sasa hivi tumekwenda mbali na hii akili mnemba, yaani mtu anaweza akajiita Salome na akafanya jambo ni ikaonekana nimefanya mimi. Tunayo Wizara, tumetunga sheria hapa za mitandao, kwa nini jambo hili halifiki mwisho na kwa nini halisimamiwi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye uchaguzi, unaweza ukashangaa wewe mwenyewe Mheshimiwa Jerry mtu anatuma *message* kupitia akili mnemba anasema mimi Jerry Silaa sigombei na hiyo ni *a night before voting*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yametokea kwenye nchi za wenzetu, ni lazima tudhibiti *immediately* haya mambo ya wizi na utapeli wa mitandaoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *short of that* tunaliingiza Taifa kwenye mazingira ambayo kila mtu hayuko salama na mimi ni *champion* wa kuhakikisha kwamba tunapata mwongozo, sheria na taratibu nzuri inayodhibiti matumizi mabaya ya akili mnemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo changamoto kubwa na hili ningeomba tu Mheshimiwa Waziri atoe mwongozo, unapokuwa umetuma pesa kupitia mtandao ikatokea fedha zile hazijaenda zile fedha zitarudishwa, lakini ile ada iliyotumika kutuma ule muamala haitokaa irudishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni fedha kidogo, shilingi 500, shilingi 1,000 au shilingi 1,200 lakini hizo fedha kidogo ndizo zinakuwa nyingi. Sisi tunaitaka Serikali itulinde sisi walaji. Ninatamani sana tulisimamie hilo na fedha za watu ziweze kurejeshwa pale ambapo inatokea muamala haujafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nichangie kuhusu Mkongo wa Taifa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesema vizuri sana. Mkongo wa Taifa ni uwekezaji mkubwa na kwa *East Africa* pengine sisi ndiyo tumefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye Mkongo wa Taifa. Ni kwa vile jambo hili halionekani kwa macho, lakini kwa uwekezaji huu, nimeisoma vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri, haelezi mahitaji ya zinazoizunguka Tanzania kwenye Mkongo huu wa Taifa ni kiasi gani, hajatueleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama haitoshi sisi tumeuza kwa kiasi gani bishaa hii, kwa sababu hizi fedha ni za Watanzania. Mwisho wa siku hii ni biashara ni lazima iuzwe na ni lazima tupate *return* n ani lazima sisi kama nchi tunufaike kwa sababu mwisho wa siku ni suala la biashara. Usipokwenda ndani ya muda utajikuta unapata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba. Nilimtaja Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo na Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Kwanza kabisa, nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ndani ya Wizara hii na nikipata *reflection* ya kazi nzuri ni ongezeko la bajeti ndani ya Wizara yetu hii tunaona mwaka 2024/2025 Wizara hii ilitengewa shilingi bilioni 180.9 lakini leo Wizara inaomba shilingi bilioni 291.5 tunaamini

maono na malengo ya Mheshimiwa Rais yanaenda kutimia kupitia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Jerry Silaa ambaye ndiyo nahodha wa Wizara hii akimwakilisha Mheshimiwa Rais vizuri, lakini tunaona akisaidiwa na Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi na Katibu Mkuu, kaka yetu Mohammed Abdulla na Naibu Katibu Mkuu - Nicholaus Mkapa pamoja na wakurugenzi wote na watendaji wote ndani ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kwa miaka hii ambapo imebadilishwa na kutengenezwa vizuri imefanya kazi kubwa katika maeneo yetu na Taifa kwa ujumla na baadhi ya maeneo ambayo tutashauri ili kuweza kuendelea kuboresha katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza mimi niombe kwanza niishauri Wizara, tumefanya kazi kubwa ya kuweka *postcode* katika maeneo mbalimbali ndani ya nchi yetu na kwa kweli zimewekwa alama mbalimbali katika maeneo yetu, lakini sasa hivi ukipita maeneo mengi hizo *postcode* zote ziliondolewa na ziliibiwa nafikiri kupitia vyuma chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tungeitaka Wizara kwa kazi nzuri ambayo ilifanyika kwa weledi mkubwa kuweza kuonesha mitaa yetu na kui-*locate* ili iweze kutambulika kirahisi, ni mkakati gani sasa mpya ambao Wizara yetu hii inakuja nao kuhakikisha sasa inarudisha uhalisia kama ambavyo kampeni kubwa na kazi kubwa imeweza kufanyika katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika mitaa mbalimbali utakuta kwa kweli vibao havipo. Sasa tungalie nchi nyingine mbona vibao vinakuwepo. Ukienda hapa Rwanda unakuta mitaa yote imekuwa *addressed* vizuri kwa *postcode* ambazo zipo. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri ninaamini kwa kazi nzuri unayoifanya utakuja na jibu la suluhisho hili ili sasa lengo la kitaifa ambalo lilikuwepo liweze kwenda vizuri na mitaa yetu iendelee kutambulika kwa *postcode* ambazo zimewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili mimi ninaomba nipite katika falsafa ya Mheshimiwa Rais ya *4R,* Mheshimiwa Rais alikuja na *4R* na mimi nitaongelea "R" mbili tu; ya *reform* na *rebuild.* Hiyo falsafa ya Mheshimiwa Rais ameileta ili kurekebisha pale ambapo tutakuwa tunaona tunaenda vizuri na ambapo hatuendi vizuri tuweze kuparekebisha na pale ambapo pana mapungufu tuwe kujazia ili tuweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukaona kwa nini Wabunge wengi wamechangia katia Sheria hii ya *Electronic and Postal Communication* ya mwaka 2010 mpaka 2022 ni kwa sababu tunaona kwamba, kuna eneo ambalo halikai vizuri. Mheshimiwa Rais ameshatupa *room* ya kupitia kwenye "R" hizi mbili to *reform* na *rebuild* ili kuweza kuweka pale kwenye mapungufu, kufanya masahihisho na kuweza kurudi kwenye mstari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wengi wamechangia katika mabadiliko ya sheria hii, lakini kwa sababu hii sheria ilitungwa kwa nia njema lakini matokeo yake yamekuwa ni tofauti. Sasa chombo chako hiki Bunge hili Tukufu kazi yake ni kurekebisha sheria pale ambapo inakuwa inaonekana haifanyi kazi vizuri. Sasa hatuna budi na tusiwe na kigugumizi kuhakikisha kwamba hii Sheria ya *Electronics and Postal Communication* ya mwaka 2022 inarekebishwa ili kuweza kuendana na hali ya kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia makampuni yote ambayo yalitakiwa yawe *listed* hayajawa *listed* lakini kampuni moja imekuwa *listed,* lakini imeweza kuleta hasara kwa wananchi wetu. Wananchi wakiuza hisa Taifa na lenyewe linapata pato la Taifa. Sasa tusione kwamba hapa ni wananchi wanaoumia peke yake, lakini hata Taifa letu linaumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana na Waziri akija hapa atuambie walivyojipanga kuhakikisha kwamba inaleta marejeo ya sheria hii iweze kurekebishwa ili wananchi wetu ambao sasa wamenunua hisa katika kampuni ambazo zimetajwa

Vodacom na maeneo mengine ili waweze kurekebishiwa na waweze kuona jinsi gani wataweza kufidia hasara ambayo wameipata pia na Taifa letu liweze kupata pato kutokana na hizo hisa zikiuzwa au gharama yake ikiongezeka ili iwe faida kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu lingine katika eneo hili nataka nishauri katika eneo la Mkongo wa Taifa. Tunaona kazi kubwa ambayo Taifa imefanya, tukirejea miaka ya nyuma hapo tulikuwa hatuwezi kuongelea hata Mkongo wa Taifa, lakini leo tunaweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuongelea Mkongo wa Taifa. Ni kwa sababu kazi kubwa na nzuri ambayo Mheshimiwa Rais wetu na Serikali yake na wasaidizi wake kupitia Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Naibu Waziri na wengine wamesaidia kuhakikisha kwamba hilo suala linatimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika matumizi ambayo ndani ya nchi yetu, Mheshimiwa Mabula pale alishauri, tunahitaji kuona *consumption* ya mkongo huu ndani ya nchi yetu unawafikia hata wananchi wangu wa kule Kitobo, wananchi wa huku Nkerenge na wenyewe waweze kutumia huo Mkongo wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, tunataka kuona ni jinsi gani Taifa letu sasa kwa kutumia hii fursa tulionayo imeweza kutanua na kuweza kuuza hii huduma nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kuwa na amani na utulivu inatupa nafasi ya kuwa soko zuri katika nchi zote zinazotuzunguka ziwe za *East Africa* au *SADC* ili kuweza kufanya biashara. Nilikuwa naangalia takwimu hapa nchi ya Uganda karibu 95% ya *internet* inapokea kutoka Kenya, lakini tunajua mahusiano mazuri ya Tanzania na Uganda, lakini tunaona kukua kwa mahitaji ya *internet* ndani ya nchi ya Uganda ni *almost* 25% kila mwaka. Kwa hiyo, bado nafasi ipo. Sasa tunatumia njia gani ya kuweza kushawishi wenzetu ambao tuna ujirani mwema nao iwe ni Uganda au nchi zingine kuweza kupeleka huduma hii na Taifa letu likapata pato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe pia Mheshimiwa Waziri wakati anakuja kuhitimisha atupe mpango mkakati ambao Wizara inayo ili kuweza kuhakikisha kwamba sasa huu mkongo wetu wa kitaifa unaweza kuingiza pato la Taifa letu na nchi yetu iweze kupata fedha na sisi tunahitaji vituo vya afya, tunahitaji zahanati, tunahitaji shule mpya na barabara ziendelee kuboreshwa kutokana na hilo pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu lingine nilitaka kusimama hapa kushukuru kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Missenyi kwa kazi nzuri ambayo Wizara ya Mawasiliano imefanya, imejenga minara katika maeneo yetu katika vijiji tofauti. Niombe Mheshimiwa Waziri bado maeneo ya Kata ya Kashenya unajua sisi tunapakana na Uganda mara nyingi tunapata mtandao wa Uganda, lakini Kanyigo bado mtandao wa shida, Kata ya Bugandika bado ni shida, Kata ya Kitobo, Kilimile Mabaale bado ni shida na Minziro na Nsunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo tumeweza kufunga minara Kakindo tunakushukuru sana, Nkerenge tunashukuru, lakini Bwenko, Makule, Kakunyu na Buchurago hiyo minara wananchi wameipokea pamoja na Kakunyu eneo hilo kwa kweli sasa hivi kuna usikivu mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru kwa nafasi na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Florent Kyombo, nilimtaja Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan na Mheshimiwa Naibu Waziri Maryprisca ajiandae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi mchana wa leo na mimi nichangie bajeti ya Wizara hii ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema kila mmoja wetu kutimiza wajibu wetu,

lakini nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo amekuwa akiendelea kulea sekta zote bila kubagua sekta yoyote na maendeleo hayo yanaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ongezeko la bajeti hii ya Wizara hii kutoka shilingi bilioni 180 mpaka shilingi bilioni 291 ni nia njema ya Mheshimiwa Rais wetu kuhakikisha sekta hii inafanya vizuri. Niipongeze pia Serikali kwa jinsi ambavyo wamefanya *disbursement* katika bajeti hii. Ukiangalia bajeti ya maendeleo katika Wizara hii Mheshimiwa Waziri mmefanya *disbursement* ya 90% katika shilingi bilioni 140 lakini shilingi bilioni 137 kwenye maendeleo imekuwa *disbursed* na sekta zake zote zimefikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wetu kaka yangu Jerry, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na timu nzima kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkifanya kazi, lakini mmekuwa mkitufikia tunapowahitaji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia ni mnufaika wa huduma za Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Wizara nzima. Nilikuwa na maeneo matatu ambayo yalikuwa hayana mawasiliano ya Chemchem, Himiti pamoja na Imbilili. Mlituma wataalamu wenu wakafika kuongeza nguvu katika ile minara na inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze kwa jinsi ambavyo pia hata katika minara hii 758, minara 482 mmeshamaliza kazi na mnaendelea vizuri, hongereni sana na endeleeni kuchapa kazi bila kuchoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize tu kwa sekta zake Serikali inatenga fedha na *disbursement* katika miradi ya maendeleo inaenda vizuri. Nadhani sekta zenu ziweze kukusanya vizuri kwenye makusanyo naona kama mko 60%, ninyi mkiongeza nguvu katika kukusanya naamini ipo siku mtajitosheleza na nisisitize kwa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi naona makusanyo ni 20%, kwa hiyo, ni vyema wakaongeza nguvu katika makusanyo kwa sababu hauwezi ukatumia wakati haukusanyi. Kwa hiyo, 20%

ni ndogo sana ukilinganisha na wengine ambao wameweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili ambayo ningependa kushauri; jambo la kwanza, ni suala la kuhuisha mfumo wa takwimu ya makosa ya kimtandao kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na wenzetu wa *TCRA*. Hili ni jambo jema. Mheshimiwa Waziri makosa ya kimtandao yamekuwa yakiwakwaza Watanzania wengi sana. Matumizi ya *whatsapp* zetu watu wanafanya ku-*hack whatsapp* zetu lakini simu zetu, *message* za kitapeli. Kuna watu wanaweza wakawa wanapiga simu tu kusumbua watu, wanatukana, wanadhalilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ifikie hatua sasa ni muda muafaka Mheshimiwa Waziri kama ulivyoeleza kwenye hotuba yako kwamba mtakapohuisha, nashauri muweze kuwaweka pamoja, pawepo na *single source* ya kuhudumia tatizo hili la makosa ya kimtandao. Kwa sasa hivi tuko na Jeshi letu la Polisi liko Wizara ya Mambo ya Ndani, pia *TCRA* iko kwenu nimpongeze sana *DG* Dkt. Jabiri amekuwa akipambana sana. Jeshi la Polisi ni Wizara nyingine, lakini *TCRA* iko Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake ameeleza pia jinsi ambavyo wana mpango wa kuwezesha Jeshi la Polisi Makao Makuu kwa kuwanunulia vifaa vya kisasa. Ushauri wangu wasiishie pia Makao Makuu tu, waende mpaka kwenye mikoa, waende mpaka kwenye Wilaya hivyo vifaa viwezeshwe kwenye maeneo hayo ili Jeshi la Polisi wakishirikiana na *TCRA* na Ofisi ya Mashtaka wawe kwenye sehemu moja, washughulike na jambo hilo tu, wataalamu wachukuliwe kutoka maeneo hayo kama ni Jeshi letu la Polisi, wachukuliwe hao wataalamu wanaohusika na masuala ya *cyber crime* wachukuliwe na wenzetu wa *TCRA* wakiwa na mitambo yao wasimamiwe na sehemu moja ili wafanye kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mwananchi akipitia kwenye matatizo hayo, ataenda polisi, lakini polisi wataenda *TCRA* mpaka waje kwa pamoja waweze kulitatua makosa mengine yanakuwa yameshajitokeza na muda unakuwa umeenda, anakuwa

hajashughulikiwa kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wewe una nia njema kununua hivi vifaa kwa Jeshi la Polisi, lakini sasa wangekaa sehemu moja ingekuwa rahisi zaidi ili waweze ku-*solve* mapema makosa ya kimtandao. Kwa kweli yanadhalilisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta wana-*hack* simu ya mtu, wanaanza kuomba fedha, wanasema mimi fulani nimepata matatizo watu wanaanza kutuma pesa mpaka waje wachukuliwe hatua muda unakuwa umeenda. Kwa hiyo, mkiwaweka kwenye *single source* ya kuwahudumia inaweza ikasaidia sana, hili mlifanyie kazi, lakini ikiwapendeza kama Serikali muone jinsi ya kuwaweka pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka kushauri siku ya leo ni suala la vipimo vya *bundle*. Kwa hali ilivyo sasa hivi mitandao ya simu iwe ni Airtel, iwe Vodacom na mitandao mingine yote wanaoamua na kusema kwamba umetumia hilo *bundle* ni mtandao husika. Mimi ushauri wangu Mheshimiwa Waziri pawepo na *center* ya kupima, pawepo na taasisi ya kupima matumizi na haya malalamiko ya wananchi dhidi ya mitandao na matumizi ya *bundle*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mimi natumia kampuni ya Airtel nitaweka *bundle* la shilingi 5,000 sijatumia vizuri utasikia ni matumizi yako tu lakini naenda kulalamika kwa nani? Nani anakwenda kuona kwamba kati ya mtandao wa simu na mimi *customer* wao ni nani ambaye amedhulumiwa?

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninadhani kupitia mitandao ya simu mkae chini na *TCRA* muone ni vifaa gani vitatumika kupima matumizi hayo badala ya kuwaachia mtandao husika ndio useme kwamba huyu mtumiaji alitumia hili *bundle* kwa matumizi yake, wakati mwingine mtu anaweka *bundle* hata hajawasha simu tayari *bundle* limeisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mnafanya kazi nzuri hebu mliangalie hili limekuwa likizua malalamiko mengi na matumizi ya *bundle* na mawasiliano kwa Taifa letu tumeona tuna

laini zaidi ya *line* ambazo zimesajiliwa. Laini za *bundle* ni kama milioni 49 za simu kama milioni 90 sisi tuko milioni 60 watumiaji ni wengi. Ninadhani tunahitaji *control mechanism* ya kuhakikisha hawa *customers* hawaonewi na mtandao wa simu usiwe ni hakimu mwenyewe akajijaji mwenyewe wakati kuna malalamiko mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya *bundle* hizi na mawasiliano kwa nchi yetu ilipofika na kwa maendeleo tuliyonayo hayaepukiki. Kuna mtu kila siku lazima aingie *internet,* kuna mtu kila siku lazima awasiliane. Kwa hiyo, mkiweka *control mechanism* ya matumizi haya mtakuwa mmefuta kilio cha Watanzania wengi ambao wamekuwa wakionewa katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Pauline Gekul nilimtaja Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Ramadhan Suleiman ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja ambayo iko mbele yetu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunatambua kwamba mawasiliano hasa ujio wa *internet* na simu hizi za kiganjani ni mapinduzi makubwa ambayo tumeyashuhudia katika miongo hii na kwa sasa tuna *generation* ambayo iliishi kabla hakuna simu za kiganjani, hakuna *internet* na sasa iko kwenye *generation* ambayo tuko katika mukhtadha huu wa mawasiliano ambayo ni jambo ni dunia nyingine kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Waziri kwenye ripoti yake na kwa mujibu wa ripoti ya *TCRA* ya mwezi Machi, 2025 jumla ya laini za simu zilizopo ni milioni 90 ambayo ikiwa ni ongezeko zaidi ya Watanzania ambao wako miliomi 60, kwa hiyo iko zaidi milioni 30 mbele ya laini nadhani na ile mtu anakuwa na mitandao kama mitatu yote anakuwa na laini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *internet users* wako karibia nusu ya ile milioni 49. Ukija wamiliki wa simu *(handset)* wako kama milioni 56 na simu janja ni milioni 24 yaani simu zile ambazo si simu janja ni milioni 56 na hizi simu janja ziko milioni 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa nina hoja na hoja yangu ni kwamba kuwepo kwa upungufu mdogo wa kuwepo kwa simu za kawaida nyingi milioni 56 inaonesha kwamba bado Watanzania wengi hawatumii *internet* katika shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *internet* kama nilivyosema na uwepo wa simu janja ni suala la muhimu zaidi. Mimi ninachoamini kwamba simu janja kwanza ni muhimu katika suala zima la usalama. Mtu anayetumia simu janja ana *address* kuliko yule ambaye hatumii simu janja. Kwa hiyo, Serikali kwanza inatakiwa na inapaswa kuona namna gani tunaweza tukawapongeza watumiaji kwanza wa *internet,* vilevile kuongeza idadi ya simu janja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri amesema kuna kampuni kule Mkuranga tayari imekuja inataka kuja kuanza kutengeneza simu janja. Mimi nadhani tujitahidi ikiwezekana mwekezaji huyo apate *incentives* za kutosha ili kwamba tuweze kupata simu nyingi janja ambazo ni za bei rahisi ili kuondoa hii *gap* iliyopo kati milioni 56 na milioni 24 iweze kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile simu zinazoingia kutoka nje nazo tupunguze kodi lengo letu tuweze kupata Watanzania wengi wanaoweza kutumia simu janja na hivyo hivyo tutakuwa tume-*boost* kutumia *internet.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi labda tupate maelezo ya kitaalamu Waziri kama atashauriwa na wataalamu, ubaguzi uliopo kati ya wananchi wanaoishi vijijini watumie 3G wa mjini watumie 4G na 5G ni Watanzania wale wale, *discrimination gap* hii ya *internet* inatokana na nini? kwa nini mitandao sisi wa vijiji inaona tutumie 2G ambayo 2G hupati *internet,* 3G inakuwa kama

unapika ugali kwa kutumia kuni mbichi, *internet* ile unahangaika nayo sana. Kwa nini ubaguzi huo upo? Naomba Waziri aje atueleze namna ya ku-*fill* hiyo *gap.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCRA* itusaidie, kuna mitandao mingine *internet* yake ni nzuri, nyingine *internet* yake ni kama kuni mbichi unapopika chakula nayo ituambie na kama hivyo kwa nini hawa-*comply?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilikuwa naona tusiuziwe *internet bundle* kwa muda, kama nimenunua kifurushi kile acha nitumie. Kwa akili ya kawaida unavyosema nitumie kwa wiki halafu ikifika wiki kimeisha, mimi naona si sawa. Jambo hili na nadhani *TCRA* hii naomba iondoke katika *financial year* hii mimi sidhani kama kuna haja ya kwamba kuwe kuna muda wa matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naishukuru sana Serikali kwa maana ya minara tumepata katika majimbo yetu lakini mimi naona haitoshi. Kwa kasi ya matumizi ya simu na shauku ya wananchi, *UCSAF* imefanya kazi kubwa na najua inapata hela kutoka kwa *operators* ili minara iweze kujengwa. Mimi nadhani Serikali iangalie vyanzo vingine ili tuweze kupata ujenzi wa minara na ikiwezekana maeneo mengi yaweze kupata minara na hivyo kuimarisha na kuleta utengamano kwa ajili ya upatikanaji wa *internet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine zipo fedha zinapatikana kwenye simu za kimataifa wanaita *international terminating,* lakini kwenye *internet* nako kuna fedha. Nilitaka Waziri atuambie kwamba Serikali inapata kiasi gani kupitia huduma ya *international calls* vilevile na kwenye mitandao hii ya *internet* pia na mkongo. Mimi najua kwa mfano nchi ya Rwanda na Burundi sisi ni *gateway* yao *how much do we get* kutokana na huduma hiyo? Kwa hiyo na mkongo wetu wa Taifa je, unatupa faida gani ambapo kama ni *gateway* ya nchi zingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu wenzangu walivyoiongelea habari ya *stock exchange* kwa kampuni moja ya

simu kuwepo mle. Mimi nadhani hii ni sheria ya Wizara ya Fedha, *TCRA* naye ni kama *regulator.* Jambo hili mukhtadha wa Serikali iliangalie kwa mapana zaidi kwamba kama Wizara ya Fedha je, 25% ile ambayo inataka iwe kwenye *Initial Public Offer (IPO)* ina maana na inaathiri vipi kama uwekezaji wa makampuni mengine yanayotaka kuja kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali ituambie kwa nini Vodacom wameingia, hao wengine wamechukua miaka kumi na mbili hawajaingia? Hayo ni masuala yote yanaweza kuja kuelezewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na nashukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kenneth Nollo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaongeza muda hadi tukamilishe shughuli yetu.

Sasa ninamwita Mheshimiwa Ramadhan Suleiman, Mheshimiwa Naibu Waziri Maryprisca ajiandae.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji kwenye hoja iliyoko mezani leo iliyoletwa na Waziri wetu Mheshimiwa Jerry Silaa.

Mimi ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya kuleta mageuzi makubwa kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninachukua fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan, kwenye sekta hii amefanya mambo makubwa ambayo yameleta mageuzi makubwa. Tunapomsifia Mheshimiwa Rais, tunamsifia kwa kazi zake alizozifanya, na kazi alaizozifanya ziko kwenye takwimu, kwenye *statistics* kwa sababu tunazo

takwimu kwenye *finger tips* zetu za yale mamabo aliyoyafanya Mheshimiwa Rais baada ya yeye kuingia madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Tanzania tumetoka watumiaji wa *internet* milioni 29 mpaka milioni 49. Machi 2021 tu tulikuwa milioni 29, leo Machi 2025 tumefika watumiaji milioni 49 na ndiyo maana tunasema Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa kwenye sekta hii pia. Kutoka milioni 29 mpaka milioni 49 kwenye miaka yake minne tu ya utawala akiwa kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alisema hapa, sasa tunajenga minara ya simu zaidi ya 750 kwenye kata zaidi ya 713. Hayo ni maendeleo makubwa sana. Makubwa mno, kwa sababu ya kutaka sekta hii ya mawasiliano ikue, Mheshimiwa Rais amepambana kadiri ya uwezo wake kuhakikisha kwamba anawekeza fedha nyingi huku ili sekta hii ikue na ilete maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya *internet* sasa hivi siyo *luxury* tena, yameshakuwa sehemu ya maisha yetu kama vile tunavyohitaji chakula, tunavyohitaji nguo, tunavyohitaji nyumba za kuishi, pia kwenye maisha yetu ya kila siku tunahitaji matumizi ya mawasiliano, aidha kwa njia ya *internet* au njia ya simu kupiga au kutuma *sms*. Tunawasiliana kwa urahisi, tunatuma fedha. Hata *operation* sasa hivi hospitalini zinafanywa kwa njia hizi za *internet*. Hizi zote zimekua kwa sababu kuna uwekezaji wa makusudi umefanywa na uwekezaji huu moja kwa moja umeendelea kukuza uchumi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo limesemwa sana hapa ambalo na mimi ninataka niliseme, ninatoa ushauri wangu kama mwanasheria; jambo la uwekezaji wa wananchi kununua hisa kwenye Kampuni ya Vodacom.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipata kusikiliza mdahalo wa wadau wa mawasiliano uliofanywa na Mheshimiwa Waziri. Jambo hili pia liliibuliwa sana na baada ya kuibuliwa nikawa *curious* kutaka kufuatilia, nikasoma kidogo nikaenda kufanya tafiti, *research* kwenye sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyosemwa na wenzangu waliotangulia kuhusu jambo hili ni kweli. Wote walisema kwa usahihi sana, wote walisema kwamba kweli mwaka 2010 tulitunga sheria tukiwa na lengo na Serikali ilikuwa na lengo zuri kabisa. Lengo lake kipindi kile lilikuwa ni kuruhusu Watanzania kuumiliki uchumi wao, *locally ownerships*, tulikuwa tunataka *locally ownership*. Pia tulikuwa tunataka kuweka *transparency* kwa *telecommunication companies*, ili kuwe na uwazi wa *transactions* zao za biashara zinazofanywa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine ilikuwa tunataka kufanya *regulatory compliance* kwa sababu tulikuwa tunazo kampuni ambazo nyingi zinamilikiwa na wageni. Kwa hiyo, tulipitisha sheria hii ili kufanya *regulatory compliance*. Kwa hiyo, tulikuwa tuna lengo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji dada yangu Mheshimiwa Salome amezungumza kwa uzuri zaidi. Tulitunga sheria tukai-*enforce* zaidi kwa kutunga *Finance Act* mwaka 2016, tukaja tukafanya marekebisho mwaka 2022, lakini inavyoonekana Mheshimiwa Waziri ni kama vile kwenye kipengele hiki sheria hii kama vile imegonga ukuta. Siyo yote, siyo *EPOCA* yote, siyo *Electronic and Postal Communication Act* yote. Hii ni sheria nzuri kwenye maeneo mengine lakini hapa ambapo wachangiaji wenzangu pia walisema, inaonekana imegonga ukuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria kugonga ukuta inatokea, siyo mbaya, inatokea sana kwenye sekta ya sheria. Ni kama vile mnaitunga sheria halafu mnataka kui-*test*, inafanya kazi? Inaenda mtaani, sasa ikishafika mtaani ina malalamiko. Wenzangu wametoa malalamiko haya kwa mifano na mifano mingi imetolewa hapa kwamba kuna jambo linatakiwa lifanywe, kuna kitu tulikosea wakati wa kupitisha sheria hii. Tunaweza tukakiri tukarudi nyuma kama Taifa, kama nchi, kama Serikali, tukaja tukaleta marekebisho ili tuendelee mbele tujikwamue hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ninahisi tulikosea, kwa maoni yangu; moja ilikuwa ni kuweka ulazima. Kwa sababu,

kwenye kifungu cha 26(1)(a) kuna neno '*shall*' limetumika. Wanataka hao *internet sub-providers* ambao ndiyo *telecommunication companies* kwa ulazima zikiwa ni *private parastatals*. Unazichukuaje *private parastatals* (mashirika ya *private)* ukazilazimisha kwa sheria yaingie kwenye soko la hisa? Soko la Hisa kampuni zinaamua zenyewe kulingana na *market*. *Market force* inavyokwenda ndiyo zenyewe zitaamua au bodi zao zikishakaa huko zikafanya *decisions* za kwamba tunataka ku-*raise capital (investment capital)*. Kwa hiyo, kama tunataka tu-*raise* na hatuna hela, hatuwezi kukopa, *lets sell our shares* ili tupate *shareholders,* waingie, watupe fedha, tukawekeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tuliweka kipengele cha ulazima wa kisheria kulazimisha hizi kampuni ziingie zika-*list* kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam? Hapo ni moja kati ya kosa tulilolifanya, lakini tunaweza tukarudi nyuma tukatoa hicho kipengele cha ulazima, tukaziacha zi-*operate privately*. Hizo kuhusiana na *regulatory compliance, transparency* zitaendelea na tutaendelea kuzitunza kwenye *regulation* nyingine, kwa sababu tunazo sheria nyingine tutawatungia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kosa lingine tulilolifanya ilikuwa ni kuwazuia wawekezaji wa kigeni kipindi kile wasizinunue hizi *shares* ambazo tulikuwa tunazisema. Tulivyowazuia ndiyo maana hiyo *drop* ya *value* ya *share* ilitokea ambayo hawa watu wanaisema hapa ilitoka shilingi 800 mpaka shilingi 200 kwa sababu sasa huna *foreigners* wanaoweza kuja ku-*chip in* kuongeza mitaji, na Watanzania hawanunui tena. Kwa hiyo, kulikuwa na makosa yaliyotokea ambayo tunaweza tukajirekebisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, Serikali nendeni mkakae mfikirie jambo hili, mje na msimamo au maamuzi ya kwamba tunaweza tukaondoa kipengele hiki ili Vodacom waka-*delist*, wakae na *shareholders* wao waliozinunua, waki-*delist* watapatana wenyewe kwamba ngoja tutawarejeshea fedha zenu ili *shares* zirudi kwetu tu-*operate* maisha yaendelee. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndiyo ulikuwa ushauri wangu kwenu. Ninashukuru sana kwa kunisikiliza na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususani barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na

pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na taarifa ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, inaonesha kuna mafanikio makubwa kwenye sekta za Mawasiliano na Teknolojia ya Habari hasa katika mikakati ya kupunguza gharama za mawasiliano kwa wananchi. Utendaji kazi ulilenga pia kuboresha miundo ya TEHAMA kuwezesha mwelekeo mzuri wa kuleta ubunifu ili Tanzania iendane na kasi ya dijitali ya kiuchumi *(digital economy)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza msukumo mkubwa kwenye kuendeleza maboresho ya mtandao wenye kasi zaidi na kuhakikisha matumizi mazuri ya *Data Center* ili kuwezesha ubunifu wa miundombinu ya TEHAMA hasa Serikalini iweze kusomana. Kutokana na kuwepo mifumo tofauti kwenye taasisi za Serikali ni muhimu sana kuunganisha mifumo yote iweze kusomana ili kuleta ufanisi unaoendana na dunia ya leo. Mwelekeo wa dunia ya leo ni kufanya shughuli zote za kitehama, nashauri Serikali kuboresha

muundo wa Wizara na taasisi zake ili kuwepo na idara mahususi itakayoongozwa na Afisa TEHAMA Mkuu *(CIO)* ngazi ya Kamishna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa muunganiko wa mifumo yote *(Core Government System),* ni muhimu kuboresha *e-government* na itawezesha ufanisi na kupunguza gharama kwa kiasi kikubwa sana. Kuwepo kwa Mkongo wa Taifa na *Data Center* ni fursa kwa kuwezesha kutengeneza mfumo wa kuratibu na kuendeleza ubunifu katika TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia imewezesha huduma ya kifedha juimishi *(financial inclusion)* na hii fursa pia kwa Serikali kuratibu miamala ili iwe sehemu ya mfumo rasmi wa malipo kwa usimamizi wa Benki Kuu na *TCRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza maboresho kwenye tozo za miamala itayoongeza mapato ya Serikali, lakini ikizingatia kupunguza mzigo kwa wateja. Serikali kwa kushirikisha wadau, itumie uzoefu wa sasa kuboresha huduma za miamala kwa kuoanisha ufanisi kwa huduma ya kifedha juimishi na tozo mbalimbali na mchango wa huduma hii kwenye kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio makubwa ya utekelezaji wa Wizara ikiwemo zoezi la postikodi, bado kuna maeneo mengi ambayo bado hayajapata huduma za minara ya mawasiliano na hata kwenye maeneo kadhaa yenye minara katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya hayapati huduma ya mawasiliano. Vijiji vingi ikiwemo katika Kata za Ulenje, Iyunga Mapinduzi, Mshewe, Mjele, Ilembo na Ihango havina minara na vingine kuna minara ambayo kwa muda mrefu haina mawasiliano. Kwa kuzingatia lengo la kupeleka TEHAMA kwa kila shule, Serikali iharakishe kujenga minara maeneo yote kwenye vijiji na vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kupitia Tume ya TEHAMA iweke msukumo zaidi wa ujenzi wa vituo vya kukuza bunifu za TEHAMA kwenye mikoa na wilaya zote za Tanzania. Serikali iendelee kutenga fedha kupitia Mfuko wa Mawasiliano

kwa Wote ili kutekeleza azma ya ujenzi wa minara zaidi nchini kote. Pia Serikali iboreshe usikivu kwenye minara yenye changamoto za usikivu na msukumo uwe kuwekeza kwenye mifumo ya 4G na hata 5G kwa mijini mpaka vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)* likamilishe mradi wa ufikishaji Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye nchi jirani zinazotuzunguka ikiwa ni sehemu ya kuboresha mawasiliano na wakati huo huo kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ifanye maboresho ya Mfumo wa *NaPA* ambao ni mfumo wa kidigitali wenye kanzidata ya anwani za makazi. Uboreshaji wa *NaPA* uwezeshe mfumo kusomana na mifumo mingine ya Serikali ikiwemo, mifumo ya ukusanyaji mapato ya *TRA* na hata mfumo wa *TAUSI* unaotumika na TAMISEMI kukusanya kodi ya majengo. Pia maboresho yawezeshe upatikanaji wa huduma za anwani za makazi kupitia *USSD code* na kuwezesha wananchi kutuma maombi ya kupatiwa anwani ili kurahisisha upatikanaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Jerry William Silaa (Mb.) na Naibu wake Mheshimiwa *Engineer* MaryPrisca Mahundi (Mb.), Katibu Mkuu Ndugu Mohamed Khamis Abdallah, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Nicholaus Merinyo Mkapa na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kwenye changamoto kwanza za udanganyifu unaofanywa na matapeli wa mitandaoni; pili, huduma za mawasiliano na kupata habari kwa watu wenye ulemavu wa usikivu (viziwi) na tatu, tatizo la mawasiliano katika baadhi ya maeneo ya jimbo langu la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza utahusu tatizo la changamoto ya udanganyifu unaofanywa na matapeli wa mitandaoni kwa kutumia namba zilizosajiliwa na makampuni yetu ya simu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa jitihada ilizochukua kuzuia uhalifu na ulaghai wa mitandaoni kupitia Kampeni ya SITAPELIKI na kutoa elimu kwa umma kuhusu usalama wa mitandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali, bado kumekuwa na wimbi kubwa la mashambulio ya mtandaoni ambapo maharamia huingilia *accounts* za wateja za *whatsApp* au zile za kawaida kwa kutumia namba zilizosajiliwa na makampuni yetu ya simu hapa Tanzania na kutuma *sms* za kutapeli. Pia kumekuwa na wimbi la matapeli kupiga simu na kufanya udanganyifu wa kuomba pesa kwa kusingizia kutumwa na watu maarufu au wenye majina wakubwa au kwa kutumia vishawishi vikali vya kumhadaa anayetapeliwa. Kwa kiasi kikubwa uharamia huu bado unaendelea na umekuwa ni kero kubwa kwa Watanzania wanaotumia huduma za simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limewaliza Watanzania wengi kwani wamepoteza kiasi kikubwa cha fedha. Kwa hali ilivyo sasa, usalama wa taarifa za simu zetu huko mitandaoni na ulinzi wake wa faragha ni shida kubwa inayokabili wateja wengi wanaomiliki simu hapa nchini Tanzania. Hivyo basi kuna umuhimu wa kuongeza juhudi kukabiliana na changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hii, sasa ni wakati muafaka wa Serikali kufanya maboresho ya sheria zilizopo au kuanzisha sheria na sera za usalama wa mtandaoni. Serikali inapaswa kuanzisha sheria kali na sera zitakazolinda ulinzi wa taarifa za watu mtandaoni. Kwa mfano, kwa kuwa matapeli hufanya uhujumu kwa kuibia wateja fedha zikiwemo za Serikali, basi watakaonaswa katika uhalifu wa aina hii washtakiwe kwa kosa la kuhujumu uchumi. Sheria kali kama hii itasaidia kupunguza uhalifu wa mtandaoni na kuongeza imani ya watu katika kutumia huduma za kidijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili unahusu huduma ya mawasiliano na kupata habari kwa watu wenye ulemavu wa usikivu (viziwi) nchini Tanzania; viziwi ni moja kati ya makundi ya watu wenye ulemavu wanaohitaji huduma maalumu kwenye mawasiliano ili waweze kuendana na mambo mbalimbali. Matatizo waliyonayo viziwi huwakwaza kupata mawasiliano katika mazingira wanayoishi na hivyo kuwaathiri kupata haki yao ya elimu, ajira, mahusiano katika jamii na maisha yao kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo ya viziwi ni ya kimawasiliano, viziwi wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la kusahaulika katika utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali iwekeze kikamilifu na kuweka miundombinu na rasilimali watu ya kutosha ili kundi hili lipate haki yao ya msingi ya kupata mawasiliano na jamii inayowazunguka. Viziwi wakishatambulika katika jamii, wapelekwe katika shule zao maalumu na wapatiwe elimu ya alama au ya aina nyingine ile itakayowasaidia kwenye mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikakati ya muda mrefu ya kukabiliana na changamoto hii, ni vyema lugha ya alama ifundishwe kama somo kwa wanafunzi wote kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu ili kurahisisha mawasiliano kwa viziwi pote nchini. Hii ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa vifaa wezeshi vinavyohusisha lugha za alama kwa kutumia kitafsiri janja cha viziwi katika kusanyiko na kitafsiri janja cha viziwi cha mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa tatu utahusu tatizo la mawasiliano katika baadhi ya maeneo ya jimbo langu la Moshi Vijijini. Kwanza kabisa niishukuru Serikali kwa jitihada kubwa za kupeleka mawasiliano karibu na watu kwani hapa nchini imejengwa minara 758 na kuiongezea uwezo minara 304 kutoka 2G kuwa 3G. Naishukuru Serikali kwani katika Jimbo la Moshi Vijijini nimejengewa minara katika Kata za Mabogini, Kibosho Kati, Kibosho Magharibi na Uru Shimbwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na huduma ya kujengewa minara niliyoainisha hapo juu, bado kwenye jimbo langu kuna maeneo yenye changamoto kubwa ya mawasiliano. Hii imetokana na maeneo haya kutokuwa na mvuto wa kibiashara, na mashirika ya kibiashara *(Mix by YAS, Vodacom, TTCL, Halotel, Airtel)* hayajawekeza kujenga minara ya mawasiliano kwenye maeneo haya. Maeneo haya ni yale yanahusisha vijiji vinavyopakana na Mlima Kilimanjaro katika Kata za Kimochi, Mbokomu, Kibosho Mashariki na Oldmoshi Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kupitia kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote iwekeze na kujenga minara ya mawasiliano katika maeneo haya. Kata hizi ni za kimkakati kwani baadhi zina vivutio vya watalii na baadhi kuna njia za kitalii kupanda Mlima Kilimanjaro. Ni muhimu watalii wakiwa katika maeneo haya waweze kutumia simu zao kwa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba kutokana na kushamiri kwa uhalifu wa mitandaoni hapa Tanzania, ni muda muafaka wa kuboresha mazingira ya kisheria na sera ili kulinda taarifa za wateja huko mitandaoni. Kwa kuwa viziwi wamekuwa wahanga wa kutopata huduma stahiki za kijamii hapa nchini, Serikali ichukue hatua za makusudi za kuhakikisha viziwi wanaweza kufanya mawasiliano na jamii inayowazunguka kwa sababu mpaka sasa viziwi wengi wana changamoto kubwa. Teknolojia ya kuwasaidia viziwi kufanya mawasiliano si anasa bali ni haki yao ya msingi na daraja la kuwapatia usawa katika jamii. Mafanikio ya hili jambo litawaongezea matumaini, heshima na nafasi ya kujitegemea. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa maendeleo ya kiteknolojia yanamfikia kila kiziwi bila kumwacha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natangulia kumshukuru Mhashimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwekeza miradi mikubwa ya mawasiliano ya simu za mkononi kupitia

maradi wa minara 1,494 *(758 plus 636)*. Nakupongeza Mheshimiwa Waziri Jerry Silaa na Naibu wako Mheshimiwa Maryprisca Mahundi kwa kazi nzuri mnazozisimamia katika Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipoingia madarakani na kuwa Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini jumla ya vijiji 22 havikuwa na mawasiliano ya simu za mkononi. Ndani ya miaka minne jumla ya vijiji 13 vimefikiwa na huduma za mawasiliano ya simu za mkononi. Jumla ya vijiji vinne vya Nandete, Mwengei, Chapita na Pungutini vilifikiwa na mawasiliano ya simu za mkononi ya minara ya *TTCL* ya 3BG mwezi Agosti, 2021. Minara na Madishi ya GB4 na 5 ya Tigo na Airtel katika vijiji vya Kandawale/Namatewa, Kipindimbi, Mkarango na Chumo. Minara hi imeongeza mawasiliano ya simu za mkononi katika vijiji kumi na vitatu. Aidha ipo miradi inayoendelea katika vijiji ya ujenzi wa minara ya *TTCL* na Tigo. Vijiji hivyo ni MT Kimwaga (Narayan), Miumbu/Mtyalambuko, Zinga Kibaoni (Nambunju), Marendego, Kandawale, Miguruwe/Mtepela na Ingirito. Miradi hi imepangwa kukamilika mwishoni kwa mwezi Mei, 2025. Itakapokamillika jumla ya vijiji 18 vitakuwa vimefikiwa na mawasiliano ya simu za mkononi ndani ya kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan na vitabaki vijiji vinne vya Hanga, Ngarambi, Nambondo na Mtende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri kwa Serikali; kwanza minara ya GB3 ya *TTCL* Nandete, Pungutini, Chapita na Mwengei ifungwe mitambo ya GB 5/4.

Pili, vijiji vinne vya Hanga, Ngarambi, Nambondo na Mtende vipelekewe miradi ya minara ya simu za mkononi ili kumaliza changamoto ya mawasiliano ya simu za mkononi; tatu, mnara wa mawasiliano ya redio wa Nangurukuru ukamilishwe na mnara wa redio wa Mlima Kitope uboreshwe ili kuimarisha mawasiliano ya redio Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, nakuomba Mheshimiwa Waziri tuambatane pamoja tukazindue mnara mmoja wa Kipindimbi

mara baadaya Mheshimiwa Rais kufanya uzinduzi wa Kitaifa wa minara 758.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mungu anayeendelea kinijalia afya na nguvu za kuendelea kuwatumikia Wana-Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa na nzuri kwenye sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari bila kuwasahau wasaidizi wake Naibu Waziri pamoja na watendaji wa Wazira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya simu na redio; naipongeza Serikali kwa kuendelea kuboresha mawasiliano ya simu kwenye maeneo mengi Wilayani Kyerwa. Kyerwa kulikuwa na shida kubwa ya mtandao wa simu ikiwemo *internet,* sehemu nyingi ulikuwa ni mawasiliano kutoka nchi jirani za Rwanda na Uganda, lakini kwa sasa hali ni nzuri kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo bado mawasiliano ya redio zinazosikika ni za nchi ya Rwanda na Uganda, niombe sana Serikali kukamilisha mtambo wa redio ili Wana-Kyerwa na wao wasikie matangazo na taarifa mbalimbali zinazohusu nchi yao, hii iwe sambamba na kuboresha mtandao pale makao makuu ya Wilaya ikiwemo kujenga minara maeneo yote yenye shida na mawasiliano ambayo tayari yalishaainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wizi wa kwenye mtandao; pamoja juhudi zinazoendelea kuchukuliwa bado wizi wa kwenye mtandao ni mkubwa sana, najuliza inakuwaje mtu anakupigia kwa namba unayoijua anakuomba pesa kwa namba hiyo hiyo na ukituma pesa inaleta jina halisi la mwenye namba ila baadae ukifanya mawasiliano na mwenye namba anakuambia hajakuomba hela!

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu wanawezaje kuchezea namba ya mtu bila kuwa na mtu kutoka kampuni ya simu na wanajuaje kwenye simu yako kuna salio kama hana mtu anayewasiliana naye kutoka kampuni ya simu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi juu ya huo wizi wa kwenye mtandao na ni hatua zipi zinachukuliwa kwa wizi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchafu kwenye mitandao ya kijamii; kumekuwapo na mmomonyoko wa maadili kwenye mitandao ya simu, ukifungua mtandao wowote wa kijamii unakutana picha chafu zinakuja zenye uchafu wa kutisha, watoto wetu tunawapeleka wapi? Tunaandaa kizazi cha kingono ngono, kizazi cha uzinzi, hii ni hatari kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua Serikali imejipangaje kudhibiti uchafu huo kwenye mitandao ya kijamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na ahsante.

**MHE. MWANTUM M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kunifanya niweze kutekeleza majukumu ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uchapakazi wake na kuendelea kutatua changamoto za Watanzania katika nyanja zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa uchapakazi wao na niendelee kuwapongeza sana kwa namna mnavyoendelea kupambana kutatua changamoto za mawasiliano katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye baadhi ya maeneo yetu bado kuna changamoto ya mawasiliano, kwa mfano katika maeneo ya Masagalu, Jimbo la Kilindi, Magoroto Jimbo la Muheza na maeneo ya Tanga Mjini. Niendelee kuiomba Wizara, muendelee kutukumbuka katika programu yenu ya minara 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishauri Wizara kuhakikisha maeneo yote ya taasisi za Serikali kama shule, hospitali, halmashauri na kadhalika yanakuwa na mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Tekenolojia ya Habari, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, awali ya yote ninapenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema ambaye ameendelea kutusimamia na kutuongoza vyema, tumeweza kutimiza majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani kubwa aliyoonyesha juu yangu. Ninasema ahsante sana mama, hakika nami sitamwangusha. Nitaendelea kufanya kadiri ya maagizo ninayopewa, lakini vilevile kwa mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, naye pia amekuwa ni mlezi mzuri, Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa na Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko. *(Makofi)*

Pia ninapenda kumshukuru Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muugano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa maelekezo yake, miongozo, ya namna njema ya kuweza kuwahudumia wananchi kwa kupitia Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Waziri wangu Mheshimiwa Jerry Silaa, naye pia amekuwa ni kiongozi mzuri kwangu na ameweza kunipa nafasi ya kufanya kazi na kuweza kumsaidia pale ilipobidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisimsahau Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge, namna nzuri mliyoifanya kutuwezesha sisi kama Mawaziri kutekeleza majukumu yetu, lakini vilevile kuweza kufanya kazi kwa ukaribu na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote na ninawashukuru sana kwa namna ambavyo mmekuwa na msaada mkubwa katika kutimiza majukumu yangu. Mmeweza kuniuliza maswali mengi nimewajibu, tumeweza kufanya mawasiliano nje ya *podium* na tumeweza kuhakikisha tunatoa huduma njema kwa wananchi. Waheshimiwa Wabunge, hongereni na asanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwa namna ambavyo michango iimeendelea katika kuwezesha bajeti yetu hii; ninawapongeza wote kwa namna njema mlivyochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda kuchangia kidogo sana na kuacha sehemu kubwa Mheshimiwa Waziri Jerry ataendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninapenda kuwashukuru kwa namna ambavyo mmekuwa msaada katika kuona kwamba hasa hii minara 758 na minara 636 tunaweza kuitekeleza katika majimbo yenu. Wakati wote mliponihitaji mliniomba na mimi niliweza kufika, tulishirikiana na tumeweza kuweka imani kubwa kwa wananchi kuona kabisa namna ambavyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kuipa nguvu Wizara yetu na kuhakikisha suala la mawasiliano linapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwatoe hofu, yale maeneo machache ambayo bado hatujayafikia, tutakuja kuhakikisha minara inajengwa na mawasiliano yanaimarika. Maeneo ambayo tuna minara ile ya zamani tunakuja ku-*upgrade* kuona kwamba lile suala la matumizi ya 3G, 4G liwe kwa wote. Hayo ndiyo malengo ya Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninapenda kuongelea suala la ulaghai mitandaoni na hili limekuwa janga kubwa sana. Ninawapa pole sana wale Waheshimiwa Wabunge ambao pia yamewahi kuwakuta. Suala hili si laana, ni suala la kumshukuru Mungu, ni suala la kumshukuru Mheshimiwa Rais, ni ukuaji wa teknolojia. Tatizo la Watanzania ni matumizi yasiyo sahihi ya ukuaji wa hii teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tutaendelea kuhakikisha tunafanya kazi kwa ukaribu na Wizara ya Mambo ya Ndani, kuona kwamba hawa wote ambao wanakwenda kinyume na matumizi sahihi ya teknolojia ambayo imekua sana hapa nchini, lakini ni mapenzi mema ya Mheshimiwa Rais aliyeruhusu fedha nyingi iweze kutumika na kuona kwamba tunaweza kusimika mifumo ambayo inaenda kutusaidia kuboreka kimaisha, lakini vilevile kiuchumi, kielimu, kiafya. Inaendelea kutusogeza katika mabadiliko makubwa ambayo dunia inataka, lakini vilevile kuona kwamba wananchi pia wananufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu kwa wananchi wote, ninapenda tu kusema kwamba wananchi wote tuwe makini katika matumizi ya ukuaji huu wa teknolojia. Kila mmoja kwanza anapaswa kuwa makini, lakini vilevile kila mmoja anatakiwa atambue angalau vitu ambavyo anaweza kuvitumia wakati wa matumizi ya teknolojia, na kila mmoja aweze kulinda taarifa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais ameweza kutupa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, lakini na sisi wenyewe lazima tulinde taarifa zetu. Usitoe neno lako la siri kwa mtu yeyote yule, lakini vilevile usitoe taarifa zako kwa mtu yeyote yule ambaye hapaswi kuzichukua, lakini kubwa, usijibu *message* ambayo hujui nani aliyekutumia, wala usifanye malipo yoyote kwa mtu ambaye humfahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kusisitiza hili kwa wananchi wote, lengo ni kuona kwamba hakuna ambaye ataendelea kutapelika na ndiyo maana tumeendelea kuleta semi mbalimbali ambazo zitatusaidia kila mmoja akumbuke. Kwa hiyo, kila mwananchi akiweka kwenye akili yake na moyo wake

kwamba sitapeliki, maana yake hakuna ambaye atatapelika, hakuna ambaye atafanya vitu tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Waziri anakwenda kuongea kwa urefu, mimi niseme nimeona tu niongelee kwa ufupi masuala ya minara, lakini masuala yanayoendelea yasiyofaa kwenye mitandao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninapenda kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Mbeya kwa kunipa nafasi hii adhimu. Heshima kubwa waliyonipa wanawake wa Mkoa wa Mbeya ninasema tu kwamba nimejitahidi kufanya kadiri ya uwezo wangu na Mungu amenifikisha hapa, lakini tarehe 28 Juni na mimi nitakwenda kuchukua fomu kwa dhamira ya kuendeleza maendeleo ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni muumini wa siasa na uchumi na tumeshaanza kufanya mwanzoni hapa. Ninaamini sasa kwa *phase* inayofuata tutakwenda kufanya mambo makubwa sana na wanawake wote wa Mkoa wa Mbeya tutakwenda kuimarika kiuchumi zaidi, ambapo itatusaidia kiafya, lakini vilevile katika kuimarisha familia zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo kwa ufupi, ninashukuru sana kwa hii nafasi, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Sasa nimwite mtoa hoja Waziri, Mheshimiwa Jerry Silaa, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi ninaomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa kibali cha kusimama hapa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru wewe binafsi kwa kutuongozea kikao hiki vizuri. Umekuwa ukifanya hivyo mara nyingi

tunaposimama hapa. Kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Wizara na wewe ninakuombea Novemba tukutane hapa na tunaamini kwa jinsi ulivyokuwa ukiongoza vikao vyetu, Waheshimiwa Wabunge watakurejesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi zaidi ninaomba nipongeze, tumepata wachangiaji 11 na mchangiaji mmoja wa maandishi, Mheshimiwa Luhaga Mpina, ametuletea mchango wa maandishi. Wachangiaji wengi wamepongeza sana na kushukuru kazi kubwa iliyofanywa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, minara ya simu inajengwa; ipo ile 758 ambayo ilikuwa inakamilika tarehe 12 Mei, imebaki michache. Alisema Mheshimiwa Sanga, ya maeneo ya hifadhi, maeneo ambayo mvua zimeathiri barabara. Iko minara 636 imeanza kujengwa na kuna awamu nyingine ya 11 ambayo tayari zabuni imetangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme mbele ya Bunge lako, shukrani na pongezi zote hizi zimwendee Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye yeye hasa ndiye kinara wa utekelezaji wa *digitalization* ya nchi yetu. Amekuwa akituelekeza, amekuwa akitupa fedha na amekuwa akihakikisha miradi hii inakamilika. Vilevile ninawashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha yanafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata maelekezo na maoni ya taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge. Ninakuthibitishia kwamba maoni na maelekezo yale yote tutayatekeleza. Masuala ya *startups*, masuala ya *Digital Technology Institute*, masuala ya ujenzi wa *Data Centre*, masuala ya kujenga zile *incubation hubs* za *startups*, masuala ya kuitumia Maabara yetu ya Vifaa vya TEHAMA vizuri, yote tutayatekeleza na tutapeleka utekelezaji wake kwa maandishi kwenye Kamati ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu kwa kifupi nisemee maeneo matatu; Waheshimiwa Wabunge wote wamechangia

vizuri na maeneo yote nikiri kwamba tumepokea na kwa sababu Wizara hii ni Wizara ya TEHAMA, tutawajibu. Tutawajibu kwa maandishi, lakini ninaomba niyasemee maeneo matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni Waheshimiwa Wabunge waliochangia kuhusu *cashless economy*. Ninawathibitishia kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mradi wa *Digital Tanzania Project (DTP)* ni kuhakikisha mifumo inasomana na kazi kubwa imefanyika. Unaposikia *Jamii Exchange* ni mfumo ambao utasaidia taasisi zote za Serikali na binafsi kubadilishana taarifa na kwenye hotuba yangu nimeelezea mifumo ambayo imeshakwisha kusomana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kupitia *Jamii Pay* tunatengeneza *platform* ambayo itafanya kile alichosema Mheshimiwa Mtaturu na Waheshimiwa wengine, *cashless economy* na kwenye *Jamii Pay* ipo ile kadi iliyokuwa inaitwa *N-Card* ambayo sasa itakuwa ni *Jamii Card,* ambayo itakuwa *both physical card* lakini vilevile tunatengeneza *soft card*, ili taasisi zote binafsi na za Serikali ambazo zina nia ya kufanya malipo zipitie kwenye *platform* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, jana alitembelea *NIDC* pale Dar es Salaam na amejionea mafanikio makubwa ya kazi inayofanywa na Wizara kwa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni matumaini yangu kwamba katika kipindi kifupi kijacho Bunge lako hili likitupitishia bajeti yetu likatupa kazi hii, tutaenda kuifanya kwa kasi na weledi wa hali ya juu na kuhakikisha tuna-*integrate* miamala ya simu, benki, kupitia mifumo ya *BOT* ili tuwe na *cashless economy* na ndio njia pekee ya kuwa na Taifa la watu ambao unaweza kuwajua wapo wapi, Mheshimiwa Bashe leo akitaka kugawa mbolea agawe kwenye mfumo wa pamoja, mikopo ya elimu ya juu ipatikane pamoja, watoto wapangiwe miradi ya elimu pamoja, ndio *unified* jamii *data lake* tunaenda kuitengeneza, na ndio kazi tunayoenda kuitekeleza bajeti hii ikipita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ninataka kulisemea kwa kifupi ni suala la utapeli na ulaghai mitandaoni. Amesema vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri kuna Kampeni ya Sitapeliki, pia juzi tulizindua mfumo ambao ume-*base* kwenye *artificial intelligence* wa Kampuni ya Airtel ambao unatoa *sms alert* kwa sababu *message* nyingi zile za kilaghai ni *message* ambazo akili unde inaweza ikazing'amua na kuweza kuwatahadharisha watumiaji. Nilitoa wito kwenye shughuli ile, lakini ninaomba kutumia Bunge lako Tukufu kuendelea kutoa wito kwa kampuni nyingine kuja na *solution* za kibunifu, ili tuweze kuwalinda watumiaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza vizuri Mheshimiwa Salome tunaenda kwenye uchaguzi. Kupitia akili mnemba/unde *(artificial intelligence)* zipo *video* na sauti zinatengenezwa. Hotuba ninayoitoa hapa kesho mtu anaweza akatengeneza picha ya *video* niliyopo hapa, lakini ninachozungumza anaweza akakitengeneza kwenye akili mnemba nikazungumza maneno tofauti kabisa ninayozungumza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuthibitishie sisi ni wanachama wa *ITU (International Telecommunication Union)*. Ukisoma *global security inde*x iliyotoka Septemba 2024, Tanzania ni nchi ya tatu kwa usalama wa mtandao na tumewekwa kwenye *Tier One* ya usalama wa mtandao. Kwa hiyo, niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu kwmaba, *TCRA* imejipanga na nitoe wito ama onyo kwa Watanzania, wale ambao wanajiona wanapenda kutumia mitandao kwa namna ambayo ni hasi, wengine wanatumia picha ya mtu wanaituma kwa *grok* wanamwambia hebu tuvulie nguo, tuchezeshee mziki, tunayo mitambo ya kisasa.

Niseme kupitia Bunge lako, sheria zipo na niwaelekeze *TCRA* waongeze umakini kuwalinda Watanzania, wananchi na viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa ambao wanaeda kwenye chaguzi kuwasaidia wananchi wafanye uchaguzi katika hali ambayo itakuwa haijaingiliwa na mitandao hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu limesemwa hapa na Waheshimiwa Wabunge wengi juu ya *mandatory listing* kwenye *stock exchange* kwa kampuni za simu na kampuni nyingine za TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kukiri kwamba tumesikia, Serikali imesikia na imepokea. Kwa uchungu mkubwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia wamenirudisha mimi darasani kwenye darasa la *MBA* kwenye *Corporate Finance, how to raise capital,* jinsi ya kuweza kuendeleza mitaji kwenye kampuni na njia hii kama alivyosema Mheshimiwa Kapinga ninaamini ilikuwa ni nia njema ya Serikali kwamba umma wa watanzania umiliki uchumi wa kampuni hizi za simu. Kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge kwamba kilichoenda kutokea inaonekana ni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri tumelipokea na ninaomba niahidi mbele ya Bunge lako kwamba kwa dhati kabisa nimechukua hoja hii kwa uzito kama Waheshimiwa Wabunge walivyowasilisha hapa. *(Makofi)*

Mimi ninawaomba watuamini na waniamini, tulichukue nikitoka hapa ninathibitisha na kuomba kusema tena nikitoka hapa muda huu nitakaa na wenzangu Wizara ya Fedha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali tukae na wadau tuliangalie na tutafute *solution* ya jambo hili bila kuathiri wananchi wetu na sheria za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru tena kidhati, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, lakini pia ninaomba nimshukuru tena Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye imempendeza nimsaidie kazi kwenye hii Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Ninaomba niendelee kumuahidi kwamba imani yake nitailipa kwa kazi. Nitaendelea kufanya kazi kwa bidii katika kuhakikisha mkitupitishia bajeti hii tunaenda kufanya kazi kubwa ya kuhakikisha masuala haya ya *communication* na *ICT* tunayafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niendelee kuwashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi anayoifanya kunisaidia, Katibu Mkuu, watendaji, wadau wetu, makampuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niendelee kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ukonga. Sisi tunaopata fursa ya kufanya kazi ya kumsaidia Mheshimiwa Rais tunatumia muda mwingi kuwatumikia Watanzania wote. Niwashukuru wananchi wa Jimbo la Ukonga kwa uvumilivu wao, dua zao, na kunistahimilia pale ambapo nitakuwa ninatekeleza majukumu ya kiserikali. Ninaendelea kuwaahidi siku zote *interest* ya Ukonga itakuwa moyoni mwangu na nitaendelea kuwahudumia kuhakikisha maendeleo yale ambayo Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyapanga kuyatekeleza yataendelea kutelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo ninaomba sasa kwa heshima, taadhima na unyenyekevu mkubwa nitoe hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jerry Silaa, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa hitimisho hilo ambalo ninaamini Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wameelewa vizuri sana.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

*Hapa (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…….........…..............Sh. 2,850,174,296

**MWENYEKITI:** Katibu kwa muda uliokuwa umeongezwa na Mwenyekiti, tusome kwa mafungu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…..............................Sh. 2,850,174,296
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…..............Sh. 719,746,276
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……...……Sh. 4,421,171,276
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……………………..Sh. 432,429,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*...............................Sh. 409,151,000
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*.....Sh. 577,585,000
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*........Sh. 515,176,276
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh. 562,514,502
Kifungu 2001 – *Communication Division*..................Sh. 1,414,035,432
Kifungu 4001 – *Information Services Department*........................Sh. 0
Kifungu 4002 – *ICT Systems Development and Services Division*.............................................Sh. 1,355,208,273
Kifungu 4003 – *Communication Safety and IT Security Unit Division*..........................................Sh. 484,761,669
Kifungu 4004 – *ICT Infrastructure Unit*..........................Sh. 743,703,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…............…Sh. 55,330,905,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……………..................…Sh. 450,000,000
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*….Sh. 300,000,000
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*……………Sh. 0
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*….....Sh. 2,800,000,000
Kifungu 2001 – *Communication Division*….....…..Sh. 157,820,320,208
Kifungu 4001 – *Information Services Department*….....................Sh. 0
Kifungu 4002 – *ICT Systems Development and Services Division*……......................................……Sh. 36,146,257,792
Kifungu 4003 – *Communication Safety and IT Security Unit Division*………........................................….Sh. 2,800,000,000
Kifungu 4004 – *ICT Infrastructure Unit*……...........……Sh. 21,400,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Mtoa hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, ninaomba kutoa Taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake. Ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana.

Sasa nitawahoji hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia na Habari, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Mawasilino na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Hakuna, wote mmeafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Mawasilino na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwahoji sasa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Kwa kusema hivyo nitumie pia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote chini ya Wizara hii kwa kupitishiwa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yenu na tunawatakia kila la kheri kutekeleza yale yote ambayo mmeyaahidi. Pia Wabunge

wamechangia mambo mbalimbali hapa, Mheshimiwa Waziri umesema unaenda kuyafanyia kazi, tunakutakia kila la kheri na tunaamini yatafanyiwa kazi kwa ajili ya kuhakikisha changamoto hizi zilizosemwa kwa niaba ya wananchi basi zinapatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Pia Mwenyekiti wetu wa Kamati inayosimamia Wizara hii na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii tunawashukuru sana kwa kuendelea kusimamia vizuri Wizara hii, ili iendelee kutoa huduma zile zinazotarajiwa. Waheshimiwa Wabunge wote mmetoa mawazo mbalimbali na ninyi pia tunawashukuru sana. Kwa ujumla wetu sisi sote basi kila mmoja kwa ushiriki wake, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.30 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 19 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*